

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Tatu – Tarehe 5 Desemba,
2013**

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, leo ni siku ya Alhamisi, ni siku maalum kwa maswali kwa Waziri Mkuu. Naona leo hamkushabikia sana na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani hayupo. Kwa hiyo, nitaanza kiongozi, wewe upo tu umekaa kwenye kitu. Mheshimiwa Eng. Mohammed Habibu Mnyaa atakuwa mwulizaji wa swali la kwanza.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ENG. MOHAMMED H. J. MNYAA]

MHE. ENG. MOHAMMED H. J. MNYAA: Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii adimu na adhimu ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, liko jambo ambalo limeleta mabishano katika jamii ya watu wa Tanzania. Bahati nzuri hili jambo ni la kikatiba, lakini pengine wengine hawafahamu. Sasa labda kwa kuwa ni jambo la kikatiba, niombe ninukuu hilo jambo halafu nikuulize swali langu.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 43 inayozungumzia masharti ya kazi ya Rais, Sheria ya 1934 na Namba 15 ya Ibara ya 9. Nanukuu: "Rais atalipwa mshahara na malipo mengineyo, na atakapostaafu atapokea malipo ya uzeeni, kiinua mgongo au posho kadiri itavyoamriwa na Bunge na mshahara. Malipo hayo mengineyo, malipo ya uzeeni na kiinua mgongo hicho, vyote vitatokana na Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vitatolewa kwa mujibu wa masharti ya ibara hii."

Sasa hili jambo kumbe ni la Kikatiba. Mimi uzoefu wangu Bungeni ni mdogo. Mimi nikuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni lini Bunge hili limepitisha mshahara wa Mheshimiwa Rais na wa kwako wewe Waziri Mkuu?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ndiyo tatizo la maswali mengine ambayo unashitukizwa hapa. Nilikuwa nimemwomba huyu bwana ukiwa na swali niarifu basi nifanaye *research* kidogo, akasema hata kidogo tutakupiga tu hivyo hivyo.

Lakini siwezi kulijibu vizuri sana, kwa sababu ni kweli suaona masuala haya ya mishahara kwa viongozi yanajadiliwa ndani ya Bunge, ingawa Katiba imeweka au

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

imetamka kwamba ndiyo itakayoongoza katika utoaji wa mishahara hii kwa viongozi, lakini vile vile hata kwa watumishi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ninachowea kusema tu ni kwamba ukishakuwa na kifungu kama hicho, kwa kawaida kunakuwa na sheria sasa ambayo inakuja inaweka utaratibu wa namna mishahara hiyo itakavyotengenezwa.

Lakini sheria hiyo peke yake kwa maoni yangu haitoshi, lazima kutakuwepo sasa na taratibu nyingine za kikanuni ambazo zinasimamiwa kwa kawaida na ofisi ambayo inashughulika na masuala ya Utumishi kwa ujumla wake, ambayo kwetu sisi hapa ni Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Kwa hiyo, mimi naamini kabisa katika mtiririko huo, mahali fulani lazima kutakuwa na utaratibu ambao ndio umeweka stahili za viongozi mbalimbali ikiwemo na mishahara pamoja na malipo ya mwisho wa kazi anapomaliza utumishi wake. Sasa ungekuwa umeniambia ningekutafutia na sheria nikai-*quote* na nini, lakini kwa kifupi ninaweza nikasema hivyo.

MHE. ENG. MOHAMMED H. J. MNYAA: Mheshimiwsa Spika, ahsante. Kwa kuwa mitandao ya kijamii ndiyo inayoonyesha mshahara wa Rais kuwa ni milioni 32, wa kwako weve milioni 26 na kwa kuwa ni jambo la kikatiba na Bunge ndiyo linalopaswa kupanga pamoja na sheria yoyote itakayoundwa.

Je, utakubaliana na mimi Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba jambo hili Bunge lako limeporwa na kupelekwa kwa *Executive*?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, afadhali ujibu uongo wa Magazeti. (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kuna wakati nilisikia, lakini halikunipa tabu sana. Niliposikia rafiki yangu Kabwe yuko huko Mpanda ananiambia Waziri Mkuu wanapata milioni 30, ndipo niliposhituka zaidi. Kwa sababu Waziri Mkuu mshahara wake anazopata fedha taslimu (mimi) ni shilingi milioni sita (6,000,000)?=. Hiyo ni pamoja na posho ya mke wangu ambayo nayo ni sehemu ya fedha hiyo. (*Kicheko/Makofi*)

Sasa mtu anapokuja na kusema ninapata milioni 30, unaona tu kwamba pengine labda ni njama au ni mtu anataka kuharibu jina la mtu. Maana alisema huyu bwana anajiita mtoto wa Mkulima, mtoto wa mkulima gani anapata mshahara mkubwa kiasi hicho. Nikasema maskini baba wa watu huyu, nadhani Mwenyezi Mungu atamwepusha na balaa ambazo zinaweza kumpata kwa kusema uongo. Unaona. (*Makofi/Kicheko*)

Nimeona niliseme kwa maana ya mimi na sitamsemea Makamu wa Rais, wala sitamsemea Rais mwenyewe. Lakini nataka nikuthibitishie Mheshimiwa, tofauti kati ya mshahara wangu mimi na Makamu na Rais, hauzidi hata milioni moja. *Statute salary*, ambayo unaweza uka-*imagine* uone bwana mkubwa anayemsema Mkuu wa Nchi anapata kiasi gani, Makamu wa Rais naye anapata kiasi gani.

Mimi nafikiri kubwa ambalo ninaweza nikalisema kwa maana ya mfumo wa nchi yetu ulivyo, ni kuwashukuru wale waliofikiria jambo hili kwamba mtakaa mwenye nyumba ya Serikali ambayo hamlipii gharama yoyote. Mnapat

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

chakula ambacho hamgharamii ninyi wenyewe. Mimi ninafikiri hili lilifanywa kwa maksudi ili kuwawezesha msitumie muda wenu mwingi kufikiria namna ya kupata fedha, kutafuta namna ya kuishi na familia yako. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kwa hili naweza nikasema lazima tuwashukuru sana Watanzania kwa kufikiria jambo zuri kama hili. Kwa kweli ukiondoa haya, mengine nitarudi tu kwa Mheshimiwa Spika na kusema na mimi ni sehemu ya Wabunge.

Kwa hiyo, kama kapo kaposho ka aina fulani tunaweka, na mimi mmeniwekea sijui laki tano zile sijui laki sita, kwa maana ya *responsibility allowance* kwa ajili ya Waziri Mkuu. Ukiondoa hiyo, sana sana itakuwa ni fedha ambazo wewe unapata na mimi napata kulingana na ukubwa wa jimbo, tunapata wote posho ya jimbo. Sasa sijui.

Lakini ninachoweza kusema tu ni kwamba nadhani kama kuna nchi ambayo imetengenewa utaratibu ambao unawapa viongozi namna ya kuwatumikia Watanzania bila kujali sana mambo yenu binafsi, ni pamoja na Tanzania. (*Makofi*)

Lakini nimalizie kwamba Waziri Mkuu huyu, silisemi hili kwa sababu nataka kujigamba; lakini kwa sababu nimeulizwa. Kama kuna fundi wa kukopa Benki, mimi ni fundi sana. Nimekopa *NMB*, nilipoona nimezidiwa nguvu nikahamia *CRDB*.

Juzi juzi hapa mliporuhusu kukopa kiinua mgongo kile 50%, mimi nimechukua 50% ya kwangu. Lakini yote hiyo ni kwa sababu ndio utaratibu mlioweka mzuri ambao unatuwezesha tuweze kuishi katika mfumo ambao mimi naamini ni mzuri, na pengine hautuingizi katika tamaa zisizo za maana. Kwa kifupi ninaweza nikasema hivyo tu. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED]

SPIKA: Sisi hatutaki kusema zaidi ya hapo, maana yake! Haya tunaendelea na Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, swali linalofuata. (*Makofi/Kicheko*).

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, pole sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anazingua utoaji wa vitambulisho vya taifa mwezi Februari, mwaka huu 2013, alieleza kuwa vitambulisho vya *bio-metric* ndivyo ambavyo vitatumika katika zoezi la kupigia kura.

Kwa vile sasa hivi *NEC* wamezuia zoezi lao hadi pale *NIDA* watakapokamilisha shughuli zao, kitu ambachoh kinaonekana kwenda katika mwendo wa kusuasua na kukatisha tamaa na hasa ukizingatia kwamba tayari Bunge sasa hivi linapitisha Muswada wa Kura ya Maoni ambayo yatafanyika kabla ya Uchaguzi Mkuu, 2015.

Nataka kujua Mheshimiwa Waziri Mkuu, kutokana na muda ambao uliopo na kauli ya Rais kwamba 2014 Katiba Mpya iwe imeshapatikana. Hivi ni kweli Serikali yako imejipangaje kuweza kufikia muda huo na ile kauli ya Rais ikaonekana kwamba ina ukweli?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ni kweli anachokisema Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed ni hisia, siyo ya kwako peke yako tu. Wako Watanzania vile vile ambao iko hofu au wasiwasi huo kwamba je, chombo hiki kitaweza kweli kutekeleza jukumu hili kwa wakati uliotakiwa ili tutakapofika kwenye Uchaguzi Mkuu tuwe tuna vitambulisho ambavyo vitatupeleka huko.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)
[WAZIRI MKUU]

Ninachoweza kusema tu ni kwamba bado mimi nina matumaini makubwa tu kwamba tutaweza. Kwa sababu kikwazo kikubwa kimekuwa ni cha kibajeti, lakini tunaendelea kukishughulikia kadiri muda unavyokwenda. Tulichelewa kidogo kutokana na mchakato wa sheria ile ya manunuzi wa namna ya kumpata mnunuzi au *supplier* atakayeweza kutupatia vifaa stahiki kwa ajili ya zoezi hili.

Lakini baadaye likapatiwa ufumbuzi, akawa amepatikana na shughuli ikawa imeanza. Ndiyo maana uliona tumeanza na utoaji wa hati hizo kwa vipande vipande hapa nchini.

Kwa hiyo, bado tunafikiri tutasukuma jambo hili kwa nguvu sana tufike mpaka mwisho *on time* ili Watanzania waweze kunufaika. *It is a challenge to the government,* lakini tunajitahidi sana.

SPIKA: Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, swali la nyongeza.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, nimeingia roho ya huruma kidogo kwa Waziri Mkuu, naona nisiongeze swali.

SPIKA: Umeishiwa bwana. Umeishiwa, ukasema huruma. Yeye hahitaji huruma. (*Kicheko*)

Haya, ahsante sana. Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, swali lingine.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. DAVID ZACHARIA KAFULILA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwezi wa 11, taarifa iliyotolewa na Kampuni ya *Price Water Coopers* ambayo ni ya utafiti uliofanywa pamoja na wao na Benki ya Dunia, umeonyesha kwamba katika kodi, Tanzania inaongoza katika Afrika ya Mashariki kwa kuwatoza wafanyakazi wake kuliko nchi yoyote; kuliko Burundi, kuliko Rwanda, kuliko Kenya na kuliko Uganda.

SPIKA: Kuwatoza kodi kubwa au kodi tu?

toza kodi kubwa. Na ningependa kumpa takwimu tu kwamba kwa mujibu wa taarifa ile inaonyesha kwamba *average tax* ambayo inatozwa wafanyakazi wa Tanzania, *average* ni asilimia 18%. Na wakati nchi pili ambayo ni Burundi ni asilimia 10.3%, na nchi ya tatu ambayo ni Uganda ni asilimia 10.2%, na nchi ya Kenya ni asilimia 6.8% na nchi ya Rwanda ambayo ni ya mwisho ni asilimia 5.6% *average*. Kwa hiyo, sisi Tanzania ndio tunaongoza kwa kuwatoza wafanyakazi wetu kodi kuliko nchi yoyote ya Afrika ya Mashariki.

Naomba msimamo wa Serikali ambayo hii ni Serikali inayoongozwa na Chama ambacho kinasema ni cha Wakulima na Wafanyakazi. Naomba kujua msimamo wa Serikali kwamba ni kwa nini inatoza kodi kubwa wafanyakazi kuliko nchi yoyote, na wakati huo huo taarifa hiyo hiyo inaonyesha kwamba Tanzania ndiyo nchi ambayo katika Afrika ya Mashariki inatoza kodi kidogo kuliko nchi zote za Afrika Mashariki. Sasa hii Serikali kwa nini inatoza kodi kubwa wafanyakazi kwa takwimu hizo na kwa nini inatoza kodi ndogo wafanya biashara. Hiki ni Chama cha Wafanya Biashara au cha Wafanyakazi?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, analolisema Mheshimiwa Kafulila ndiyo uhalisia wake ulivyo. Kwa sasa hivi ndio mfumo ulivyo wa kodi Hapa nchini. Lakini upande

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

wa Serikali, Waziri wa Fedha yuko hapa pamoja na wenzake, tumeanza kuangalia uwezekano wa kuona namna gani tunawenza kuangalia eneo hili kwa upande wa watumishi, ili tuweze kufika mahali ambapo tunafikiri hatutafanana sana na nchi nyingine kwa sababu hoja si utumishi, lakini mazingira vile vile ya nchi lazima uyazingatie na uweze kuona uweke nguvu kubwa wapi na upunguze kiasi gani na kwa upande gani. (*Makofii*)

Kwa hiyo, katika zoezi hilo tutaangalia maeneo yote pamoja na kodi zetu kwa upande wa wafanya biashara. Unaweza ukakutana na wafanya biashara kwa ujumla, na wenyewe wanawnung'unika kwamba kodi ni nyingi sana, tunakuwa watu ambao hatuwezi kushindana kabisa na nchi nyingine.

Kwa hiyo, itabidi zoezi zima hili liangaliwe kwa ujumla wake; Wafanya biashara, watumishi. Halafu tutawianisha tuone sehemu gani tuweze kuongeza kidogo, sehemu gani tupunguze zaidi ili mradi tu tuweze kuona kama tutakuwa na ahueni kwa sehemu kubwa.

Lakini tunaangalia vile vile hata sheria ya VAT na wenyewe tunaiangalia upya ili na wenyewe tuweze kuona kama tunawenza. Maana utakapochukua hatua upande mmoja, lazima utafute upande mwengine ku-easy up ili uweze kuwa na wigo mpana zaidi wa watu ambao wako tayari kulipa hiyo kodi. Kwa hiyo unalouliza ni la msingi kabisa, na sisi bahati nzuri tumeanza kulifanyia kazi tuone kama tutafika mahali tuweze kupata suluhu ya jambo hili.

SPIKA: Mheshimiwa Kafulila, swali lingine la nyongeza.

MHE. DAVID ZACHARIA KAFULILA: Mheshimiwa Spika, hii Serikali imekuwa ni Serikali ya kuahirisha mambo mengi kwa muda mrefu. Na majibu ya Waziri Mkuu, siku zote ni majibu ya kuahirisha.

Naomba niulize kitu kimoja. Serikali hii kwenye Bajeti ya mwaka 2009 kwa mfano, iliahidi kwenye Bunge kwamba

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DAVID ZACHARIA KAFULILA]

itapunguza kodi kwa zana za kilimo. Lakini tangu Bajeti ya 2009/2010 na mpaka leo ukizungumza na watu ambao wanaagiza vifaa nya kilimo, wanasesma hali bado iko vile vile.

Lakini Serikali hii mwaka 2012 walihidi watapunguza misamaha ya kodi kwa wafanya biashara kwa kuzingatia kwamba Tanzania ndiyo inaongoza kwa kutoa misama mikubwa ya kodi kuliko nchi yoyote Afrika Mashariki.

Tunatoa *exemption*, misamaha ya kodi asilimia 4.5% ya *GDP* (pato La taifa); wakati nchi zingine wanatosha kati ya asilimia 1% mpaka 2%. Sasa majibu haya ya leo kwamba tutaaangalia, majibu yaliyopita mengine mlituambia tutaaangalia.

Naomba kujua, kama Waziri Mkuu, ni lini unawaahidi wafanyakazi wa Tanzania kwamba Serikali yako itakuwa tayari kupunguza mzigo huu mkubwa wa kodi ili kusudi wawe na uhakika wa majibu yako?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Kafulila, kwa nini unauliza na huku umekasirika, unaona kama unapambana. Kwa nini usiulize vizuri tu kwa utaratibu tu, inakuwa kama unagombana na Waziri Mkuu bwana.

SPIKA: Ana matatizo. (*Kicheko*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, Ndugu yangu Kafulila ungekuwa umesoma vizuri yote mawili uliyosema, ungekuta kwamba ulichokisema kingetakiwa kuwa *qualified* vile vile.

Kwa sababu ni kweli kumekuwa na kilio kwa muda mrefu juu ya kupunguza bei kwenye sekta ya kilimo. Sasa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

ukiniambia limeahirishwa, si kweli. Tulikaa na tukapunguza maeneo mengi tu.

Eneo ambalo tulibaki tunahangaika nalo ni lile ambalo linahusu hasa vipuri. Kwa sababu vipuri kulingana na taratibu za *TRA*, ndiyo eneo ambalo kodi yake lazima tuiangalie tena, watuambie tunaifanya namna gani. Lakini tulishachukua hatua tayari kwenye eneo hilo.

Lakini ni kweli kwamba kwa upana wake inawezekana bado kuna maeneo kadhaa ambayo lazima vile vile tuendelee kuona namna gani ili tuweze kuvuta zaidi watu katika sekta ya kilimo. Lakini hatua kwa maana ya zile ambazo zilikuwa zimelalamikiwa tulishafanya.

Haya umezungumza hata hata hili jingine la pili kwenye exemptions nyingine ni juzi tu hapa tulikuja tukapitisha sheria hapa tumefuta baadhi ya misamaha ambayo ilikuwa inatolewa na hasa kwenye mafuta.

Kwa hiyo, sasa hivi mwekezaji anayekuja kuwekeza hapa mlitushauri na siye tukafikiri ni jambo zuri tukaondoa zile exemptions zote zinazohusiana na matufa, sasa hivi hakuna labda itokee kwamba ni kitu ambacho kitakuja kuangaliwa tena baadaye, kwa hiyo zipo jitahada za Serikali katika maeneo karibu yote ambayo yanasemwaa au yanalamikiwa ili tuweze kuona ni namna gani tunaweza tukafikisha jambo hili pazuri tukawa na watu wengi zaidi ambaa wana *complay* badala ya kuwa na watu wachache ambaa wanatozwa fedha nyingi zaidi, kwa hiyo tutaendelea tukishauriana pale tutakapoonekana ni muhimu tutafanya.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Nchi yetu imegubikwa na kutawaliwa na vitendo vya ujisadi, katika maeneo tofauti na ujisadi kwa maana ya dhana pana si

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOSES J. MACHALI]

vitendo nya wizi wa fedha peke yake ni pamoja na kuwafanya wananchi vitendo nya kikatili, vitendo nya kinyama kama ambavyo leo hii vinafanyika kule katika Jimbo langu la Kasuru Mjini na ambavyo una taarifa navyo.

Wananchi leo hii wanafyekewa mazao katika eneo ambalo Serikali imekuwa ina-claim kwamba ni eneo la hifadhi. Lakini eneo hilo ambalo tumekuwa tukikueleza kwa zaidi tangu mwaka juzi ni eneo ambalo wananchi wanalima kwa zidi ya miaka thelathini hadi sasa.

Leo wananchi wanakwenda kufyekewa mazao na Serikali hii hii ambayo mnasema kwamba nyie mnawajali wakulima na kauli mbiu yenu imekuwa ni kilimo kwanza. Nini kauli ya Serikali kuhusiana na suala zima la kuzuia zoezi la kuwanyanyapaa wakulima wa Wilaya ya Kasulu na Mkoa wa Kigoma la kuwafyekea mazao katika eneo la Kagerankanda.

Serikali inazungumza nini. Imewachomea nyumba hata katika baadhi ya maeneo, tumeripoti lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu uliahidi kulitatua tatizo hili lakini hakuna ambacho umeweza kufanya mpaka dakika hii. Naomba kauli ya Serikali inawasaidiaje wakulima hawa.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwanza nataka niwaombe Watanzania kwa dhati tu, si jambo jema kwa Watanzania kuamua kwenda kwenye maeneo ambayo ni hifadhi ama za misitu ama za wanyamapor. Maana mgogoro unaanzia pale, kama watu tutaheshimu sheria na taratibu za nchi hili haliwezi kuwepo, kwa hiyo kitu cha kwanza watu tusivamie au kuingia kwenye maeneo ambayo yametengwa mahsus kwa ajli ama ya misitu au wanyamapor.

Kuhusu hili la Kasulu, la Kasulu umekuwa unalieleza sana nilipokuja ziarani ulikuwa unalieleza vilevile, mimi nika-cross check na watu wa Mkoani nikaambiwa kusema kweli

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

lile ni eneo la hifadhi na hakuna mtu anayetakiwa kulima ndani ya hifadhi. Nikawaambia basi vizuri, kama ni eneo la hifadhi, fuateni taratibu za kuwaelimisha wananchi pale ili waweze kuondoka kwa utaratibu ambao ni mzuri. (*Makofii*)

Jana na juzi umeniambia, kwamba wananchi wale waliokuwa mle walikuwa wamelima sasa nasikia wamefyekewa vyakula na kadhalika na kadhalika. Nikarudia kusema hili hili kwamba tatizo linaanza kwa sababu Watanzania hatutaki kusikiliza hili kwamba inapokuwa ni hifadhi tusiruhusu watu kwenda mle ndani. Nikakuahidi kwamba nitazungumza na Mkuu wa Mkoa nione kama hiyo hatua ya kufyeka imefanyika au inaendelea mpaka leo, nimezungumza naye mimi, akaniambia Mheshimiwa Waziri Mkuu zoezi hilo kweli lilitanyika na baada ya kupata taarifa akaagiza zoezi hilo lisimame.

Jana amenithibitishia kwamba zoezi hilo lilitimama kwa sababu aliwaambia kwamba kwa nini mliacha mpaka wakalima halafu mnataka kuja kuchukua baada ya kuwa mazao yameanza kulimwa kwa hiyo akasema msingi ulikosewa tangu mwanzo lakini amekwisha lisimamisha *DC* hayupo lakini amesema ameagiza vyombo visimamie na kuhakikisha kwamba hilo haliendelei kufanyika tena. Hiyo ndiyo taarifa ambayo nimeipata jana. Kwa hiyo, kwa kifupi naweza nikasema hivyo tu. (*Makofii*)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa kwa mujibu wa ibara ya 8 ya katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaeleza bayana kuwa Serikali iliyoko madarakani itapata mamlaka yake kutoka kwa wananchi na kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Kasulu Mkoani Kigoma wanahitaji eneo lile kulitumia kwa kilimo na kwa nyakati tofauti, kaeni kimya, na kwa nyakati tofauti.

SPIKA: Mheshimiwa Machali, naomba ufute maneno yako hayo.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nayaondoa maneno yangu, lakini naomba uwaambie waache kuzomea, wanaguna kitu gani, ni utovu wa nidhamu huo.

SPIKA: Mheshimiwa Machali, kwanza ukae, kwanza ukae tuzungumze, ukae, ukae kwanza kwanza nimesema Kafulila sio Kafulila ni Machali nimemwomba afute maneno yake kuwaambia waenzake kaa kimya kwa hiyo naomba uondoe haya maneno halafu uendeleee.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimwa Spika ni aheri nikae chini kuliko kuondoa maneno kwa sababu utovu wa nidhamu uko kwao, nisiulize swali langu.

SPIKA: Kwa nini mnapenda ushindani, tulishawaambia jamani Bungeni lazima muwe huru kuzungumza *sleep of a tongue* ni jambo la kawaida. Lakini usifanye hasira ndivyo Bunge livilvyo. Kwa nini hamzoei. Mheshimiwa Machali mbona tunabishana! Machali mbona tunabishana! Sidhani kama ni lazima.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana tunakushukuru kwa kujibu maswali vizuri hata kama watu leo walikuwa wachache. Lakini naomba mjue kwamba hasira ni hasara. Sasa tuendeleee. Katibu, tuendeleee. (*Makofii*)

MASWALI YA KAWAIDA

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. EZEKIEL D. WENJE]

Na. 30

Akidi Katika Vikao vya Halmashauri

MHE. EZEKIEL D. WENJE (K.n.y. MHE. HIGHNESS SAMSON KIWIA) aliuliza:-

Sheria Na. 8 ya 1982 inazitaka Halmashauri zote nchini ziwe na Kanuni za Kudumu za kutekeleza majukumu yake Kanuni Na. 8 (1, 2, 3) inayohusu Halmashauri zote Nchini kuwa na Akidi halali katika kuendesha mikutano yao:-

(a) Je, kwa mujibu wa Maeleo haya ni halali Halmashauri yenye wajumbe 14 kufanya Mkutano wa Uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti huku wajumbe wa kikao hicho wakiwa 6 tu?

(b) Je, Uchaguzi unaofanywa na Halmashauri bila kuzingatia akidi utakuwa halali?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Highness Samson Kiwia, Mbunge wa Illemela, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli uchaguzi wowote unaofanywa na Halmashauri yoyote pasipo kuzingatia akidi kama ilivyofafanuliwa katika kifungu cha 36 cha Sheria za Serikali za Mitaa ya 1982 (Mamlaka za Miji) Sura 288 na Kanuni za Kudumu katika Kanuni ya 8 (1) (2) na (3) sio halali.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Illemela ina jumla ya Madiwani 14 wekiwemo Wabunge. Tarehe 9 Novemba, 2012 ulifanyika mkutano wa Baraza la Madiwani kwa ajili ya uchaguzi wa Mstahiki Meya na Naibu Meya.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO A NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):

Aidha, ni kweli kwamba kati ya wabunge 14 wa Baraza la Madiwani, ni wajumbe 11 ndio waliofanya uchaguzi wa viongozi hao wawili kwa sababu wajumbe wengine watatu (3) walikuwa kifunguno kwa muda wa miezi 3 kwa kosa la kudharau amri halali ya Mahakama, (*Contempt of Court*) kuititia shauri la madai Namba 58 la mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, kati ya wajumbe 11 waliotakiwa kufanya uchaguzi, wajumbe watano (5) hawakuhudhuria mukutano huo pamoja na kupatiwa taarifa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya llemela.

Hivyo, wajumbe sita (6) waliofanya uchaguzi huo walikidhi akidi inayotakiwa kwa sababu walikuwa zaidi ya nusu ya wajumbe wote 11 kama ilivyoelezwa hapo juu. Hivyo kikao hicho kilikuwa halali. (*Makofii*)

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria za uchaguzi kwenye Halmashauri ya namna ya kupata Naibu Meya au Meya, akidi inayotakiwa katika hivi vikao vyta uchaguzi siyo *simple majority* ni *two thirds* ya *majority* na ukichukua hata ukichukua idadi ya watu 14 wote ambao ni wajumbe wote kwenye hiyo Halmashauri *two third* inatakiwa iwe 9 ukichukua sasa hiyo 11 anayosema Mheshimiwa Waziri kwamba ndio walioalikwa *two third* ya 11 kwa mahesabu ya haraka haraka ni 7.3 kwa hiyo tunarround up inakuwa 7 (saba).

Sasa katika hicho kikao anavyosema kwamba wajumbe sasa waliohudhuria na kufanya uchaguzi walikuwa ni wajumbe sita (6) ambayo bado iko chini ya *requirement* ya akidi ambayo ni *two thirds* sasa swalii langu:-

(a) Kwa nini Waziri amelidanganya Bunge kwamba akidi ilitosha kwenye hichi kikao?

(b) Kwa nini Serikali isitoe tamko hapa leo la kufuta huu uchaguzi kwamba haukuwa halali?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)]

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Wenje, kama ifuatavyo:-

Kama niliviotangulia kusema, madiwani watatu (3) walikuwa wamefungwa gerezani kwa kifungo cha miezi mitatu (3) madiwani waliokuwa wapo ni 11 na katika chaguzi zetu zote tunazochaugua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti katika Halmashauri zote tunatumia *simple majority* hatujawahi kuwa na *two third*.

Mheshimiwa Spika napenda nirudie tena sijalidanganya Bunge arudi akasome hiyo sheria tena ambayo ye ye ameisoma ni zaidi ya nusu. (*Makofi*)

MHE. CECILIA D. PARESO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swalii dogo la nyongeza. Kwa kuwa kuna marekebisho makubwa yamefanyika katika Kanuni za kudumu za Halmashauri mbalimbali nchini na ni Halmashauri chache tu imefanikiwa kuzipata hiso kanuni na kuanza kuzitumia ili hali Halmashauri nyingi bado haijapata hiso Kanuni.

Je, ni lini sasa Kanuni hiso mpya zitafika Halmashauri zote nchini na utekelezaji uanze. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Pareso, Kama ifuatavyo:-

Kanuni zile za kudumu tulizituma katika Mikoa yote kwa soft copy kupitia Mikoa, kwa hiyo kama kuna Halmashauri yoyote ambayo haijapata Kanuni zile iwasiliane na Mikoa wao husika eidha kwa RAS au AAS wao lakini

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. HALIMA JAMES MDEE]

kote tumetuma kwa wakati mmoja na hata Waheshimiwa mnawenza mkazitafuta hizo mitandao kwenye Kanuni.

Na. 31

Ujenzi wa Kiwanda cha Nyama Dar es salaam

MHE. HALIMA JAMES MDEE aliuliza:-

Miaka kadhaa iliyopita Kampuni ya *R&M* kutoka Malaysia imechangia Makataba na Halmashauri za llala, Kinondoni na Temeke wa ujenzi wa Kiwanda cha Nyama lakini mradi huo haujaanza mpaka sasa:-

(a) Ni kiasi gani cha fedha na mali ambacho kila Halmashauri ilichangia na ni nani alikuwa mkusanyaji wa michango hiyo na alikuwa anaweka wapi?

(b) Kampuni ya *R&M* ya Malaysia na *EAMETCO* zilipatikanaje na zilikuwa na nafasi gani katika mradi/ mkataba huo?

(c) Je, Halmashauri za Mkoa wa Dar es salaam zilinufaikaje na mradi huo na ni nini hatma ya fedha/mali ambazo Halmashauri hizo zilichangia katika mradi huo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Kawe, lenye vipengele (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha kilichotolewa kwa kila Halmashauri za Mkoa wa Dar es salaam kwa ajili ya ubia wa kuanzisha kiwanda cha kusindika nyama ni kama ifuatavyo. Halmashauri ya Jiji ilichangia kiasi cha shilingi 663,876,001/= pamoja na kiwanja

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI MEN. YA UTUMISHI WA UMMA]

chenye thamani ya shilingi 599,700,000/= Halmashauri ya Manispaa ya llala Shilingi 554,567,334/= Halmashauri ya Manispaa ya Temeke shilingi 242,606,927/= na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni 180,033,333/=. Hivyo jumla ya fedha zilizochangwa kuwa shilingi 1,641,084,595/=. Karibu fedha zote zilizochangwa zilitumika katika hatua za awali za uanzishwaji wa kiwanda hicho.

Hata hivyo, fedha zilizotolewa katika Halmashauri za Manispaa ya llala, Temeke na Kinondoni zilipelekwa katika akaunti Namba 0104020761800 ya Kampuni ya *East Africa Meat Company (EAMEATCO)* iliyofunguliwa Benki ya Standard Chartered na kubakia na salio la shilingi 51,814/= tu.

(b) Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *EAMETCO* ni Kampuni Binafsi ya uwekezaji wa ndani na *R&M* ni Kampuni kutoka nchini Malaysia ambayo illingia ubia na Kampuni ya *EAMEATCO* kwa ajili ya kuwekeza katika Kiwanda cha kusindika nyama. Kampuni hizi zilipatikana kupitia andiko la mradi lilioandaliwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali ili kupata uwekezaji katika kiwanda hicho Jijini Dar es salaam.

(c) Mheshimiwa Spika, Ubia baina ya Halmashauri za Mkoa wa Dar es salaam, Kampuni Binafsi ya *EAMEATCO* na Kampuni ya *R&M* ya Malaysia haukuzaa matunda yaliyotarajiwa kutokana na uwepo wa kasoro nydingi katika muundo na uendeshaji wa Kampuni iliyotarajiwa kuanzishwa.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru shilingi bilioni 100.6 ambazo ni sawasawa na bilioni 1600 zilizotokana na wananchi wa kawaida sana wa Dar es salaam ni pesa nydingi sana sasa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba fedha hizi zilitumika kwenye hatua za awali zote za uendelezaji wa mradi lakini mimi nafahamu kwamba ripoti za *CAG* ziliainisha kwamba kulikuwa na ubadhilifu kwenye matumizi ya fedha za huu mradi na naamini kwamba Mheshimiwa Waziri anajua kwamba ripoti za *CAG* zilihoji matumizi ya fedha na utaratibu mzima wa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN J. MNYIKA]:

huu mradi. Ni kwa nini Mheshimiwa Waziri amelidanganya Bunge kwa kusema kwamba zilitumika katika hatua za awali za uendelezaji wa mradi ilihali akijua kulikuwa na matumizi mabaya kwenye fedha hizo?

Pili, Wizara hii ya TAMISEMI imelifahamu jambo hili na kwa mujibu wa Mheshimiwa Waziri mwenyewe kwamba TAMISEMI iliongoza Kikao, Ofisi ya Waziri Mkuu mwaka 2009 wakakubaliana kwamba mradi huu usitishwe na fedha zirejeshwe jambo hili tumelikumbusha 2010, 2011, 2012, 2013 na leo Mheshimiwa Waziri anajibu kwamba Ofisi yangu inalifahamu swala hili analifahamu na analifanya kazi kwa kuzingatia sheria zilizopo.

Mheshimiwa Spika, majibu haya yanaashiria uzembe kwa upande wa Serikali. Ni kwa nini basi Mheshimiwa Waziri ama achukue hatua za haraka au Idara yake iwjiblike kwamba inaendeleza mizigo ya kulinda ufisadi wa miaka mingi namna hii? Ningeomba majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa John Mnyika kama ifuatavyo. Ni kweli kwamba pesa zilitumika katika maandalizi ya awali, zilitumika vizuri, zilitumika vibaya lakini pesa zilitumika.

Sasa nnachotaka kusema uzembe sio wa TAMISEMI peke yake kwa sababu hao waliochanga ni katika Halmashauri za Manispaa za Dar es salaam ambazo Mnyika naye mwenyewe ni Mbunge. Kwa hiyo, kama ni matumizi wameyafanya wao na hatua za kuchukua wao wanapaswa pia kusimamia kuchukua.

Kwa hiyo, kusiwe ni suala kwamba matumizi mabaya yanafanya kwenye, Halmashauri tunashindwa kuwachukulia hatua watu ambao tuna mamlaka nao halafu kila kitu tunasukumia TAMISEMI. Mnao uwezo wa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kuwachukulia hatua, lakini na sisi tunasema tutalifuatilia.
(Makofi)

Na. 32

Mikakati ya Kuondoa Rushwa NchiniMHE.

MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU aliuliza:-

Rushwa ni adui wa haki na kufanya ukuaji wa uchumi kwenye nchi yeote kuwa mdogo sana, katika nchi yetu rushwa imekomaa takribani kwenye taasisi zote na nchi kwa ujumla.

Je, Serikali ina mikakati gani kuondoa janga la rushwa nchini?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kujibu swalii la Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba kukubaliana na Mheshimimwa Mbunge kwamba Serikali inatambua kuwepo kwa tatizo la rushwa nchini na athari zake katika uchumi na maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Kutohana na hali hii, Serikali inayo mikakati mbalimbali ya kuzuia na kupambana na rushwa nchini.

Mikakati hiyo ni pamoja na kuongeza uelewa wa wananchi juu ya vitendo vya rushwa na umuhimu wa kushiriki kwao katika kuzuia na kupambana na rushwa, kuongeza wigo wa Wadau wa mapambano dhidi ya rushwa kwa kushirikisha Wizara, Idara na Wakala za Serikali, Serikali za mitaa, Asasi za Kiraia, Mashirika ya dini, Vyama vya Siasa, Vyombo vya habari, Sekta binafsi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mikakati mingine ni kuweka mfumo mzuri wa ufuatiliaji wa miradi ya Maendeleo ili

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA]

kuhakikisha kunakuwepo na thamani ya fedha yaani (*Value for Money*) na kuwaelimisha wananchi kutambua wajibu wao katika kusimamia miradi inayotekelozwa kwenye maeneo yao, kuimarisha maadili, uwajibikaji na kubadili tabia za wanasiasa, watendaji na wataalam hasa wa Jeshi la Polisi, Mahakama, Maliasili na Utalii, Mafuta na gesi.

Mheshimiwa Spika, mikakati mingine ni kuweka mfumo nzuri wa ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha kunakuwepo na thamani halisi ya fedha na kuwaelimisha wananchi kuambua wajibu wao katika kusimamia miradi inayotekelozwa kwenye maeneo yao. Kuimarisha maadili, uwajibikaji na kubadili tabia za wanasiasa, watendaji na wataalam hasa wa Jeshi la Polisi, Mahakama, aliasili na Utalii, Mafuta na Gesi.

Aidha, Mheshimiwa Spika, zinafanyika tafiti na udhibiti wa kupitia mifumo na taratibu mbalimbali zinazoongoza utendaji wa Taasisi za Serikali, Mashirika ya Umma na Taasisi binafsi ili kupima uzingatiaji na utekelezaji wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali kwa lengo la kubaini mianya ya rushwa na kuzishauri taasisi hizo namna bora ya kuzuia na kusimamia utekelezaji wa mifumo na taratibu zilizorekebishwa, baada ya kubainika kwa mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa rushwa imeenea takriban kwenye Taasisi zote kwa ujumla, napenda kuchukua fursa hii kutoa rai kwa viongozi wa ngazi zote tukiwemo Waheshimiwa Wabunge kuwa sehemu ya juhudzi za mapambano dhidi ya rushwa katika nchi yetu.

SPIKA: Mheshimiwa Amina Amour, swali la nyongeza.

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(1) Baada ya Serikali kuweka mikakati yote hii, je, imejitathmini na kuona hali ikoje?

(2) Hivi karibuni Chama cha Wabunge cha kupambana na rushwa (*GOPAC*) walipitishwa walipitisha azimio la kuzitaka nchi mbalimbali ambazo watabainika wachukuaji rushwa wakubwa na kupilisha sheria kwa wahumiwa kama *crime against humanity*.

Je, Serikali inaonaje isilet sheria kutoa hukumu hiyo?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Baada ya tathmini kufanyika, kwanza tumetambua mianya ya rushwa ni ipi; tumetambua hiyo. Baada ya kufanya hivyo, tumefanya utaratibu wa kuongeza wigo wa wadau wa kupambana na rushwa na tumeanzisha taasisi mbalimbali za kuzuia rushwa katika sehemu mbalimbali.

Kwa mfano, katika Wizara kuna kamati za kuzuia rushwa, katika Idara za Serikali za Mitaa na katika Taasisi zote za Serikali. Tumeenda mbali zaidi kuanzisha klabu za kuzuia rushwa katika Shule za Sekondari na Shule za Msingi pamoja na Vyuo Vikuu. Kwa hiyo, hizi ni jitihada ambazo tumezifanya baada ya kuona kwamba mianya ya rushwa imekuwa ni mingi na tumeibaini.

Hali ikoje! Kutokana na uwazi (*transparency*) katika Taasisi mbalimbali kwa sasa, hali ya rushwa inapungua kwa sababu uelewa wa wananchi ni mkubwa sana. Kwamba

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

mwananchi sasa anatambua kwamba hii ni haki yake ya msingi, kwa hiyo hawezি kutoa rushwa.

Kwa mfano, katika huduma za jamii, katika Hospitali, katika Shule za Msingi, Sekondari na kadhalika; na katika huduma mbalimbali za jamii. Kwa hiyo, ule utambuzi wa wananchi (*awareness*) kwa wananchi kuhusu suala la rushwa angalau limejaribu kupunguza ile takwimu ya rushwa kuwa kubwa.

Hilo la pili ambalo amelisema Mheshimiwa Mbunge ni zuri, naomba tulichukue ili tuweze kulifanyia kazi. Mimi baada ya kutoka hapa nitaonana na Waheshimiwa Wabunge ambao Mwenyekiti wake ambaye anasimamia hiyo taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa ili tuweze kuongea, tuone kwamba tutaliingizaje katika mfumo wa Serikali.

SPIKA: Mheshimiwa Vincent Nyerere.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Ahsante Mheshimiwa Spika, nilipenda kujua Serikali lini itakuwa *serious* katika kutenda. Maana tumekuwa tukipata majibu tu badala ya vitendo.

Kwa mfano, Serikali ya Mkoa wa Mara inatuhumiwa kwa kudai rushwa kwa wakandarasi wanaojenga Hospitali ya Mkoa wa Mara, lakini wale wale bado wako kazini. Lini Serikali itawachukulia hatua?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Nyerere, kama ifuatavyo:-

Serikali iko *serious* ndiyo maana ina mikakati, imeanzisha vyombo mbalimbali pamoja na ufuatiliaji wa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, YA UTUMISHI WA UMMA]

mambo mbalimbali. Na wenyewe mnaona, kesi mbalimbali ziko Mahakmani, na wanaochukuliwa hatua labda kwa kuwa hatutangazi hadharani. Lakini wanaochukuliwa hatua ni wengi sana.

Kuhusu suala *specific* la Mkoa wa Mara, rushwa lazima ithibitike. Chombo pekee kinachothibitisha kwamba huyu amepokea au ametoa rushwa ni Mahakama. Ni vyema tukiona kwamba hatua za kinidhamu hazichukuliwi, tunaenda kwenye mkondo wa kuchukua hatua za kisheria, yaani kuwapeleka Mahakmani.

Lakini kwa wafanyakazi tunachukua hatua mbili. Tunaweza tukachukua hatua za kinidhamu, na upande mwininge tunaweza tukachukua hatua za kuwapeleka Mahakmani.

Kwa hiyo, Hatua zote mbili hizi tunachukua, na tuko *serious* katika jambo hili. Ndiyo maana unaona watu wanapelekwa Mahakmani, wanasimamishwa au wanawekwa pembeni bado wakiwa kazini ili kupisha uchunguzi mbalimbali.

SPIKA: Mheshimiwa Hamad Rashid.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED: Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi tumemsikia Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU akilalamika kwamba kazi kubwa wanayoifanya ya kufanya uchunguzi na kukamata wahalifu, lakini kutokana na ukiritimba ulioko kwa DPP, kesi nyingi haziendi Mahakmani. Kuna ukweli gani na kauli hii?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad kama ifuatavyo:-

Kwa bahati nzuri, Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa Waziri wa Katiba na Sheria, na pale tuliunda Kamati Maalum ya Ofisi ya AG – yaani upande wa *DPP*, upande wa Polisi na upande wa TAKUKURU; ili kuweza kufuatilia mienendo ya kesi mbalimbali. Kutohana na Kamati hii mara nyingi wanafautana pengine kwenye Magereza na sehemu mbalimbali katika kutatua matatizo ya rushwa au pia kuangalia kule magerezani kwa nini kuna mlundikano wa kesi nyingi.

Kwa hiyo, kuna *cordination* kati ya TAKUKURU pamoja na Ofisi ya *DPP* pamoja na Mahakama. Hiyo kamati inafanya kazi vizuri, na kwa sasa utaona kwamba *at least* kuna uelewano kati ya Ofisi ya *DPP* na Ofisi ya TAKUKURU.

SPIKA: Naomba tuendelee na Wizara ya Fedha. Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa atauliza swali linalofuata.

Na. 33

Fedha za Miradi ya Maji

MHE. MARIA IBESHI HEWA aliuliza:-

Fedha nyingi za kutekeleza miradi ya maji nchini huombwa nje:-

Je, kwa nini tusitumie fedha za ndani?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)
ali;jibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)]

Mheshimiwa Spika, misaada na mikopo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji imekuwa sehemu muhimu ya Mfumo wa Bajeti (*Budget Frame*) ya Serikali kwa muda mrefu sasa. Hali hii haiwezi kuепukwa mara moja kutokana na sababu kuu mbili.

Kwanza, mapato yetu ya ndani Bado haitoshelezi kugharamia mahitaji yote muhimu ya Serikali pamoja na shughuli za maendeleo. Pili, washirika wetu wa maendeleo bado wana imani na Serikali yetu na hivyo wanaendelea kutoa misaada au mikopo nafuu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli huo naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba utekelezaji wa Bajeti ya Sekta ya Maji umekuwa ukipungua mwaka hadi mwaka. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 miradi ya maji ilitumia jumla ya shilingi bilioni 465.8.

Kati ya fedha hizo, fedha za ndani zilikuwa shilingi bilioni 140.0 sawa na asilimia 30.06% ya fedha zote za miradi ya maji na fedha za nje zilikuwa shilingi bilioni 325.7 sawa na asilimia 69.94%. Katika mwaka huu wa fedha 2013/2014, miradi ya maji imekisiwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 553.2. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 312 sawa na asilimia 56.4% ni fedha za ndani na shilingi bilioni 241.2 sawa na asilimia 43.6 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kupunguza utegemezi kutoka kwa washirika wetu wa maendeleo hatua kwa hatua. Hii itawezekana endapo kila Mtanzania atatimiza wajibu wake wa kufanya kazi kwa bidii na kulipa kodi kulingana na na sheria, kanuni na taratibu za kodi na nchi kwa ujumla na hivyo kukua mapato ya Serikali.

SPIKA: Mheshimiwa Maria Ibeshi, swali la nyongeza.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. MARIA IBESHI HEWA: Ahsante Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili mafupi ya nyongeza:-

Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, napenda kuuliza:-

(1) Wakati Serikali ilipoanzisha mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria, ule mradi mkubwa, maji yakaenda Shinyanga mpaka Kahama. Je, ulitumia fedha za ndani au ulitumia fedha za nje?

(2) Kama huo mradi uliweza kutumia fedha za ndani (*let's say*) na ukafanikiwa vizuri, walithubutu wakati huo. Je, Serikali kwa sasa hivi kwa nini isiendelee kuthubutu na kuanzisha miradi kutoka hata sehemu mbalimbali (*not necessarily*) kutoka Ziwa Victoria, ili kupunguza adha za akina mama wanaohangailka huko kutafuta maji, sehemu nyingi wanahatarisha maisha yao. Je, Serikali inanijibu nini, au uthubutu huo ulifutwa?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi kujibu swali hili la Mheshimiwa Maria Hewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kutekeleza mradi wa kutoka lhelele kuja Kahama na Shinyanga, iilitumia kwa kiasi kikubwa fedha zetu za ndani.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ameuliza Mheshimiwa Mbunge kama iko miradi mingine, na ningependa nimjibu Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo iko katika jibu la msingi ambalo limetolewa vizuri sana na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha. Kwamba mwaka huu wa fedha, Serikali inatumia fedha za ndani nyingi kuliko fedha za nje, katika kutekeleza miradi ya maji nchini kote.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE]

Mheshimiwa Spika, Serikali iko tayari na inaendelea kubuni miradi mikubwa na mingine midogo kwa ajili ya kutatua matatizo ya maji na lengo ni kuhakikisha kwamba ifikapo mwishoni mwa mwaka 2015 tunafikia uwiano wa watu wanaopata maji vijiji wa asilimia 74% na wale wanaoishi mijini kwa asilimia 90%.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Ahsante. Mheshimiwa Kandege, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Nakushukuru sana, Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli ulio dhahiri kwamba kumekuwa na mwitikio mkubwa sana kwa kutekeleza miradi inayofadhiliwa na *World Bank*.

Swali, napenda kujua kutoka Serikali, ni tatizo gani limesababisha pesa zisipelekwe katika miradi ambayo ilishaanzishwa, na hivyo kusababisha wakandarasi wasitekeleze miradi hiyo kwa wakati?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Umelielewa swali au arudie.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Kandege, kama ifuatavyo:-

Kuhusiana na miradi ya *World Bank*, suala la kuchelewa, siyo kucheleweshwa kwa sababu ya kucheleweshwa, isipokuwa ni taratibu zenyewe. Kila *tranch* inapotolewa na *World Bank* lazima tuwe tunapata *a no*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DAVID Z. KAFULILA (K.n.y. MHE. DKT. MREMA)]
objection kutoka kwao, na taratibu zile za kuhakiki matumizi kabla fedha nyingine hazijatolewa.

Kwa hiyo, nafikiri ni katika huo utaratibu, kunaonekana kama kuna urasimu wa ziada. Lakini kwa kifupi kwa pesa za *World Bank* ambazo tayari zimeidhinishwa huwa zinatolewa mara zinapokuwa zimehakikiwa.

SPIKA: Ahsante sana, tuna swali linalofuata, Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Kafulila siyo, ndiyo ukaenda kukaa hapo hapo. (*Makofi/Kicheko*)

Na. 34

Mikopo Inayotolewa na NMB – HIMO

MHE. DAVID Z. KAFULILA (K.n.y. MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA) aliliza:-

NMB – Himo imekuwa ikitoa mikopo yenyeye riba nafuu kwa vikundi vyta wajasiriamali vyta akina mama, vijana na wazee:-

(a) Tangu Benki hiyo ianzishe mradi huo ni watu wangapi wa Jimbo la Vunjo wamenufaika?

(b) *NMB*imekopesha kiasi gani cha fedha tangu ifungue Tawi la Himo?

(c) Kati ya wajasiamali waliokopeshwa mikopo, wako wanawake wangapi?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dk. Agostine Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a), b) na (c) kama ifuatavyo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DAVID Z. KAFULILA]

(a) Tawi la *NMB Himo* lilitifunguliwa Februari, 2013 ili kusogeza huduma za Kibenki karibu zaidi na wananchi. Mpaka kufikia tarehe 15 Oktoba, 2013 Tawi la *NMB Himo* limeweza kutoa mikopo kwa wajasi amali 151.

(b) Jumla ya kiasi cha fedha kilichokopeshwa kwa wajasi amali 151 ni shilingi 470,300,000/=.

(c) Mheshimiwa Spika, katika wajasi amali 151 waliolpata mikopo, wapo wajasi amali wanawake 83 ikiwa ni asilimia 54.97% ya wajasi amali wote waliopata mikopo.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Kafulila maswali ya nyongeza.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Tanzania ni nchi ambayo inaongoza kwa kuwa na benki nyingi katika nchi zote 14 za *SADDEC*. Lakini Tanzania ni nchi ambayo riba za kibenki kwa ajili ya wakopaji ziko juu kuliko nchi nyingi. Naomba msimamo wa Serikali, ni kwa nini Tanzania ina Benki 53, kiasi ambacho ni cha juu kuliko nchi zote kwenye nchi za *SADDEC*; lakini bado huduma za kibenki kwa maana ya riba, iko juu kuliko nchi nyingi katika nchi za *SADDEC*. (*Makof*)

Swali la pili, kutokana na matatizo haya ya huduma za kibenki, ilifika mahala wajanja wachache wakajitokeza wakaanzisha vitu walivyovita *DECI*. Kwa kuwa Serikali, kuititia Banki Kuu, ndiye msimamizi wa taasisi zote za fedha. Chombo kike kikaanzishwa, kikatapeli watu; mpaka leo maskini wengi Tanzania Vijijini na Mijini wanalia kuhusu pesa zao.

Kwa kuwa Serikali ndiyo ambayo inayosajili na kusimamia taasisi za fedha, ni lini Serikali itabeba dhamana ya kuwalipa watu wote waliodhulumiwa na *DECI* iliyoanzishwa kwa mamlaka ya Serikali? (*Makof*)

SPIKA: Hivi suala la *DECI* haliko Mahakamani, mimi sijui. Basi naomba ajibu swali la kwanza. Nasema ajibu swali la kwanza. Mheshimiwa jibu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)]

MHE. NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE): Ahsante Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba nijibu swali moja la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Kafulila kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa tuna benki nyingi Tanzania, kwa sasa hivi zimefikia 53; lakini riba bado iko juu. Sababu moja kubwa ni kuwa Benki zenyewe hazijasambaa kote kwa maana ya mitandao, kama ambavyo ingetegemewa. Lakini vile vile Benki hizi bado zinatumia gharama kubwa sana kujиndesha, kutokana vile vile na jinsi ambavyo zimejipanga. Mfumo wake mzima wa gharama zake ni mkubwa.

Serikali sasa hivi inaangalia uwezekano wa kuzishauri Benki nyingi ambazo zimeingia sokoni bila kutathmini vizuri mfumo mzima wa gharama na jinsi watakavyozihimili kwa kuwashauri kwanza. Siyo kuwa kila benki inayoanzishwa ijiwekee mfumo wake yenye wa kompyuta, wa *data base* na vitu mbalimbali. Lakini vile vile siyo lazima kila benki inayoanzishwa, na yenye we iwe na *ATM* zake na kila kitu.

Kwa hiyo, kuna ushauri ambaao umetolewa, na wengine wameshaanza kuufanya, wa kuwa na muungano wa *switches* au *systems* ambaao utawapunguzia zile gharama zao ili na wao sasa katika kujиndesha waweez kupunguza zile riba ambazo zinasumbua na kuleta usumbufu kwa wananchi.

SPIKA: Mheshimiwa Vita Kawawa.

MHE. VITA RASHID KAWAWA: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)]

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utaratibu uliokuwepo wa Vyama vya Msingi wa zao la tumbaku vimekuwa vikikopeshwa na mabenki ikiwemo benki ya *NMB* na kwa kuwa msimu huu maombi yao ya mikopo hiyo ya pembejeo yaliwasilishwa toka 13 Agosti, 2013 na hakuna majibu yanayoeleweka mpaka leo na msimu umewadia, *supplier* wa pembejeo ameshafikisha pembejeo mkoani Ruvuma na hawezi kusizisambaza pembejeo hizo kutokana na kukosekana kwa *authority* kutoka benki ya *NMB*.

Je, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Wizara ya Fedha kwa pamoja na kwa dharura mnaweza kusaidia kulishughulikia hili ili kuokoa uchumi wa Wananchi wa Wilaya ya Namtumbo na uchumi wa Taifa hili.

SPIKA: Mheshimiwa Vita Kawawa hakika kabisa swali hili ni geni, Waziri akikuruza atakavyokuruza usimwambie majibu hayatoshi. Na ye ye anajuaje habari za tumbaku, haya jibu kama unaweza, kama unayo habari, kama unayo habari jibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE): Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa fedha naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita Kawawa, kama ifuatavyo:-

Kusema kweli sina taarifa kamili juu ya suala hili, lakini naweza tu nikazungumzia hapa kijuu juu kuwa kuhusiana na maombi yaliyotumwa *NMB* kwa ajili Wakulima wa Tumbaku kulikuwa kuna suala la kutathmini malipo au mkopo wa nyuma kabla mwingine kuidhinishwa. Sasa hili ni suala ambalo mimi niko tayari kwenda kulifuatilia kwa umakini zaidi njue zile data haswa, lakini kijuu juu kulikuwa kuna suala kuwa benki inaangalia kuwa kuna mikopo mingine ambayo hajakamilishwa kulipwa sasa kuna mingine imeletwa kuombewa. Sasa mimi nakubali nitachukua hili tutaongea na Waziri wa Kilimo tuangalie jinsi gani tunawaaproach *NMB* watupe jibu sahihi halafu mimi binafsi nitamjibu Mheshimiwa Kawawa. (*Makofii*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA AFYA]

SPIKA: Ahsante sana, naomba tuendelee na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Na. 35

Hospitali za Mikoa Kupatiwa Madaktari Bingwa

MHE. MUNDE A. TAMBWE aliuliza:-

Hospitali nyingi za Mikoa ikiwemo ya Mkoa wa Tabora hazina Madaktari Bingwa wa kutosha.

Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kupeleka Madaktari Bingwa hasa akina mama ili kupunguza adha kubwa wanayopata wananchi?

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Munde Abdallah Tambwe, Viti Maalum Tabora, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Hospitali nyingi za Mikoa ikiwemo Hospitali ya Mkoa wa Tabora hazina Madaktari bingwa wa kutosha. Serikali inaendelea kufadhili madaktari katika fani za Ubingwa ili kupunguza tatizo hili.

Katika kipindi cha mwaka 2010/2011 - 2013/2014 Serikali imefadhili jumla ya madaktari 385 katika fani mbalimbali za ubingwa.

Mheshimiwa Spika, mikakati mingine ya harakati ya kupeleka madaktari Bingwa kwenye Hospitali nyingine za Rufaa za Mikoa ili kupunguza adha kubwa wanayopata wananchi ni pamoja na:-

(i) Kuwaajiri madaktari Bingwa ambao hawakuwa waajiriwa wa Serikali na kuwapangia kazi kwenye hospitali za Rufaa za Mikoa. Katika utaratibu huu waajiri husika wanatakiwa kuandaa Bajeti ya mishahara ya madaktari bingwa kulingana na mahitaji yao na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MUNDE A. TAMBWE]

kuiwasilisha Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa ajili ya kibali. Baada ya kupatiwa kibali, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii husaidia taratibu za kuwapata madaktari hao kutoka kwenye soko la ajira.

(ii) Kuwahamisha vituo vya kazi madaktari waajiriwa wa Serikali baada ya kuhitimu mafunzo ya udaktari bingwa. Madaktari hawa huhamishwa kutoka kwenye Hospitali za Wilaya ambazo kwa utaratibu hazina ikama ya madaktari bingwa au kuwahamisha madaktari bingwa kutoka maeneo ambayo yana idadi kubwa na kuwapeleka maeneo ambayo tatizo ni kubwa.

MHE. MUNDE A. TAMBWE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Waziri kwa mikakati yao mizuri ya kusomesha madaktari, lakini Mheshimiwa Spika mi sikumwuliza Mheshimiwa Waziri anasomesha madaktari wangapi, nimetaka kujua hospitali yangu ya Mkoa wa Tabora ambayo kwa sasa imepandishwa hadhi na kuwa Hospitali ya Rufaa kwa niaba ya Serikali kwamba wamepandisha hospitali zote za Mikoa kuwa hospitali za Rufaa. Ikama ya madaktari bingwa 6.

Mheshimiwa Spika mpaka leo hii toka mimi nimezaliwa hakuna daktari bingwa ndani ya Mkoa wa Tabora, nimemwuliza ana mkakati gani sasa wa haraka wa kupeleka madaktari bingwa wa wanawake na watoto, wa upasuaji, wa mifupa, ukilinganisha bodaboda zinazoweza kuvunja miguu vijana wetu, anijibu ana mkakati gani wa haraka wa kupeleka madaktari bingwa ndani ya Mkoa wa Tabora na wakati huo huo tuna shortage ya madaktari wa kawaida 21 aniambie ana mkakati gani na kwa muda gani atanipelekea madaktari bingwa katika Mkoa wa Tabora?

Kwa kuwa wodi zetu za Mkoa wa Tabora zina vitanda 40 na vitanda hivyo wanalala wagonjwa 2 kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA AFYA]

maana ya wagonjwa 80 na wagonjwa hao wanahudumiwa na nesi mmoja kwa usiku kucha na kusababisha wananchi wa Mkoa wa Tabora kukosa huduma stahiki kusababisha manesi hawa kulaumiwa pasipokuwa na lawama hizo kwa sababu mgonjwa mmoja kazidiwa wanaenda kumwita daktari, mwingine huku anataka kujifungua, mwingine huku anataka kukata roho, mwingine huku *drip* imekwisha na kukosa huduma stahiki kwa hiyo tuna-shortage ya manesi 270. Aniambie Mheshimiwa Waziri ananipelekea lini Manesi na Madaktari? Hilo ndilo swalilangu, Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI JAMII:

Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Munde kama ifuatavyo:-

(i) Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Munde kwa sababu alishakuja kwenye Wizara yangu na tulishazungumza kuhusu maswala haya ambayo sasa hivi anayaauliza, ki ukweli kwamba Serikali mwaka huu tumepeleka pale madaktari wanaozidi 8 lakini pia kuna madaktari bingwa kwenye Hospitali hiyo ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora ambao tumewapata kutoka katika mahusiano yetu na Serikali ya China.

Madaktari bingwa hao mmoja ni wa taaluma ya masikio, pua na koo, na mwingine ni mwenye taaluma ya kibingwa katika mambo ya moyo na mwingine mwenye taaluma ya kibingwa katika maswala ya mifupa yaani (*orthopedic surgeon*). Madaktari hawa watatu wapo kama madaktari bingwa.

Tatizo ni kutokuwa na madaktari bingwa katika eneo la watoto, eneo la akina mama wajawazito na kwa Serikali tunatoa tamko kwamba kama tulivyoainisha zoezi kubwa la kuongeza uwezo wetu wa kufundisha madaktari bingwa katika taaluma hizo na kwa mujibu wa kupandisha hadhi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Hospitali za Mikoa kuwa Hospitali za Rufaa za Mikoa zimepandisha pia mahitaji yake kutoka mahitaji ya madaktari 5 zamani sasa itakuwa na mahitaji madaktari bingwa karibu 30 kwa mujibu wa ikama hiyo ya hospitali ya rufaa ya Mkoa.

Katika tafsiri hii Serikali mwaka jana tuliajiri watumishi 8,000 na mwaka huu tunaamini baada ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kutoa kibali cha kuajiri madaktari na wauguzi ambao wataajiriwa.

Namthibitishia Mheshimiwa Munde kwamba tutahakikisha Mkoa wa Tabora kwamba watapata idadi ya kutosha kuhudumia Watanzania pale.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Maryam S. Msabaha swali la Nyongeza.

MHE. MARYAM S. MSABAHA: Mheshimiwa Spika, Ahsante naomba nami nimwulize Naibu Waziri wa Afya swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Madaktari wengi bingwa ambao wanakwenda kusoma nje kwa pesa za Serikali na wengi wamekuwa hawarudi kutokana na tatizo la kuboreshewa mishahara na maslahi yao.

Je nitahakikishaje madaktari ambao wanakwenda kusoma wamerudi kuja kuwasaidia Watanzania ambao wako Mikoani Hospitali zote za Mikoa na za Rufaa?

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USATAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam kama ifuatavyo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. DALALY PETER KAFUMU]

Madaktari bingwa wanapopata udhamini wa Serikali kwenda kusomeshwa nje na hata ndani tumeamua na tulisema kwenye Bunge hili kwamba watakuwa wanasantai mkataba wa kuendelea kufanya kazi na Serikali baada ya kumaliza masomo yao.

Taratibu hiyo itatumika ili kuweza kudhibiti kuhakikisha kwamba wanaotumia fedha za Serikali baada ya kupata elimu wanakuja wanawatumikia wale waliowachangia fedha hizo.

SPIKA: Naomba tuendelee na swali linalofuata.

Na. 36

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, Ahsante sana, najua umekusudia Mheshimiwa Khatibu Said Haji, Mbunge wa kudumu wa Konde.

Sheria ya kudhibiti Waganga wa Jadi

MHE. DKT. DALALY PETER KAFUMU aliuliza:-

Kumekuwepo na tabia ya Waganga wa Jadi kujitangaza kuwa wanatibu magonjwa yote yakiwemo magonjwa sugu kama UKIMWI, hali hii imesababisha wananchi wengi kuamini na kuacha matumizi ya dawa za hospitali pamoja na masharti ya magonjwa hayo na kupelekeea watu wengi kupoteza maisha:-

Je, ni lini Serikali itatunga sheria ya kudhibiti hali hiyo kama zilivyo za nchini India na China ili kuokoa maisha ya wananchi?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USATAWI WA JAMII
aliijibu:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)
[NAIBU WAZIRI WA AFYA]

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daktari Dalali Peter Kafumu, kutoka Igunga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tiba asili imerasimishwa kuwa tiba mojawapo ya huduma za tiba zinazotambulika na Serikali hapa Tanzania. Sera ya Afya ya Serikali ya mwaka 1990 ambayo ilifanyiwa mapitio mwaka 2007 inaitambua Tiba Asili kama mojawapo ya huduma za afya zitolewazo kwa wananchi hapa Tanzania.

Aidha Serikali kupitia Bunge lako tukufu katika mwaka 2002 ilitunga sheria ya Tiba Asili na Tiba Mbadala namba 23, kanuni ya maadili kifungu cha 10 (1) ambacho kinazuia mtu yelete kujitangaza bila kufuata taratibu za baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala. Kanuni ya dawa kifungu cha 15 (1) ambacho pia kinazuia mtu kujitangaza bila kibali cha baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera na Sheria hakuna mganga wa Tiba Asili anayeruhusiwa kujitangaza au kutoa matangazo yoyote kuhusu huduma anayoitaoa bila kibali cha baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala. Vile vile kwa kuwa suala la kujitangaza katika Tiba Asili linahusisha sheria mbili, sheria ya vyombo vyahabari na utangazaji na sheria ya Tiba Asili na Tiba Mbadala.

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na baraza la habari itaendelea kufuatilia masuala ya kujitangaza kunakofanyika na waganga wa Tiba asili na kuchukua hatua stahiki. Kutokana na kuwepo kwa sheria mbili zinazohusu matangazo ya tiba asili, sheria ya vyombo vyahabari na utangazaji na sheria ya Tiba Asili na Tiba Mbadala Serikali kwa sasa itaendelea kuzitumia sheria hizi kudhibiti matangazo yanayohusu tiba asili na tiba mbadala yasiyofuata taratibu za kisheria zilizopo.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kafumu swali la nyongeza.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA AFYA]

MHE. DKT. DALALI P. KAFUMU: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yamekidhi, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(1) Kwa kuwa Serikali inatambua kuwepo kwa Waganga wa Jadi wanaotoa matangazo kinyume cha sheria, Serikali inachukua mkakati gani wa kuhakikisha watu hawa wanaacha kufanya hivyo ili kuokoa maisha ya wananchi wengi ambao wanaamini matangazo na kwenda kwenye dawa ambazo hazina uwezo wa kutibu magonjwa yao?

(2) Serikali inaweza kulieleza nini Bunge hili pamoja na Wananchi wa Tanzania kuhusu matibabu ya Babu wa Loliondo, walifanya utafiti wakaona nini kuhusu dawa hizo na hatima ya matibabu hayo ikoje kwa sababu wengi tulienda tukiwa pamoja na Wabunge lakini sasa hatusikiki tena? Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana kumbe wote ni Loliondo, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USATAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu maswali 2 ya Mheshimiwa Dkt. Kafumu, Mbunge kama ifuatavyo:-

(1) Kwa mujibu wa sheria namba 23 ya mwaka 2002, matangazo yanakatazwa bila kufuata taratibu za kupitia Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala na kwa tafsiri hiyo anayetangaza anakuwa amevunja sheria na sheria inatangaza adhabu anayostahili kupata. Tulitoa agizo wakati wa mkuutano wa madaktari wa Mikoa na madaktari wa Wilaya kushirikiana na Wakurugenzi wao kulisimaia hili katika Wilaya zote nchini.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Nina taarifa baadhi ya Wilaya wamefanikiwa, na Wilaya nyingi bado hazijafanya maamuzi ambayo tulishayafanya. Narudia kuchukua fursa hii kutoa taarifa tena na kuwataka Wakurugenzi na Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya kusimamia zoezi hili kuhakikisha kwamba haya matangazo yanaondolewa mara moja.

(2) Kuhusu suala la Babu wa Loliondo, kwa upande wa Serikali kinachofanyika kikubwa ni kutafiti juu ya kufahamu usalama wa dawa inayotolewa kwa mlajji na pale usalama wa dawa unapothibitishwa kwamba hauna madhara kwa yule mtumiaji suala la imani juu ya kupona kutokana na kutumia dawa hiyo kwa mganga wa jadi ambaye amekwisha andikishwa ni swala la imani kati ya anayepokea tiba na yule anayetoa tiba ambaye kwa mujibu wa sheria ameruhusiwa kufanya hivyo.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, Ahsante sana, najua umekusudia Mheshimiwa Khatibu Said Haji, Mbunge wa kudumu wa Konde.

Mheshimiwa Spika moja ya tangazo lilioshika kasi sana kwenye magazeti takribani yote ya udaku ni suala la dawa la kuongeza nguvu za kiume na kurefusha maumbile ya kiume, tunataka kujua hili Wizara ya Afya imelithibitisha na kama hamkulithibitisha ni kwa nini kila gazeti la udaku linatoa taarifa hii kwamba kuna dawa ya kurefusha maumbile ya kiume na kuongeza nguvu hizo? Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Kwani si biashara? Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo. Matangazo yote kwa ujumla kama jibu langu la msingi hayaruhusiwi mpaka pale yawe yamethibitishwa na kuruhusiwa na Baraza la tiba asili na tiba mbadala.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CLARA DIANA MWATUKA]

Matangazo yanayoruhusiwa kwa mujibu wa sheria hiyo ni kuonyesha eneo ambalo yule mganga wa Tiba asili au tiba mbadala anatoa kwa maana ya kumwelekeza yule anayetaka huduma kwake aweze kufika kwake kwa urahisi na sio kutangaza uwezo wake wa kutibu ugonjwa wowote.

Katika tafsiri hii matangazo yote hayaruhusiwe yakiwemo haya yanayotoka katika magazeti ya udaku na kwenye sehemu nyingine. Kwa hiyo, ni suala sasa la baraza ambalo kwa mujibu wa sheria limepata mamlaka ya kulisimamia hili na tunawaomba wafanye kazi waliyopewa kwa mujibu wa sheria.

SPIKA: Ahsante sana naona sasa muda wangu leo unataka kuwa *exactly*. Sasa naenda Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundsi. Mheshimiwa Clara Mwatuka, atauliza swali hilo na Mheshimiwa Riziki.

Na. 37

Vifaa Mbalimbali vya Elimu Mashulenii

MHE. CLARA DIANA MWATUKA aliuliza:-

Katika miaka ya arobaini na saba Serikali ilikuwa inatoa vifaa vyote vinavyohitajika mashulenii kama vile madawati, vitabu, daftari na kadhalika. Hata hivyo kwa shule zile za kati, *Middle Secondary* walipatiwa chakula, sare na malazi pia na wazazi walilipa karo tu.

Je, Serikali ilitumia mbinu gani kufanikisha hayo yote isiweze kutumia mbinu hizo kufanikisha masuala ya elimu katika kipindi cha sasa?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI
aliibuu:-

Mheshimiwa Spika, ⁴² kwā niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundsi napenda kujibu swali la Mheshimiwa

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa Serikali imeanzisha Programu na Mipango mbalimbali ili kurahisisha ugharamiaji wa elimu. Mipango hiyo ni ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na Mipango ya Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES), ambayo inafanikisha utoaji wa vifaa mbalimbali vyta kufundishia na kujifunzia kuititia ruzuku ya uendeshaji (*Capitation Grant*), kwa kiwango cha shilingi 10,000 kwa kila mwanafunzi wa elimu ya msingi na shilingi 25,000 kwa mwanafunzi wa elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya jitihada mbalimbali na kupata mafanikio makubwa katika kuongeza fursa za Watanzania kupata elimu ikilinganishwa na hapo awali miaka ya 1960. Kutokana na mafanikio hayo, pamoja na changamoto ya idadi ya ongezeko la wanafunzi, tathmini ilifanyika na kuona kuwa, ugharamiaji wa elimu uwe kwa mfumo wa Serikali kushirikiana na wadau wengine (*cost sharing*), kama ilivyoelekezwa katika Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 1995, Kifungu Na. 10. Hivyo, natoa wito kwa wadau mbalimbali wa elimu, kuendelea kuchangia gharama katika utoaji wa elimu ili kuweza kutekeleza utoaji wa elimu bora nchini kwani uwezo wa Serikali hautoshelezi mahitaji yote kwa wakati huu.

SPIKA: Mheshimiwa Riziki Omar Juma, swali la nyongeza!

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Namshukuru pia Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri japokuwa hayatoshelezi.

(i) Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake amesema kwamba enzi za kikoloni ambazo tulitawaliwa na Waingereza na Wajerumani elimu ilikuwa ikitolewa kwa lengo mahususi. Kwa ajili ya kuwatayarisha Wananchi watakaofanya kazi kwa masilahi ya Serikali hizo zilizokuwepo hasa kupata watumishi waliokuwa wakihitajika. Naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri; je, elimu inayotolewa leo katika nchi yetu haina lengo mahususi? (*Makof!*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. RIZIKI OMAR JUMA]

(ii) Vitu muhimu vya kufundishia katika shule zetu hasa za sekondari ni vifaa vya sayansi, maabara na vifaa ambavyo ni vya kisasa ili kuweza kutoa vijana ambao watakuwa na elimu ya kutosha ya sayansi na waweze kuendana na soko la ajira katika ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia. Serikali ina mpango hasa madhubuti kuhakikisha shule zetu zote za sekondari zinajengewa maabara zenye vifaa vya kisasa ili vijana wetu wajifunze na waendane na soko hasa ukizingatia kwamba uchumi yetu umeongezeka pamoja na kwamba wanafunzi wameongezeka lakini na uchumi umekua?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru ahsante.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Riziko Omar Juma, kama ifuatavyo:-

Pale nilipotamka kwamba, lengo mahususi kwa elimu ya wakoloni ilikuwa ni kwa ajili ya kuwatafuta wafanyakazi wao wenyewe kwa ajili ya ofisi zao na wote tunajua tumesoma historia ya darasa la nne, darasa la saba, kidato cha pili mpaka kidato cha nne inasema hivyo; ilikuwa ina maana ya kutofautisha. Wakati huo na wakati huu malengo ni yale yale, lakini sasa hivi kuna utofauti kidogo wa namna tunavyotoa elimu yetu, lengo la zamani na lengo la sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vifaa vya maabara kwa kila sekondari; tulishaahidi kwamba, kila sekondari itakuwa na vifaa vya maabara na mwezi uliopita wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais akiwa Bagamoyo na mimi nilikuwepo, alitamka na kutoa agizo kwa Wakurugenzi wote kwamba, ifikapo mwaka 2014, Wakurugenzi wote kwenye shule za sekondari wahakikishe shule zinakuwa na umeme wa juu (*solar power*) ili angalau tunapopeleka vifaa vya maabara viweze kufanya kazi na kwa kupitia *Capitation Grant* hii ambayo nimesema shilingi 25,000 kwa kila mwanafunzi kwa upande wa sekondari, shilingi 12,000 zimetengwa pale kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI]

ajili ya kununua vifaa, vitabu, pamoja na vifaa vyatia
maabara kama ambavyo tumeagizwa kufanya hivyo.

SPIKA: Mheshimiwa Ndassa, swali la nyongeza!

MHE. RICHARD M. NDASSA: Ahsante sana
Mheshimiwa Spika. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri
ni lini Serikali italetaa taarifa ya vifaa viliviyosambazwa
baada ya kununuliwa kupitia chenji ya rada? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, naomba ujibu kwa kifupi
tu maana amesema ni lini.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:
Mheshimiwa Spika, ni kweli tumeshasambaza vifaa hivyo
ambavyo mimi niseme ni vitabu, kwa shule zote za msingi
nchini kupitia ile chenji ya rada na pale ilikuwa na matumizi
mawili, ni vitabu na madawati. Kwa hiyo, kwa upande wa
vitabu tumemaliza na sasa hivi tupo katika kuandaa
madawati kwa ajili ya kuyasambaza tena.

Mheshimiwa Mbunge anataka ile taarifa ambayo
niahidi tu kwamba, ikiwezekana tutaileta ili Wabunge wote
waweze kuona hasa kwenye Majimbo yao kwamba
tumepeleka vitabu vingapi katika shule kwenye Majimbo
yao.

SPIKA: Tuendeleee na swali linalofuata, Mheshimiwa
Nimrod Mkono, kwa niaba yake Mheshimiwa Njwayo!

Na. 38

Umuhimu wa Elimu ya Michezo Mashulenii

**MHE. JUMA A. NJWAYO (K.n.y. MHE. NIMROD E.
MKONO)** aliuliza:-

Nchi nyingi duniani hutoa kipaumbele katika elimu
ya michezo ya aina zote kuanzia elimu ya awali na hatimaye
kujipatia mafanikio makubwa katika mashindano ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JUMA A. NJWAYO]

kimataifa kama olimpiki na kadhalika, kinyume na ilivyo Tanzania; Sera yetu ya Elimu nchini haitoi kipaumbele katika elimu ya michezo katika shule za awali na za msingi na badala yake kuna mtaala wa haiba na michezo ambao hakuna bajeti yoyote inayokidhi mahitaji ya elimu hii kama vile viwanja, vifaa vya michezo, walimu wa michezo na kadhalika:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kufanya mapinduzi ya elimu hii ya michezo kwa shule zote kuanzia shule za awali hadi chuo ili kuinua viwango vya ushindani kimataifa?

(b) Je, Serikali itaanza lini kutenga bajeti maalum kwa kila mwaka kwa ajili ya walimu wanaofundisha michezo mashulenii kwa kupewa mafunzo maalum ili kuwaandaa vijana wetu katika mashindano ya klimataifa?

(c) Je, Serikali haioni kuwa ni wakati mwafaka kuomba msaada kutoka nchi marafiki kama China, India, Marekani na kadhalika, ili kurudisha hadhi ya kiwango cha michezo Tanzania?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mbunge wa Musoma Vijijiini, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya kila jithihadu kuimarisha michezo kuanzia shule za awali hadi vyuo vikuu. Katika kutekeleza hilo, Serikali imekuwa ikisimamia Mtaala wa Elimu ya Awali na Elimu ya Msingi kwa pamoja inayotekeliza ratiba ya shule iwe na vipindi vya matendo ya haiba na michezo. Pia vipindi vya michezo hufundishwa katika ngazi ya sekondari. Aidha, Vyuo vya Ualimu huandaa walimu wa kufundisha michezo katika shule za awali, msingi na sekondari. Vivyo hivyo katika ngazi ya elimu ya juu, shahada ya elimu kwa michezo imekuwa ikitolewa kwa wahitimu wa shahada ya kwanza ya elimu kwa lengo la

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI]

kupata walimu wa michezo katika vyuo vya ualimu na shule za sekondari. Kwa mantiki hiyo, elimu ya michezo inayotolewa katika ngazi zote za elimu ni kama nilivyo sema, elimu ya awali, elimu ya sekondari, elimu ya msingi na elimu ya vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuandaa walimu, Serikali inaendelea kuhimiza shule zote ziwe na vifaa vya michezo pamaja na viwanja. Aidha, inaimarisha elimu ya michezo kupitia vipindi vya michezo shulenii ili kufanya mapinduzi ya elimu ya michezo kwa ngazi zote kuanzia shule za awali hadi chuo kikuu. Sambamba na jitihada hizo, Serikali imeweka utaratibu wa kuwashindanisha wanafunzi na wanachuo katika mashindano ya michezo kwa shule za msingi (UMITASHUMTA), kwa shule za sekondari (UMISETA) na vyuo vya ualimu ama vyuo vyote (UMISAVUTA) ili kubaini vipaji na kuinua viwango vya ushindani kimataifa.

(b) Mheshimiwa Spika, wakati wa kufunga Michezo ya UMISETA iliyofanyika Kibaha Mkoa wa Pwani mwanzo Juni mwaka huu wa 2013, Serikali kupitia Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawaza za Mikoa na Serikali za Mitaa (Elimu), Mheshimiwa Kassim Majaliwa, iliahidi kuwaendeleza walimu wa michezo kwa kutenga bajeti maalum kila mwaka kwa ajili ya kuwapa mafunzo maalum walimu ili kuwaandaa wanafunzi wetu katika mashindano ya kitaifa na kimataifa.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikishirikiana na Taasisi na Mashirika mbalimbali ya Maendeleo yasiyo ya Kiserikali katika juhidi za kuendeleza elimu na michezo nchini. Aidha, Serikali inashirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la Finland, kuendesha mafunzo ya elimu kwa michezo na kutoa vifaa vya michezo kwa vyuo 12 vya ualimu pamoja na shule za msingi na sekondari katika Mikoa ya Mtwara, Lindi na Singida. Vilevile Serikali kwa kushirikiana na shirika hili, mwaka 2013 imezindua Mradi wa Kitaifa wa Kutoa Mafunzo na Vifaa kwa shule 60 za sekondari. Pia Serikali imekuwa ikishirikiana na makampuni na mashirika mbalimbali ya umma katika kuendeleza michezo shulenii.

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI]

Nachukua fursa hii kuyashukuru Makampuni na Mashirika ya *Vodacom*, *Tigo*, *Airtel*, *TTCL*, *Cocacola* na Mifuko ya Hifadhi za Jamii kama *NSSF* na mengine, kwa kuchangia na kudhamini Mashindano ya Uendeshaji wa Michezo Elimu ya Msingi na Sekondari mashulenii.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza. Kabla sijafanya hivyo, naomba kutumia nafasi hii kuipongeza Timu ya Taifa ya Tanzania Bara, *Kilimanjaro Stars*, kwa ushindi iliouopata jana dhidi ya Timu ya Burundi na hasa nampongeza sana kijana wetu, Bwana Mbwana Ali Samatta, kwa kufunga goli zuri na kutumia uzoefu wake wa kimataifa kutuwakilisha Watanzania. (*Makofii*)

Baada ya maelezo hayo ya awali, naomba sasa niulize maswali mawili kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Shule nyingi za Kata zilizojengwa hapa Tanzania zilijengwa na Wananchi na kwa utaratibu wa kawaida hamasa kubwa ilikuwa kuwa na madarasa tu, hakukuwa na mpango kamambe uliowekwa wa kujenga viwanja vya michezo. Je, Serikali sasa inazisaidiaje shule hizo Tanzania nzima kuhakikisha zinakuwa na viwanja vya kisasa na bora ili kuinua suala la michezo kuanzia kwenye shule zetu za msingi na sekondari? (*Makofii*)

(ii) Kwa kuwa tunacho Chuo cha Michezo kule Malya Mwanza lakini kimekuwa kikipewa bajeti ndogo na hata udahili wa wanafunzi umekuwa mdogo. Je, kwa nini Chuo hiki sasa kisipewe kipaumbele maalum kibajeti ili kitumike kuongeza wataalam pia kuinua ari na viwango vya michezo nchini ili siku chache zijazo tufahamike kimataifa kwa kutumia Chuo hiki?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Mheshimiwa Spika, kuhusu shule za sekondari wakati zinajengwa kulikuwa na sintofahamu ya masuala ya viwanja, ni kwamba, tusingeweza kusajili shule hizo bila kuwa na maeneo ya kuwa na viwanja. Kuna wakati fulani Serikali ilifuta masomo haya ya michezo mashulen; UMISETA, UMITASHUMTA na baadaye hata vigezo vya usajili wa shule pale ikaonekana viwanja siyo lazima sana. Baadaye tena ilikuja ikarudisha na sasa hivi viwanja ni moja ya vigezo ili uweze kusajiliwa kupata shule ya sekondari.

Vilevile si vibaya huwa tunasema kwamba, shule ambazo hazina viwanja zinaweza zikafanya michezo kwenye shule jirani hata kama pana shule ya msingi ama shule ya sekondari na hilo linafanyika katika shule zote za sekondari nchini.

Swali la pili kuhusu Chuo cha Malya kilichopo Mwanza kwamba, tukiimarishe kwa ajili ya michezo. Mimi naomba nichukue hili ili niwasiliane na Wizara ya Michezo na Utamaduni, tulifanyie kazi pamoja na Wizara ya Elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI).

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini kutokana na muda. Mheshimiwa Eugen Mwaiposa atauliza swali hilo, kwa niaba yake namwona Mheshimiwa Blandes.

Na. 39

Kupeleka Umeme Maeneo Mbalimbali Chanika

MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MHE. EUGEN E. MWAIPOSA) aliuliza:-

Umeme ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme kwenye maeneo ya Mvule na Kitonga - Kata ya Chanika,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GOSBERT B. BLANDES]

Kifaru, Majohe, Bombambili na Nyang'ando - Kata ya Kivule na Nzasa - Kata ya Chanika ili kutoa fursa kwa Wananchi kupata maendeleo ya haraka zaidi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Eugen Elishiringa Mwaiposa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia *TANESCO*, inatekeleza Mradi wa Kupeleka Umeme Katika Maeneo ya Majohe, Bombambili, Nzasa na Mvuti. Kazi ya Mradi huu zitahusisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 11 yenye urefu wa kilomita 17.1; ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 41.5; kufunga transforma 10 zenyewe uwezo wa KVA 200 na kuwaunganishla umeme wateja wa awali wapatao 3,200.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu unakadirwa kugharimu jumla ya shilingi bilioni 2.112 na umeingizwa kwenye bajeti ya *TANESCO* ya mwaka 2014 na kazi za Mradi zinatarajiwa kuanza mwezi Januari, 2014 na kukamilika mwezi Juni, 2014.

SPIKA: Mheshimiwa Blandes, swalii la nyongeza!

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Spika, nashukuru na nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri sana. Pamoja na hayo, nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Ahadi hii imekuwa ni ya muda mrefu na Mheshimiwa Mwaiposa amekuwa akiulizia na majibu yamekuwa yakifanana hivi. Nilitaka kujua majibu haya ni ya mwisho kwamba Mheshimiwa Mwaiposa asiulize tena?

(ii) Kwa kuwa Serikali iliahidi kupeleka umeme katika Jimbo la Karagwe ambako ninatoka na Serikali imekuwa ikitisema kwamba mchakato wa kumpata mzabuni

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. GOSBERT B. BLANDES]

unaendelea. Nataka kujua mzabuni atapatikana lini na kazi hiyo itaanza lini?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mbunge wa Karagwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli majibu juu ya Mradi ya maeneo ya Chanika na suala zima la usambazaji wa umeme, yamekuwa yakiulizwa sana na Mheshimiwa Mbunge. Nachukua nafasi hii kumhakikishia kwamba, pamoja na changamoto za kibajeti iliyonayo *TANESCO*, kwa sababu Miradi hii inafanywa na *TANESCO* na kwamba maeneo haya ya miji mikubwa hayapo katika mpango wa umeme vijijini; kwa hiyo, pamoja na changamoto hizo za *TANESCO* lakini sasa wametuhakikishia kwamba, wameweka kwenye bajeti na hii ni hatua muhimu. Mimi mwenyewe nitasimamia kuhakikisha maeneo haya yanapata umeme sasa.

Swali la pili juu ya Jimbo la Karagwe na Mradi wa *REA*. Nichukue nafasi hii kumhakikishia Mbunge wa Karagwe, nimefika Karagwe na mimi mwenyewe niliahidi, nikuhakikishie kabisa miradi hii lazima tutaitekeleza. Tumechelewa tu kumpata mkandarasi, lakini Desemba hii mchakato utakamilika, Januari lazima kazi ianze.

Nachukua nafasi hii kuwahakikishia na Wabunge wengine wa mikoa ambayo ilikuwa imekosa wakandarasi kwa kupitia Miradi ya *REA* kwamba, mchakato ule unaishia ukingoni, wamenihakikishia kabla ya tarehe 15 ya mwezi huu, watatangaza wakandarasi hao na kama ikizidi basi tutakapokuwa tunasherehekea Xrismas wakandarasi watakuwa wanajulikana wa kila mkoa na kazi zitaanza mwezi Januari kwa kasi kubwa sana. (*Makofii*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na leo nina kazi ya ziada.

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[SPIKA]

Ninao wageni sijui wako wapi; tuna wageni saba wanatoka kwenye asasi inaitwa *Moslems and Christians Brotherhood Society*, kwa kifupi MCDS, wanaongozwa na Mwenyekiti wake, Ndugu Hamad Rajab Tao. Hawa ni watu ambao wanajaribu kuona tunaishi kindugu, kirafiki, bila mgawanyiko wowote ule wa misingi hiyo. Naomba wasimame walipo kama wapo. Kumbe hawapo, aah ahsante. Karibuni sana, fanyeni kazi hiyo kwa dhati kwa sababu umoja na upendo tunauhitaji sana katika nchi yetu na ndivyo tulivyolelewa. Ahsanteni sana, karibuni. (*Makof*)

Shughuli za kazi; Mwenyekiti wa Kamati wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Edward Lowassa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Msekwa B, watakuwa na kikao chao.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitangaze tunayo tanzia; hivi leo tumepata msiba wa askari, Koplo Mwita Maro, ambaye alikuwa anafanya kazi ya ulinzi katika mageti yetu. Juzi alikuwa anajisikia vibaya akapewa ruhusa ya kwenda kupumzika, lakini alipojaribu kwenda hospitali hakufika na kuamkia leo asubuhi amefariki. Mazishi yanaandaliwa nyumbani kwake Kikuyu, Mtaa wa Kikuyu Chidachi, Manispaa ya Dodoma na Ofisi itashiriki katika kuandaa mazishi hayo.

Yule kijana mpaka juzi alipokuwa kazini alikuwa analinda geti hili mnaloingilia ninyi Waheshimiwa Wabunge. Mwenyezi Mungu ampumzishe mahali pema peponi. Amina.

MWONGOZO WA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, leo nimesema nina muda mfupi, sasa haya maneno mengine kama ni ya maswali, naomba msiniulize kwa sababu nimetoa msimamo tayari. Nani alisimama kwanza? *Are you sure?* Mheshimiwa Wenje!

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 63(1). Leo nilipouliza swali na majibu niliyopewa na Mheshimiwa Waziri, Kanuni za Kudumu za Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Toleo...

SPIKA: Unataka mwongozo nifanyeje?

Mwongozo unaniuliza nifanyeje? Usiniliulize habari ya Halmashauri sizijui!

MHE. EZEKIEL D. WENJE: Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), alipokuwa akijibu swali langu alilidanganya Bunge na Taifa na ndiyo ninataka ku-substantiate kwenye maelezo ninayotaka kutoa hapa.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, ninaomba kukukatisha, uniwie radhi. Labda huwa hamuwi katika kiti cha Bunge; nimekwishatoa maelezo, kama kuna maswali ambayo ninyi hamkuridhika, ni haki ya Mbunge kuniandikia mimi kwamba hakuridhika na swali hili. Kwa sababu ya lile swali uliloniletea nitajibu, lakini tukianza kubishana, mimi sijui hata habari za Halmashauri. Kusema mwongo sijui.

Mheshimiwa Mbunge, sasa ninakuagiza kaniandikie uniletee na hata mwagine yejote atakayeuliza habari za maswali, nimekwishatoa mwongozo kutoka swali la Mheshimiwa Seif, nikamwambia juzi tena ninafikiri ni Mheshimiwa Moses Machali, aniyandikie, huo ndiyo utaratibu. Tukianza kubishana hapa hatutamaliza, wala siyo maswali yetu. Mheshimiwa Mnyika!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nitakuandikia na kukuletea.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa mujibu wa...

SPIKA: Hiyo *microphone* ya Mheshimiwa Moses Machali inaleta fujo, mstari huu Wataalam muuangalie.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), kuomba mwongozo wako kuhusiana na jambo ambalo limetokea mapema asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Spika, wakati nimesimama ninamwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, walikuwa wakiguna na kama kuzomea hivi. Hali ambayo kwa mujibu wa Kanuni zetu, hakuna mahali ambapo inaruhusiwa kumzomea Mheshimiwa Mbunge wakati anaendelea kuuliza maswali au kuzungumza Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Kiti chako killinitaka pia niondoe maneno yangu, nikauliza ni wapi ambapo imeandikwa kwamba Mbunge mmoja kuvunja Kanuni kwa mujibu wa Kanuni zetu halafu Kiti kisimkemee, lakini Mbunge aliyesema watu wakae kimya ili aweze kuendelea Kiti kikaona Mbunge yule ni mtovu wa nidhamu na ni mkosefu?

Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako iwapo inaruhusiwa humu Bungeni, kama Mbunge amesimama anazungumza, ni ruhusa kwa Wabunge wengine kutoa hali kama vile ya kejeli au kuzomea kwa namna yoyote ile? Kama inaruhusiwa jambo hili, ninakiomba Kiti chako kitoe mwongozo.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, unajua katika maisha ya humu ndani, neno kuvumiliana ni muhimu sana. Bahati mbaya na ninyi mnaniingilia kazi yangu, mimi nina kazi ya kuongoza vikao, siongozwi na mtu mmoja mmoja huko aliko. Kwa hiyo, ukikuta nimekfumbia macho, maana yake sisikilizi na wewe ungelinisikiliza. Kwanza, wewe ningelitaka kukuchukulia hatua baada ya kubishana na mimi ndiyo ningelikufukuza kabisa, lakini na mimi nikavumilia. (Makof)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

Waheshimiwa Wabunge, ninachokisema, uvumilivu ni wa muhimu sana. Wewe ulikuwa una hoja yako, tena ilikuwa nzuri kabisa, ila ukaongozwa vizuri kwa kuwasikiliza hao jamaa. Umewasikiliza hao ukaharibu hoja yako. Hoja yako ilikuwa nzuri sana, ndipo niliposema hasira ni hasara. Ulichouliza kilikuwa muhimu sana na Wananchi wangelifaidika sana kuliko ulikochepukia, hiyo haisaidi kitu.

Waheshimiwa Wabunge, uvumilivu ni kitu cha maana sana. Haya mambo, mimi ndiye ninayeongoza kikao hapa. Kwa hiyo, ninaomba sana mtuelewe hivyo. (Makofi)

MUSWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni wa Mwaka 2013
(The Referendum Bill, 2013)

*(Kusomwa Mara ya Pili)
(Majadiliano yanaendelea)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nitakaowaita kama hawapo sirudi nyuma. Ninaye Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba na Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy ajiandae. Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, wasiokuwepo leo sirudi nyuma!

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa shukrani za dhati kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia katika Muswada ulioko mbele yetu. Kabla ya kuchangia, ningeliomba uniruhusu nilishukuru Bunge lako au nikushukuru wewe binafsi, Serikali ya Muungano, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa kunisaidia katika matibabu ambayo kipindi cha Kikao cha Kumi na Mbili chote sikuhudhuria hapa. Nilikuwa na matatizo, nilikuwa siwezi kusimama wala Kukaa kitako, lakini sasa nimerudi ninashukuru na niko jadidi. Ahsante sana. (Makofi)

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

SPIKA: Ahsante na sisi tunamshukuru Mungu.
(*Makofi*)

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Mheshimiwa Spika, nimesimama kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni (*The Referendum Bill, 2013*).

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Ninaiunga hoja hii mkono ikiwa ni pamoja na marekebisho yaliyofanywa na Kamati ya Katiba na Sheria. Nawapongeza Waziri wa Katiba na Sheria na Timu yake na Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa Tanzania Bara na Zanzibar, kwa kazi hii nzuri waliyoifanya na kutufikisha hapa tulipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesema ninaunga mkono Sheria hii na ninaunga mkono *NEC* wasimamie utaratibu wa kura za maoni kwa Tanzania Bara na *ZEC* wasimamie utaratibu wa kura za maoni kwa Tanzania Visiwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hawa ndiyo waliokuwa wamesimama na kusimamia chaguzi zilizopita na wana uzoefu wa kutosha na hata wametufikisha hapa. Kubwa zaidi ninalotaka kulizungumza ni kwamba, suala la Masheha, lillipopigwa kelele hapa kwamba hawafai, ninaunga mkono tena kwa kusema kwamba, Masheha wamefanya kazi nzuri na waendelee kufanya kazi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninawashangaa wale wanaosema kwa Zanzibar Masheha hawafai. Kuna usemi unasema: "Wafadhiliika Wapundaka." Kwamba, yule anayekufadhilli, unameuzea punda unampandia. Hebu watuambie ni nani hapa aliyetoka Zanzibar amefika hakupita ndani ya mikono ya Masheha? Masheha hawakuwekwa na Baraza la Wawakilishi?

Mheshimiwa Spika, tujiulize vilevile Serikali ya Mapatano ya Zanzibar, kura za maoni waliosimamia ni akina

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. KHERI KHATIB AMEIR]

nani; siyo Masheha hao hao? Uchaguzi uliofanyika wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Wabunge, waliosimamia ni akina nani? Kubwa zaidi Sheria ya kuweka Masheha imetungwa na nani, si na Baraza la Wawakilishi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, hapa pana tatizo. Kwa bahati mbaya watu wanasema mnafiki, yaani mtu mwongo hajifichi, akikaa katika jamii ya watu ataonekana. Ninaogopa kusema kuna kauli mbaya zaidi ya kusema, lakini watajaza wale wanaojua Kiswahili kwamba hafichi kidole, lazima atakionesha kidole chake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kuna wanaoleta mvutano wa siasa katika Bunge. Hili ni Bunge la Watanzania, ndani ya Bunge humu siasa yako inakaa nyuma, wewe unazungumza masuala ya Bunge yanayohusu nchi na yanayohusu Wananchi wote. Wewe Mbunge inawezekana unacho chama chako, lakini waliokuchagua siyo wa chama chako peke yake. Ukisimamia katika misingi ya chama chako, kuna hatari unakoelekea hukujui. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kuna rafiki yangu mmoja aliniambia, alisema Kheri katika siasa zetu za Tanzania kuna vyama vya siasa na kuna vyama vya harakati. Wanasema kwamba, chama cha harakati hakiwezi kikawa chama cha siasa kwa sababu bado kipo mbioni na hakijui nini kinafanya.

Mheshimiwa Spika, tunapokuwa humu Bungeni, tuondoe suala la harakati, tuwe kama vyama vya siasa. Harakati walizonazo ziachwe huko nje, wakitoka humu waende wakagombane nje ya Bunge na ugomvi wa nje wasituletee humu ndani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ninaiunga mkono hoja hii, kwa asilimia mia kwa mia.

Kwa machache haya niliyoyazungumza, nilitaka kuwakilisha dhamira yangu na dhamira ya walionichagua, dhamira yangu na dhamira ya Watanzania waliokuwa na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. KHERI KHATIB AMEIR]

itikadi sahihi na dhamira yangu na dhamira ya wale ambao wanaitakia mema nchi hii.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. ABDALLAH SHARIA AMEIR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nizungumze walau mawili, matatu. Ninamwomba Mwenyezi Mungu, aniwezeshe yale nitakayoyazungumza, kama nitakuwa nimeyakosea, pamoja na wewe Mheshimiwa Spika, mnisamehe.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nimesema hivyo? Kuna msemo wa waimbaji wanasema, itabidi na mimi niseme kidogo: "Bubu hutaka kusema mambo yanapomzidia. Imenibidi mwenzenu leo ninasimama mbele yenu kauli yangu kuitoa." Hayo ni maneno ya waimbaji siyo yangu mimi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninapenda kumpa pole Sheha wangu wa Shehia ya Tomondo, ambaye katika kipindi cha uandikishaji wa Daftari, alimwagiwa tindikali kwa sababu ya kufuata sheria alizopewa. Hakumwagiwa kwa sababu nydingine yoyote, alimwagiwa tindikali kwa sababu ya kufuata sheria alizopewa na Baraza la Wawakilishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Tundu Lissu, alizungumza na alisema ana imani na Wazanzibari na anawatetea Wazanzibari. Ninasema kwamba, asitudanganye, hana imani ya Wazanzibari wala hana nia ya kuwatetea Wazanzibari wala Watanzania. Anajitetea ye ye mwenyewe na anakitetea Chama chake cha CHADEMA. (*Makofii*)

Ninayasema haya, mwanangu niliyemzaa yule pale alizungumza jana, akasema hatupendi Wazanzibari na kweli, Kambi ya Upinzani siyo Kambi ya Upinzani ni Kambi ya CHADEMA. Wazanzibari hakuna Wapinzani; mbona hakuna hata mmoja aliyepewa nafasi aliyemtetea kwamba

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ABDALLAH SHARIA AMEIR]

na wao wawe Mawaziri Vivuli? Huu ni uongo na uzandiki ndani yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika taarifa yake alimnukuu sana Naibu Waziri anayeitwa Mahadhi. Mahadhi kama kasema basi kasema kama Mahadhi hakuwasemea Wazanzibari. Ninasema kama kasema, sina uhakika, nadhani yeze mwenyewe akipata nafasi atasema kwamba alisema au hakusema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, haya tuliyoyapitisha hapa, yaliyoletwa hapa, tumeyajadili na tumeyapitia wakati mwingine mpaka saa nane za usiku na saa saba za usiku na tuliondoka na azimio moja kwamba, tunapeleka hili. Leo ukitoka ukiwa unayazungumza aliyyoyazungumza Waziri au Naibu Waziri, huyasemi yale tuliyokubaliana, mimi ninadhani huu ni unafiki na siyo ukweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi ninasema ndugu yangu kama hana la kusema basi anyamaze au ayaseme ya CHADEMA wanafukuzana kwa nini? Hayo ndiyo ya kuyasema eti, hapa atuachie Wazanzibari wenyewe na tumo tunaweza tukasema kama tunavyosema. Bubu mimi lakini ninasema, tunaweza kusema na tunaweza kuyazungumza ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ninasema Wanzibari tupo wenye na tunaweza kuyazungumza wenye. Tulikubaliana kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa na leo tumo ndani ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa Wazanzibari. Kwa hiyo, mtu atakapokuja azungumze masuala mazima yanayohusu kile kilicholetwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tujuje kwamba sisi tuna dhamana mbele ya Mwenyezi Mungu. Tutahukumiwa kwa lile ambalo tutalifanya kinyume na matwaka ya waliotuleta hapa.

Mwenyezi Mungu, ametuumba sisi na ametuweka katika madaraka haya si kwa sababu ya uwezo wetu, yeze

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ABDALLAH SHARIA AMEIR]

mwenyewe ndiye aliyetuleta na alijua kwamba hawa wanaweza wakafanya kazi ya kuwatetea wale waliowachagua. Sasa tuje hapa tuzungumze masuala mazima ambayo yanahusu Watanzania. Hizi Sheria tunazopitisha ni Sheria za Kura ya Maoni. Kura ya Maoni kuna ndiyo na hapana. Kweli Watanzania wote wanaweza wakajiandikisha, lakini ni kweli watapiga wote kura ya kusema Ndiyo na Hapana, haiwezekani. Tukiangalia takwimu zilizopita za uchaguzi, Watanzania wangapi wamejiandikisha na wangapi waliopiga kura! Sasa tusivutane tukafika pahala tukahisi tunakokwenda hatukujui kumbe tunakujua.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kusema haya ya dhati ndani ya moyo wangu. Ninawaomba sana ndugu zangu wa *CUF*, sisi ni wamoja, kama sisi ni wamoja basi twende katika umoja ambao tumekwenda nao. Kama kuna kasoro basi tukae wenyewe tuzirekebishe kasoro zetu, tusije tukawa tunazungumza mambo ambayo hatujatumwa na Wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana, uvumilivu lazima uwepo kama ulivyosema. Walisema tukanyamaza na sasa hivi tuseme wanyamaze. Kwa nini wanaumwa wanainuka kwani sisi tulikuwa hatujui kusema, kaeni kama tulivyokuwa tumekaa sisi. (*Makofii*)

CUF hamfanyi kwa masuala ya Wazanzibari siyo kweli. Mnayoyaleta hapa siyo masuala ya Wazanzibari. Mnayaleta hapa masuala mnayoyajua ninyi wenyewe. Tumekubaliana tuwe wamoja tutekeleze yetu ya Wazanzibari kwa pamoja, hamuwezi tuambiwe kwamba haya hatuwezi. Baraza la Wawakilishi ndiko kunakohusika kwa kusema na siyo hapa. Wapelekeeni Wawakilishi kwamba huu Muungano tulionao haufai, basi tukae nao pembeni kwani kuna ulazima gani! Tusidanganyane jamani. (*Makofii*)

Tusiwendanganye Wananchi wetu tukawaweka katika nafasi ambayo hawaihitaji. Katiba mpya ndiyo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ABDALLAH SHARIA AMEIR]

wanayoihitaji Watanzania, hawahitaji malumbano ya vyama.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nasema naogopa sitaweza kusema kumbe naweza eeh! Wale ambao hawapo tayari na hili watupishe, tunasema tunakubaliana na mimi nasema nakubaliana na ZEC isimamie kura ya maoni Zanzibar na NEC isimamie kura ya maoni Tanzania Bara. Naunga mkono asilimia mia moja na kumi, siyo kumi na moja, mia moja na kumi. (*Makof!*)

Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na ninaomba radhi kama nimekosea katika kuzungumza yangu, niseme kwamba nilikosea kwa bahati mbaya lakini sikukusudia kufanya hivyo. Ahsante! (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Lusinde, atafuatiwa na Mheshimiwa David Silinde!

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuwezesha kuamka salama. Vilevile nakushukuru wewe binafsi kwani umekuwa ukiliendesha hili Bunge kwa uaminifu na umahiri mkubwa na umekuwa ukituvumilia vijana wako wakati moto unapowaka kidogo na kutusihii turudi kwenye utaratibu.

Mheshimiwa Spika, naomba niuchangie Muswada huu wa upigaji kura za maoni. Mengi yamesemwa na umezungumzwa wasiwasi wa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge na wengine wakafika mbali kwamba, huenda tukipitisha sheria hii tutakuwa tunakinanza na matakwa ya Katiba ya Nchi. Wabunge haohao walikuwepo wakati tunapitisha Sheria ya mwanzo ya Mabadiliko ya Katiba na hakuna kifungu hata kimoja kwenye Katiba kinachoruhusu ile Sheria itungwe; pale hatukuwa tunavunja Katiba, lakini leo tupo awamu ya tatu sasa tunakwenda kwenye kukamilisha hii kazi, tunavunja Katiba! Vyama vyao vimeteua mpaka Wajumbe kwenye ile Tume, pale

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE]

hatukuwa tunavunja Katiba, lakini leo tunataka kutunga sheria yenyewe ya upigaji wa kura za maoni hapo sasa tunakinzana na Katiba!

Mheshimiwa Spika, mambo haya tukiyaacha tu yaendelee hivihivi kwamba ni kweli kila Mbunge anaruhusiwa kusema anachoweza kusema humu ndani ya Bunge, tutakuwa tunapotosha Umma wa Watanzania. Kinachotungwa hapa ni kuwaruhusu Watanzania wapige kura za maoni. Mimi kama Mbunge naweza kuwa jambo moja naliunga mkono na lingine siliungi mkono, lakini mwisho wa siku wengi watakavyoamua pamoja na mimi tutakuwa wote tumeshiriki katika kuitunga Sheria ya Kura za Maoni.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kwa maoni yangu nataka niishauri Serikali kwamba, mambo yanayopigiwa kelele hapa siyo huu Muswada bali ni nia tulizonazo baadhi yetu. Unajua kusudio lako kama hautaki kulitamka moja kwa moja unaweza kuwa unazungushazungusha tu. Nawashauri Serikali hivi kwa nini tusingeandaa Sheria ya Kura za Maoni lakini ya Wananchi kujibu tu wanataka muundo wa Serikali wa namna gani maana hilo ndiyo linaloleta tabu? Wananchi wangepiga kura kwanza kuhusu muundo wa Serikali moja au mbili, tatu au nne na kadhalika halafu ndiyo iletwe kwenye Bunge tuje tutunge, tungetunga kitu ambacho kina *consensus* ya Wananchi kuliko hapa tunatunga sheria kisha tunaipeleka kwa Wananchi na wanaikataa tunarudi tena hapa; tutafanya mchezo huu mpaka lini?

Mheshimiwa Spika, mawazo yangu yalikuwa hayo.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye suala la kwa nini Watanzania waliopo njie wasipige kura. Mimi niliwahi kusema hapa Bungeni na leo narudia kusema kwamba, ukifanya safari na mtu ambaye hataki kwenda atakusumbua sana! Kila utakapomwambia ongeza mwendo yeye atapunguza, kila utakapomwambia jua linazama ongeza mwendo, atatembea taratibu atakwambia miguu imechoka, kumbe nia yake hataki kwenda. Leo hata hili tukilikubali, bado

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE]

tunajua kuna Watanzania wengine wako nje kihalali na wengine hawako kihalali, yaani itatupa tabu tu na wasimamizi wa hivyo vituo watakuwa Mabaloi watawakataa tena whatasema ni wa CCM. Tukimaliza hilo tukakubaliana nalo watakuja na lingine kwamba wafungwa wapige kura. Mimi nawaelewa hawa, lengo lao hawataki kwenda huko tunawaburuza tu lakini miyo yao haipo tayari kwenda huko. Wataibuka na hoja kila kukicha. (*Makofii*)

Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, leo hawa wanamsifu Rais kwa sababu moja tu kwamba, Mheshimiwa Jakaya ni Mwanadiplomasia, siyo kwamba anapowakubalia hawa anawakubaliana kwa kuwa wanafanya vizuri, hapana! Refa ukiwa unachezesha mpira kati ya timu nzuri na timu dhaifu, wakati mwingine ni lazima ulee mechi; ndiyo anachofanya Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, analea mechi isije ikavunjika katikati.

Sasa wao wanafikiri Rais anawapenda, *no*, Rais anachezesha mechi, ni Mwanadiplomasia na anajua hapa hii timu imeshafungwa magoli saba, nikiendelea kupuliza *penalty* hawa whatasusa, sasa ni bora niwaruhusu twende nao hivyo hivyo, wanacheza rafu tunaenda nao hivyo hivyo. Msije mkafikiri kwamba, Rais anawaheshimu, hamna lolote. Ninataka niwaambie na siku ile nilisema kwamba, katika ndoa, niliishia hapo, mwanamume anamuoa mwanamke kwa ujumla wake, hamuoi kwa kitu kimojakimoja. Kama ingekuwa mwanamume anamuoa mwanamke kwa kitu kimojakimoja, inawezekana kidole alichonacho mkeo wewe hukipendi, lakini kwa ujumla wake zile sifa zake zinasababisha umuoee.

Wenzetu wanataka kila kitu kiwe kizuri, hata wanawake wanatukubali sisi kwa ujumla wetu, hawachuji kitu kimojakimoja. Kuna kucha unayo, mkeo hataki lakini anakubali kwa sababu ya ujumla wa vitu vyako ulivyo navyo na busara yako uliyonayo. Leo hawa wanatulazimisha tutunge Katiba ya ajabu kabisa, Katiba ambayo itakuwa haina dosari kabisa.

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE]

Nimemkiliza jana Mheshimiwa Mbunge wa Ubungo, ambaye mimi ninamheshimu sana, anazungumzia dosari tu na analamu kwa nini Jimbo lake lilitangazwa la mwisho; mbona huipongezi Tume kwa nini Jimbo la Musoma Mjini lilitangazwa la kwanza na mlisinda CHADEMA? Jimbo la kwanza kutangazwa kwenye uchaguzi ni la Musoma Mjini, ambalo walishinda CHADEMA na waliolitangaza ni walewale waliolifanya Jimbo la mwisho liwe la Mheshimiwa Mnyika. Sasa pale wamekosea, lakini huku wamepatia; vitu vya ajabu sana hivi! (*Kicheko/Makofi*)

Hebu tuambizane ukweli, ujue siku hizi imekuwa sasa ni kawaida mtu hata akisimama kwenye foleni ya ATM akaenda akakuta mtando haufanyi kazi anasema CCM hao, kama huyo mtu ni wa CHADEMA anasema hawa ni CCM. Aah, mitando wakati mwingine inagoma! Jimbo langu mimi mwenyewe nilishinda kwa kura zaidi ya elfu thelathini na wapinzani wangu kwa ujumla wote walipata 1,600, lakini matokeo yalitangazwa baada ya siku saba, kila ukienda wanasema sijui kwenye *computer* haziingii na kadhalika, lakini baadaye wakatangaza, haikuwa nongwa ila la Mnyika tu ndiyo lilitakiwa litangazwe la kwanza!

Sasa hawa Tume watatetewa na nani maana humu ndani tuna Wabunge wawili wa Mahakama, hakuna Wabunge wa Tume? Kwa hiyo, nimeona na mimi niwatetee Tume jamani, vitu vingine ni mitambo tu inaweza ikakwamisha ukaenda ukaambiwa uje baadaye. Wakati mwingine hata kwenye *internet* unakosa mtando unalazimika kusubiri, sasa kusubiri ndiyo iwe tatizo kwamba tulimshinikiza tulimlazimisha? Mimi sioni kama hiyo ni sahihi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba, kuna Mbunge mmoja jana ameonesha hofu, anasema tabu waliyoipata kwenye uchaguzi. Sasa hivi kweli tunataka tutunge Katiba ambayo hakutakuwa na shida kwenye uchaguzi? Haiwezekani! Yaani unataka kachumbari halafu hutaki pilipili, ujue wewe si mlaji wa kachumbari!

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE]

Mtu yeote anayetaka kucheza mpira wa miguu, rafu ni sehemu ya mpira wa miguu. Sasa kama hutaki mwanao akanyagwe, mwambie asicheze mpira. Wanasesma eti ooh, sisi tulipata tabu, tena tabu mtakayoipata itakuwa kubwa kuliko ile. Kama suala ni uchaguzi tu, uchaguzi wote huwa unakuwa ni wa nguvu.

Mheshimiwa Spika, nataka nikwambie kwamba, tusiwedanganye watu kwamba tunataka tutunge Katiba ambayo uchaguzi utakuja kwa mtelezo tu, hakuna kitu kama hicho. Kila mwaka wa uchaguzi hata ukivichukua vyama vyenyewe ndiyo kunakuwa na migogoro. Wewe angalia tu hata vyama vya siasa vyenyewe, mwaka wa Uchaguzi wa NCCR Mageuzi ndiyo Kafulila alipoingia kwenye matatizo. Mwaka wa uchaguzi wakati ule Marehemu Chacha Wangwe aliingia kwenye matatizo. Mwaka wa uchaguzi ulimwingiza kwenye matatizo Kabourou. Mwaka wa uchaguzi Zitto ameingia kwenye matatizo. Uchaguzi wowote una shughuli zake. Kwa hiyo, mtu anayesema eti ooh tulilingia kwa tabu kwa hiyo tutunge Katiba ambayo itatuingiza kirahisi, hilo jambo halipo; tabu itakuwa palepale. (*Kicheko*)

Sasa hivi tunasema tunataka kuishi kidijitali. Chukulia mimi nina kijiji kimoja kinaitwa Matembe, pale Matembe ili ufile kwenye shule ya msingi iliyopo karibu iko kilomita 18, sasa naitaka Serikali kama haiwezi kuwasogezea kituo wapiga kura wa eneo lile kwa kutumia gari, basi ijenge haraka sana shule ya msingi pale ili wapiga kura wapigie pale. Tunapozungumzia gari la wapiga kura, tunazungumzia kuhusu kusogezza huduma wakati wa uchaguzi. Sasa ukisema kila kitu wewe una wasiwasi nacho, hivi kweli tutaishi kwa wasiwasi? Unapolala usingizi ni rafiki wa kifo, mbona huna wasiwasi na usiku unalala? Ukija huku ooh nina wasiwasi; una wasiwasi wa nini? Wasiwasi wa kitu gani? Hapa hatuwezi kukaa kwa ajili ya wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge jana wameingilia Mihimili mingine. Ndugu zangu kama Baraza la Wawakilishi limeshindwa kazi, nendeni

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE]

mkawaambie kulekule Wawakilishi wenu. Baraza la Wawakilishi lipo na wanalipwa mishahara na wamechaguliwa na Wananchi wafanye kazi, sasa Wabunge huku msijifanye ninyi mnajua sana kuliko Wawakilishi wenu, kwani ninyi fomu za uwakilishi hamkuziona mbona hamkugombea? Leo mnaleta ufundi hapa tunaiambia dunia, kwani Wawakilishi hawawezi kuiambia dunia ila ninyi? Ninyi ni nani? Aah, huku ni kutaka sifa ambazo hazina sababu yoyote. Wawakilishi wamechaguliwa na Wananchi na mnasema ooh, tunakuona Makamu wa Pili wa Rais; Makamu wa Kwanza wa Rais hamumwoni mbona hamumwelezi?

Msiendeshe siasa za hujuma! Mmemng'ang'ania baba wa watu hapa tunakuona Makamu wa Pili wa Rais na Makamu wa Kwanza mbona hamumwambii mnawambia Makamu wa Pili tu wa Kwanza mnamrukaje? Acheni mambo ya kuingilia Mihimili mingine, mmechagua kuwa Wabunge zungumzieni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, habari ya Uwakilishi Zanzibar waachieni wenyewe wako kule, wala ninyi siyo wenyewe. Mimi nawashangaa mnajitkuza ni wenyewe; ninyi ni wenyewe wa wapi?

Ninyi ni Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania siyo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Zanzibar. Wapo wenyewe waachieni wafanye hiyo kazi. Kwa nini mnaingilia mihimili ambayo siyo ya kwenu sau mmekosa hoja humu? Tunaiambia dunia ijue, dunia ijue kwani wale hawawezi kuiambia dunia ila ninyi? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haya ni mambo ya ajabu sana, hebu tuache kila mtu afanye kazi yake. Nami nasema hata katika ndoa ukiona ndoa ya watu wawili kaingia wa tatu, ujue hiyo ndoa imeingia mdudu. Ndoa yetu na CUF imeingiliwa na CHADEMA, sasa ni tabu; wenzetu hawatuelewi, tuna mkataba, tuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa wameruhusu hawa kuingia basi ni vurugu kila siku.

MBUNGE FULANI: Kumbe kuna ndoa!

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Kumbe hujui kwamba tuna Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar wa kwoo, sasa hao wameingia wametoka wapi, tuliwaambia msiwakubali hao watawavuruga. Mmekuwa hata hamchangii hoja mmeng'ang'ania tu kwamba ooh, sisi tunataka tuisemee Zanzibar iwe huru!

Mheshimiwa Spika, Tume Huru ya Uchaguzi. Hivi tunavyozungumza uhuru kwanza tunazungumzia uhuru upi? Tuwe tunafafanua jambo mojamoja tu tunasema na tunasema uhuru wenyewe uwe huu. Tanzania leo hii tukubaliane hapa bila kusema uongo, unaweza kumpata refarii wa mpira ambaye hapendi Simba au Yanga? Hivi hao ninyi mnaowataka watu huru ni watu gani hao? Watatoka nchi gani ambaa miyo yao itakuwa haina mapenzi na vyama vyetu viliviyotuleta hapa? Hivi kwa nini tunadanganya jamanii? Tunazungumzia habari ya kwamba Tume ile ilitutangaza kwa nguvu, Tume hiyo hiyo ya uchaguzi ndio iliyo tangaza Majimbo yote lakini leo kwa kusema wewe umeshinda unasema ilikuwa kwa kazi ila kwa kusema mwenzako kashinda pale haikuwa kwa kazi.

Mheshimiwa Spika, tutapoteza muda bure, niliwaambia na leo ninawakumbusha tena kwamba, suala la Katiba linapochukua muda mrefu na kutumia pesa nyingi za Watanzania siyo kwamba Watanzania wote wanafurahishwa nalo. Kuna zaidi ya robo tatu ya Watanzania leo hawajanywa chai, kuna watu wana matatizo makubwa, wanalala chini, wanapata shida ya kusomesha watoto wao, matibabu ya mtu kupona anakufa lakini sisi kila siku tunaleta porojo tu, tunafikiri hii Katiba itakuwa mwarubani wa kutibu kila kitu?

Leo hii tuna Katiba inayozungumza haki za binadamu, lakini bado kuna watu wanawaua watu wenyewe ulemavu wa ngozi. Katiba gani hiyo tutakayo iandika ambayo kila kitu kitakuwa ni suluhu?

Ukiwasikiliza wachangiaji wote utagundua *interest* zao ni za kiuchaguzi chaguzi tu, hawazungumzii masilahi ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE]

nchi, hawazungumzii masuala ya mgawanyo wa rasilimali za nchi, bali wanazungumzia habari za nitashindaje kuwa Mbunge kiurahisi; hakuna urahisi kwenye uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, mapambano ya vyama wakati wa uchaguzi ni kitu cha kawaida, lakini nasema katika maswali ambayo yanaandalialiwa, mimi ningeshauri kitu kimoja; tatizo linalokuja hapa wenzetu Wazanzibari hawataki kuwa wawazi; wapo Wagogo wanaoishi Dar es Salaam, wale Wagogo uchaguzi wote wanawachagua Wabunge wao kulekule Dar es Salaam ambao watawaongoza. Kuna tabia iliyojificha uya watu wa Zanzibar ambao wanataka kuvuka kwenda kuwachagulia watu Viongozi halafu warudi tena kuja kukaa huku; tabia gani kwa nini usipige kura kwako ili huyo Kiongozi akutawale wewe?

Wewe unakwenda kumchagua mtu amtawale mwingine halafu unarudi kuja kuuza machungwa Kariakoo, piga kura Kariakoo. Ukiacha hiyo wala hakuna ugomvi, hata Tume ya Taifa ya Uchaguzi hiyo *NEC* ikisimamia wala hakuna ugomvi. Kinacholeta ugomvi hapa ni sifa za mpiga kura wa Zanzibar na sifa za mpiga kura wa *NEC*, ndiyo kinacholeta shida kwamba hawa wanataka wawavushe watu waliopo huku na maboti wakajandikishe kule halafu baadaye warudi kuja kufanya shughuli zao. Hilo linawakera wale walioko kule, kwa nini hamuwi kama Wagogo na Wasukuma wanapiga kura huko na Wakwere walioko kule wanapiga kura huko na Wanyakyusa waliopo Dar es Salaam wanapiga kura Dar es Salaam, ninyi mnachohangaika ni nini mpaka wakati wa uchaguzi mfunge safari? Hii ndiyo inayoleta tabu, tuwe wawazi tu, wala hakuna kitu kingine hapa.

Mpango wa kuvusha watu kutoka huku kwenda kule kuongeza nguvu ndiyo unaosababisha haya, ndiyo maana unaona mtu anasema kwa vyovyote vile tutashinda; mshinde nini? Mnashinda kwa hoja ipi kama siyo ya kuvunja Muungano? Maana hakumaliza Mbunge

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE]

anasema mkija na hii tutashinda na mkija na ile tutashinda; mtashinda kwa hoja gani?

Maalim Seif alisema, hakuna mtu aliyeshinda kwenye uchaguzi uliopita wala aliyeshindwa, iliyoshinda ni Zanzibar. Leo anasimama Mbunge wake anasema tutashinda; mnamshinda yupi? Mnamshinda Maalim Seif maana Yule ndiye Makamu wa Kwanza wa Rais?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tusichanganyane, katika masuala haya, mimi napenda Waheshimiwa Wabunge tujielekeze kwenye kutunga sheria za nchi, hii Katiba ambayo leo tunasema inavunjwa ndiyo tunasema yote iondoke.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Nilisema nitamwita Mheshimiwa David Silinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ili na mimi nichangie Muswada wa Kura ya Maoni wa Mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, ningependa nianze na utangulizi, maana yamekuwa yakisemwa mengi na mengine ni vizuri kuyajibu, japo ulikuwa hutaki kuyazungumza lakini ni vizuri kuyajibu.

Mheshimiwa Spika, jukumu letu kama Wabunge wa Upinzani ni kuhakikisha tunaikosoa Serikali ili ijirekebishe tujenge Taifa. Sasa kama jukumu letu la kuikosoa Serikali linashindwa kueleweka vizuri ndani ya Bunge, Taifa la leo lisinjekuwa hapa lilipo bila Upinzani.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ni lazima lieleweke ni kwamba, maoni yoyote ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni lengo lake ni kujenga ili kuonesha wapi mmesahau mnapaswa kurekebisha, kama ambavyo sisi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DAVID E. SILINDE]

tukichukua nchi ninyi mtakavyokuwa Wapinzani mtafanya hivyo. Ni utaratibu wa dunia nzima. Kwa hiyo, hili lieleweke wazi.

Mheshimiwa Spika, kuna Mbunge mmoja alikuwa anasema Mheshimiwa Tundu Lissu, yale siyo Maoni ya Mheshimiwa Tundu Lissu ni maoni ya Kambi. Mheshimiwa Tundu Lissu analeta maoni ya CHADEMA, siyo maoni ya watu wa Zanzibar wala sehemu nyingine. Jamani, namshukuru kidogo Mheshimiwa Lusinde amesema hapa kwamba, hili Bunge ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hiyo, tuna jukumu la kuzungumza mambo yote yanayohusu Zanzibar na Tanganyika, yote tuna jukumu la kuyasema. Kwa hiyo, hakuna mtu ambaye anaweza kutupangia humu ndani tuiseme ya Zanzibar; ana ubavu gani? Mbona wapo wengine hapa wanajadili mambo ya Bandari ya Dar es Salaam, wanajadili mambo ya Gesi na tunakaa kimya humu ndani kwani yanawahu?

Hatuwezi kufika huko tunakotaka twende, lakini ni lazima tuwekane sawa. Tunasema kwa lengo moja kwa sababu Katiba tunayokwenda kujadili ni ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wala siyo Katiba ya upande mmoja wa Tanganyika ama Zanzibar. Kwa hiyo, hili ni lazima lieleweke.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba, tunapojadili mambo ya msingi hatupaswi kucheka ama kuchekesha watu, tujadili hoja. Sisi ni Wabunge wa kujadili mambo ya msingi. Kwa kweli huwa tunakasirika sana lakini ni busara tu ndiyo inayotufanya tutulie na ndiyo maana tunasema msingi bora unajengwa kwa maandalizi mema. Kwa hiyo, chochote mtakachokileta tutakikosoa, mtakirekebisha kitapita na tutaendelea, ndiyo utaratibu. Tunajua kabisa kuna makosa na kuna mambo mema yanayofanyika katika jamii.

Mheshimiwa Spika, naomba hilo lieleweke. Kwa sababu kuna watu wamenisikitisha sana, wengine wanaitwa akina Nyimbo, Wabena wa kule llembula, lakini

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DAVID E. SILINDE]

wanajadili ya Zanzibar utafikiri wao ni watu wa kule. Tunawafahamu Wabena wa Illembula, lakini leo wanapiga kelele utafikiri wao ni Watanzania kweli kweli! Jamani tujadili mambo ya Utanzania wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo, naomba niende kwenye hoja za msingi. Kwenye Sheria yetu mimi nataka kujadili sehemu ya kwanza, kuhusu haki ya mpiga kura na kupiga kura. Mpaka sasa Sheria yetu inaruhusu mtu anayepaswa kupiga kura ni yule tu aliyekidisha katika Daftari la Kupiga Kura; ndivyo Sheria inavyotaka.

Mheshimiwa Spika, tunataka tujue na mtueleze kwamba Daftari litakalotumika kwenye Kura ya Maoni ni hili liliopo sasa ambalo halijafanyiwa maboresho. Mtueleze kwa sababu haya ndiyo marekebisho ambayo yanatakiwa yaende kufanyika. Mheshimiwa Rais alishatamka kwamba, tunataka Katiba Mpya ipatikane kabla mwaka 2014 Aprili, wakati ule tunaposherekea Sherehe ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar ndicho alichokisema. Sasa mtueleze, kwa sababu Sheria ya Uchaguzi inataka marekebisho kila baada ya miaka miwili na nusu, lakini mpaka leo marekebisho ya Daftari au maboresho ya Daftari la Kupigia Kura hayajafanyika. Sasa kama ni hivyo mtuambie ni lini mtafanya hayo maboresho?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mpaka sasa hivi hakuna dalili ya maboresho ya Daftari la Kupigia Kura; sijui mna hofu ya nini? Boresheni, miaka mitatu iliyopita kuna Watanzania wengi sana sasa hivi wamefikia ule umri wa kupiga kura na miaka ya nyuma watu wengi hawakujidikisha na wengine wamepoteza vitambulisho vyao. Kwa hiyo, waandikisheni ili tuweze kwenda kwenye Kura ya Maoni itakayogusa Watanzania wote, siyo wale waliopita mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ningependa kufahamu; kwenye hii Haki, Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais na hata Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna mahali

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. DAVID E. SILINDE]

wamewahi kutamka kwenye mikutano mbalimbali kwamba, Vitambulisho vya Utaifa vitatumika kwenye kupiga kura ya Uchaguzi Mkuu ujao pamoja na haya mambo mengine yanayoendelea.

Nimejaribu kupitia kwenye Sheria sijaona Vitambulisho vya Utaifa kama vitatumika, sasa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu na Mheshimiwa Waziri watuambie kama vitambulisho vitatumika kwenye kupigia kura ya maoni ya Taifa; na kama havitatumika mtuambie maana sasa vitakuwa na haja gani? Tuelezwe hilo tuweze kufahamu.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine ambalo tunataka kufahamu kwamba taarifa tulizonazo mpaka sasa Serikali imenunua mashine ya kutengeneza vitambulisho vya *electronic* vya *NIDA*. Wametumia karibu dola bilioni 400 kupata hiyo mashine. Sasa Sheria inaruhusu mfumo wa *ki-electronic* kwenye kupigia kura za maoni za Muswada mpya ambao tunakwenda kupidisha? Tuelezwe hayo yote ili tuweze kupata ufanuzi wa mambo yanavyokwenda. Hilo ndio lilikuwa sehemu ya kwanza ambayo sasa tunahitaji ufanuzi iboreshwe ili Taifa liweze kupata Sheria itakayosaidia.

Mheshimiwa Spika, katika Sehemu ya Kwanza vilevile mimi kuna mahali pamenitatiza kidogo kuhusu tafsiri ya kituo cha kupigia kura. Wameeleza mambo mengi, lakini panapotatiza zaidi na ambapo tunahitaji sasa ufanuzi utolewe kwa Taifa zima ni eneo ambalo linasema kwamba, gari litatumika kama kituo cha kupigia kura katika baadhi ya maeneo. Tunataka kupata ufanuzi sababu ni nini?

Mheshimiwa Spika, sababu ni kwamba, moja, hata miundombinu tu ya nchi hii sasa hivi bado kuna maeneo hayafikiki na hayo magari hayawezi kufika.

Pili ni kwamba, matumizi ya magari kwa wakati uliopo hatuwezi kujaribu jambo katika suala nyeti kama hili. Kwa sababu unapoenda kwenye *referendum*, yaani kwenye

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DAVID E. SILINDE]

masuala nyeti tunakuja kutengeneza utaratibu mpya wa kujaribu masuala nyeti jamani, hapo mnakuwa hamjalitendea haki Taifa.

Kwa hiyo, ushauri wangu suala la gari kutumika kama kituo cha kupigia kura liondolewe, isipokuwa kama mnataka kujaribisha kama linafanya kazi, tumieni kwenye Uchaguzi wa Serikali za Vijiji, tumieni kwenye Uchaguzi wa Madiwani na *by-election* zote halafu mtuambie kwamba jamani ule utaratibu unaotumika kweli unafaa ama haukufaa. Kwa hivi sasa utakuwa ni mpya na hii yote ni kwa sababu gani? Lazima tuwe wakweli jamani, matumizi ya magari kwa Tume hii ambayo tunatumia kwa sasa, bado haiwezi kukidhi ile haki ya Watanzania wote. Kwa sababu ni wizi wa hali ya juu wa kura za Wananchi. Hili tunalipinga moja kwa moja, kwa sababu tumekuwa tukiona utaratibu unavyoenda na Watanzania mpaka sasa tumezoea kupiga kura katika maeneo ambayo ni ya kudumu. Tunajua kwamba, tutapigia kura shulenii, tutapigia kura kwenye Kituo cha Afya, tutapigia kura kwenye Ofisi ya Mtendaji wa Kijiji ambako mtu anajua.

Leo kuna maeneo kama Momba hayana mawasiliano, unapeleka gari eneo ambalo halina mawasiliano si kura zinaabiwa huko huko jamani! Magari yakipelekwa manane au sita unawezaje ku-control kule? Mimi nilivyoliona hili kwa macho ya mbele kabisa ni dalili ikifanikiwa kwenye kura za maoni watasema hata kwenye Uchaguzi Mkuu itatumika, tutapiga bao Wabunge wengi wa Upinzani kwa *style* hii.

Mheshimiwa Spika, tuwaambie ukweli jamani kwa *style* hii, haya magari mengi yatachomwa moto katika uchaguzi unaokuja. Mengi yatachomwa moto kwa sababu yatashindwa ku-control, yatakwenda katika maeneo ambayo hayana mawasiliano, hakuna mtu anayejua. Norway wanaweza kuya-afford kwa sababu *network* yao inaeleweka vizuri. Nchi za Sweden kote wanatumia mfumo wa magari kwa sababu inaeleweka. Sasa kama tunaweza kwenda katika mfumo wa magari, kwa nini mnakataa mtu

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. DAVID E. SILINDE]

ambaye labda ni Mnyamwaga wa Dar es Salaam asipige kura ya Momba kwa sababu yeye anapigia watu wa nyumbani kwake kama ambavyo inafanyika kwa watu wa Marekani?

Wamarekani waliopo Tanzania wanaweza kumpigia kura Obama aliyeko Marekani kwa nini wasimpigie kura Jakaya Mrisho Kikwete nchini kwake? Kwa nini wasimpigie Mheshimiwa John Mnyika ama Kawe Mheshimiwa Halima Mdee ama akina Mtemvu wa Temeke; kwa nini wasiwapigie kura pale? Hili naomba vilevile lieleweke na liwekwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili, ambayo napenda kupatiwa uafanuzi nataka ule Muundo wa upatikanaji au usimamizi katika Tume ungepitia Sehemu ya Saba pamoja na Sehemu ya Nane.

Mheshimiwa Spika, ninapendekeza kitu kimoja, kwenye Kanuni ni Maafisa wa Jimbo kwa maana katika ngazi ya Wilaya ambapo usimamizi wake utakwenda kwenye Wakurugenzi ama Wakuu wa Idara. Nini tunachokipendekeza? Tunasema katika hizi ngazi za Wilaya ama ngazi za Mikoa, Maafisa wa Tume waombe, kwa nini mnakataa waombe ambao wanapitia katika Majimbo. Nchini kwetu hapa tuna Majimbo 239, sasa Majimbo 239 tuna uwezo wa kupata hawa watu, wakaomba watu wenyewe vigezo wakachujwa wakasimamia.

Hatuwezi kuwa na Tume huru kwa ngazi ya juu, huku chini kama mfumo ni mbovu haiwezekani. Sheria inasema yatakayosemwa chini na yule Msimamizi Mkuu katika ngazi ya Jimbo ama Mko, ndiyo yatakuwa majibu ya mwisho. Sasa wote hawa wakishaharibu unategemea kule juu kutakuwaje? Lazima muundo tuutengeneze vizuri kuanzia ngazi ya chini.

Mapendekezo yangu ni kwamba, Watumishi wa Umma katika ngazi za Wilaya isipokuwa chini ya usimamizi wa vituo, kwa mfano, walimu wanaweza wakafanya,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DAVID E. SILINDE]

watendaji wa vijiji huko chini wanaweza wakafanya hiyo kazi, lakini ngazi ya Wilaya na ngazi za Mikoa lazima tuondoe. Kwa sababu asilimia kubwa ya viongozi unaweza ukateua Mkuu wa Wilaya ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM au Mkuu wa Mkoa unaweza kumwondoaa ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM, ni *Political Appointee Position*, tunataka watu huru. Tunajua wazi kabisa kwamba, watakuwa na mtazamo, lakini ni watu ambao wataweza kuwajibika kwa Wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, hili ningependa lifanyike. Waombe, wachujwe na wateuliwe watu wenye sifa zinazofaa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nimalizie kwa kusema kwamba, yale mliyokuwa mnayasesema, Zanzibar tunaye Waziri Kivuli ambaye ni Mhesimiwa Raya Ibrahim Khamis na inaeleweka vizuri kwamba tuna Wabunge vilevile wapo upande wa Zanzibar, kwa sababu Zanzibar ni Tanzania. Namwondoaa wasiwasi yule aliyekuwa anasema hatuna Waziri wa Kivuli kutoka Zanzibar, yupo; sawa jamani! Kwa hiyo, aelewe hivyo moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Jaddy, atafuatiwa na Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba, atafuatia Mheshimiwa Christina Mughwai Lissu.

MHE. JADDY SIMAI JADDY: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia Muswada uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu hautakuwa mrefu na wala sitakuwa na mengi sana ya kuongea. Katika Muswada uliopo mbele nitachangia zaidi kwenye Daftari la Wapiga kura, ambalo limegusiwa kwamba nalo litatumika katika kura ya maamuzi ya Katiba Mpya hususan kwa upande wa Zanzibar.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JADDY SIMAI JADDY]

Mheshimiwa Spika, baada ya kusikiliza maelezo mengi ya Wajumbe hasa kutoka Zanzibar kuhusiana na Daftari la Kudumu la Wapiga Kura upande wa Zanzibar, kuna mmoja aliyahifadhi kufika mahali akasema hilo Daftari bora lifutwe kabisa lisiwepo kwa sababu halitaki.

Mheshimiwa Spika, historia ya Daftari la Kupiga kura Zanzibar ilitokana na hamasa ya Vyama vyta Upinzani. Baada ya uchaguzi wa Vyama Vingi wa mwaka 1995 na kuonekana Chama cha Upinzani kimeshindwa, Wapinzani wenye wakasema hatutokwenda tena kwenye uchaguzi bila Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Mwanzo Serikali ilikuwa inaonesha nia ya kukataa hili Daftari, lakini Wapinzani wakasema hatutokwenda kwenye uchaguzi bila hilo Daftari. Serikali ikakubali kuanzisha Daftari. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wakati linaanzishwa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa upande wa Zanzibar, bado Wapinzani wakawa na malalamiko kwamba kura zinaibiwa, wanaingizwa mamluki ndani ya Daftari la Kupiga Kura. Kwa hiyo, ili liboreshwe kifanyike nini? Inaonekana kuwa ndani ya Daftari lile wanaingizwa wasio Wazanzibari. Kwa hiyo, Wapinzani bado wakaja na hoja nyingine tuliboreshe daftari la wapiga kura Zanzibar ili liwe na Wazanzibari watupu kwa maana ya kwamba wakuja wasipate nafasi ya kupiga kura Zanzibar.

Utaratibu gani utumike; ikaanzishwa Sheria ya Vitambulisho vyta Uzanzibari Mkaazi kwa maana ya kwamba, watakaoingia katika Daftari la Kupiga Kura wawe Wazanzibari tu. Hoja hiyo pia iliibuliwa na Wapinzani, ikapitishwa katika Baraza la Wawakilishi, Vitambulisho vyta Uzanzibari Mkaazi vikawa ni sehemu ya kupata haki ya kuandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Zanzibar. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, bado upande wa Vitambulisho vyta Uzanzibari Ukaazi kukawa na matatizo; Wapinzani wakasema bado vitambulisho wanapewa wasio Wazanzibari; ili ipatikane kitambulisho wa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(MHE. JADDY SIMAI JADDY)

Uzanzibari Mkaazi kilicho sahihi kifanyike nini? Ikaboreshwa kwamba, ili upate kitambulisho cha Uzanzibari Mkaazi ni lazima uwe umezaliwa Zanzibar, kwa maana hiyo ikaongezwa dondoo nyingine kwamba ni lazima kipatikane cheti cha kuzaliwa ndiyo upate Kitambulisho cha Uzanzibari Mkaazi. Utakapokipata Kitambulisho cha Uzanzibari Mkaazi ndiyo uweze kuandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Mheshimiwa Spika, haya yote yalianzishwa na Vyama vya Upinzani Zanzibar. Mimi leo ninashangaa kusikia Mpinzani anasema Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lifutwe Zanzibar! (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kinachoendelea sasa hivi Zanzibar ni *Ungujanisation*; watu wanatoka maeneo mbalimbali kuingia Zanzibar. Sasa kuna kitu kinataka kufanyika; ni kwamba, watu wa Vyama vya Upinzani wanaingia Zanzibar kwa madhumuni au kwa mkakati labda pengine kutaka kuhodhi baadhi ya Majimbo ya Zanzibar. Kwa hiyo, wanachokifanya wao, wanatoka sehemu moja wanakuja Zanzibar na kuhamia kwa maana ya kuhodhi maeneo.

Mheshimiwa Spika, kibaya wanachokifanya wanashahau kitu kimoja, Sheria za Zanzibar, yejote ambaye anakaa Zanzibar, Zanzibar imegawanyika katika mtindo wa Shehia. Ukikaa katika Shehia, cha kwanza kabisa wakati unaingia katika hiyo Shehia lazima upeleke taarifa kwa Sheha kwamba nimeingia katika Shehia yako, naomba kibali cha kunitambua kwamba mimi sasa mkaazi katika Shehia yako. Katika utaratibu huu wa *Ungujanisation* sasa, wenzetu wanakuja kutoka sehemu nyingine wanafika Zanzibar, wakifika wanafikia mitaani tu huko hawaripoti kwa Sheha.

Sasa unapofika wakati wa kuandikisha wapiga kura katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na wanapoenda kwa Sheha kutafuta vibali vya ruhusa ya kwenda kuandikisha kuwa wapiga kura, ndipo ambapo wakati

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JADDY SIMAI JADDY]

mwininge wananyima hivyo vibali kwa sababu Sheha hawatambui hawakwenda kuripoti wakati wanaingia katika Shehia hizo. (Makof)

Mheshimiwa Spika, hili ndilo ambalo linagoma kwa upande wa Zanzibar. Wengi wa watu ambao wanakataliwa ni kutokana na kutotimiza masharti ya Sheria ambayo imetungwa na Baraza la Wawakilishi, Baraza ambalo ndani yake kuna Wajumbe walio karibu sawa na Wajumbe wa Chama Tawala, ambao wamekubaliana kwa pamoja kwamba, sasa utaratibu wetu wa kuishi Zanzibar utakuwa ndiyo huu. Wenzetu wanaukiuka utaratibu huo sasa inakuwa ni nongwa. Wewe unaingia Zanzibar halafu unajificha vichochoroni, inafika wakati wa kupiga kura unataka kwenda kuandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, unanyimwa kibali na Sheria unasema Sheha mbaya.

Mheshimiwa Spika, haya yote yanatokea ubaya wa Sheha utakuwa Zanzibar tu, kwa sababu Pemba vilevile kuna Masheha, malalamiko haya hayapo, yapo Zanzibar tu kwa sababu gani? Kwa sababu Zanzibar ni yetu sote, Pemba ni ya kwao wao. (Makof)

Mheshimiwa Spika, hili ndiyo linalogomba Zanzibar. Mheshimiwa Rashid Mohamed Hamad jana alichangia vizuri sana. Alizungumza kwamba, kwa wale ambao hawana sifa kuingia katika Daftari la Wapiga Kura Zanzibar, uwekwe utaratibu waingizwe katika Daftari la Kupiga Kura la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Utaratibu huu ndiyo ambao ultumika katika uchaguzi uliopita wa mwaka 2010. Ultumika utaratibu huu kwa sababu uchaguzi wa mwaka 2010 wakati wa kuboresha Daftari la Wapiga Kura Zanzibar kuna Viongozi wa Vyama vya Upinzani waliwashawishi Wanachama wao wasiende kuandikisha katika Daftari la Wapiga Kura wakagoma wakakosa hiyo haki kwa sababu walifuata amri ya kiongozi wao kwamba, msiende kujandikisha katika Daftari la Wapiga Kura. Wakatayarisha utaratibu wa kupiga kura katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na utaratibu huo mwaka 2010 ultumika.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JADDY SIMAI JADDY]

Ninaungane na Mheshimiwa Hamad Rashid kwa mawazo yake aliyyo yatoa jana kwamba, wale ambao hawataingizwa katika Daftari la Kupiga Kura la Zanzibar kwa maana ya kutotimiza masharti ya kisheria, basi uwekwe huo utaratibu na ambapo bado unaendelea kutumika basi utakuwepo.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono kwa asilimia mia moja suala la kura ya maoni, lakini suala la kusema Daftari la Wapiga Kura Zanzibar lifutwe kwa kuwa halina maana, hili siliungi mkono.

Mheshimiwa Spika, kwa maneno hayo machache, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Christina Mughwai.

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Katika mjadala huu, nina mambo mawili tu ya kuzungumza, lakini kabla sijaanza kusema naomba na nizungumzie mjadala ambao unaonekana kushika kasi kuhusu suala la Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, tangu jana nimefuatilia mjadala na kwa kweli nimeshangaa kuona baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliomo ndani ya Bunge hili, wanakijaribu kutuzuia sisi Wabunge wa Upinzani eti tusizungumzie masuala ya Zanzibar. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Zanzibar kama ilivyo katika Katiba ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa Mheshimiwa Mbunge ndani ya Bunge hili anaposema baadhi ya Wabunge wasizungumze mambo ya Zanzibar eti hawajatutuma, eti hayatuhusu, mimi nashindwa kuelewa iwapo Mheshimiwa Mbunge huyu anajua hata kwa sababu gani yupo ndani ya nyumba hii! (*Makof*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CHRISTINA L. MUGHWAJ]

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni ina Wabunge kutoka Zanzibar, CHADEMA tuna Wabunge kutoka Zanzibar, CUF wana Wabunge kutoka Zanzibar, Kambi ya Upinzani ina wafuasi katika nchi nzima na Zanzibar ikiwemo. Kwa hiyo, naomba niweke wazi na ninaunge mkono maelezo yaliyopo katika Hotuba ya Kambi ya Upinzani kwamba, *so long as* Zanzibar itaendelea kuwa sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sisi tutaendelea kuyasemea mambo ya Zanzibar. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tena nashangaa huyu Mbunge anayetoka Zanzibar anapotuambia sisi Wabunge wa Bara tusizungumzie mambo ya Zanzibar hayatuhusu, anasahau kwamba ye ye anakaa kwenye Bunge la Bajeti la miezi mitatu Dodoma akizungumza mambo ya Bajeti ya Wizara ambazo siyo za Muungano. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mambo yanayohusu wanyamapor kwa mfano, yanazungumzwa katika Bunge hili, madini yanazungumzwa katika Bunge hili na mambo kadha wa kadha, lakini kule Zanzibar sidhani kama kuna mbuga za wanyama, sisi tunanyamaza na kila kitu kinajadiliwa. Tunaelewa kila Mbunge ndani ya Ukumbi huu ana haki ya kuzungumza mambo yote yaliyoko katika eneo la Jamhuri ya Mungano wa Tanzania. Kwa hiyo, Zanzibar sisi tutaisemea, tutawasemea wafuasi wetu wa Zanzibar na hakuna mtu atakayetuzuia ilimradi hatuvunji Sheria. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba sasa nizungumzie mambo mawili katika mjadala uliopo Mezani. Napenda nizungumzie suala la ushiriki wa kura katika makundi maalum na husasan hapa nizungumze kushiriki katika kura kwa Watanzania wanaoishi nje ya Tanzania. Kupiga kura ni haki ya Kikatiba ya kila Mtanzania. Imefika wakati sasa Serikali ya Tanzania, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, iwatendee haki Wananchi waishio nje ya Tanzania ili waweze kutimiza wajibu wao wa Kikatiba kushiriki katika zoezi la uchaguzi. Kumekuwa na hoja zikijengwa hapa

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI]

kwamba, wakati bado haujafika, nchi yetu bado haipo tayari kuwashirikisha Wananchi walioko nje ya nchi, kwamba Watanzania ambao wako nje ya nchi wametapakaa duniani kote, tutawapataje hatujui walipo, bajeti ni ngumu.

Mheshimiwa Spika, hivi ni kweli Serikali haijui idadi ya Watanzania walioko nje ya nchi? Kama ni kweli hawajui namna ya kuwapata hizo Balozi zetu zilizoko katika nchi mbalimbali zinafanya kazi gani? Ajabu kusikia Watanzania wametapakaa duniani kote tutawapataje! Kwa kweli hii haiingii akilini. Tunapozungumzia suala la gharama kwamba ni ghali kuwashirikisha Watanzania. Suala la uchaguzi tena kuandika Katiba mpya, ambalo linakuja mara moja katika maisha ya mwanadamu na hii ni fursa kwa kizazi chetu kilichopo sasa hivi kwamba ni ghali? *Obvious*, ni kwamba hili zoezi ni ghali Serikali inapaswa kujianaa kigharama ili kila Mtanzania aweze kushiriki fursa hii adimu katika maisha yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono kipengele cha kwamba, Watanzania waishio nje ya nchi wafanyiwe utaratibu ili nao waweze kushiriki katika zoezi la kura ya maoni.

Kipengele kingine ni kifungu cha 43 katika Muswada huu, nacho kinahusu mambo ya pingamizi la matokeo ya kura za maoni. Kipengele hiki kinasema kwamba, Kamati ya Kura itaweza ku-*submit* au kupeleka pingamizi Mahakamani ndani ya siku 14. Tena pingamizi hilo litapokelewa ikiwa litakuwa limetimiza pamoja na mambo mengine, limekusanya sahihi siyo chini ya asilimia kumi kutoka Majimbo matano kila upande wa Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, naona hiki ni kipengele kigumu sana kutekeleza; chukulia jiografia ya Tanzania Bara ilivyo, Majimbo mengine ni makubwa sana, ukisema mtu akusanye asilimia ya kumi ya wapiga kura kutoka kwenye Jimbo la watu laki tatu kwa mfano, hapo unahitaji kukusanya sahihi elfu thelathini; ukusanye sahihi elfu thelathini kutoka Majimbo matano ya Tanzania Bara, ukusanye sahihi elfu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CHRISTINA L. MUGHWAJ]

thelathini kutoka Majimbo ya Tanzania Zanzibar kwa wastani, halafu zoezi hilo lifanyike ndani ya siku 14. Hivi katika hali ya kawaida inawezekana kweli ndani ya siku 14?

Mimi naona katika kifungu hicho imeeleza kwamba Mahakama nazo zitafanya utaratibu wa kesi ya hilo pingamizi ndani ya siku saba. Mimi siyo mwanasheria, lakini nafikiri Wanasheria wanaweza kutueleza, kwa taratibu zetu za Mahakama na kesi zinavyoendeshwa kweli Mahakama inaweza ikaendesha kesi ya uchaguzi huu kwa siku saba? Kweli Wanasheria wanaweza kupeleka pingamizi Mahakamani tena kwa kukusanya sahihi za makumi elfu kama nilivyotolea mfano ndani ya siku 14? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naona sharti hili au kifungu hiki kimewekwa ili watu washindwe kupeleka pingamizi la matokeo ya kura ya maoni, hata kama wanaona matokeo hayakuwa sahihi. Serikali inashindwa kusema kwamba haturuhusu pingamizi, sasa wanajifanya wanaruhusu kwa kuweka masharti ambayo hayatekelezeki. Afadhalil watumie muda wa siku ambazo zinatumika katika chaguzi zingine za kawaida na siyo siku 14 za kupeleka pingamizi wala siku saba za kutekelezwa na Mahakama kama ambavyo Muswada unaaelekeza. Vinginevyo, itakuwa ni vigumu kweli, haiwezekani kuanda pingamizi la kupinga matokeo ndani ya siku hizo chache. Kama haiwezekani kuongeza siku, basi ni afadhalil kutoa kabisa kifungu hicho ili ileweke kwamba, kura hizi za maoni pingamizi haziruhusiwi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi nashukuru na nitaunga mkono hoja iwapo mambo yote tuliyoyaeleza yatazingatiwa. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante nashukuru. Sasa nimwite Mheshimiwa Shibuda, atafuatiwa na Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein.

MHE. JOHN S. MAGALLE: Mheshimiwa Spika, nami napenda kushukuru kwa kupata fursa hii niweze kuchangia Muswada wa Sheria ya Kura za Maoni wa Mwaka 2013.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN S. MAGALLE]

Mheshimiwa Spika, naomba kuanza na kauli isemayo kwamba; uongozi ni kukubaliana na matatizo na siyo uwanja wa kupeana maneno ya kusutana na kushutumiana. Haya hayajengi hata kidogo, heri kukosoana kuliko kusengenyana. Napenda sasa kutambulisha ya kwamba, sisi Wabunge wote ni vyema tukatambua tuna deni la kuthamisha Bunge hili na tuna deni la kuthaminisha kila mmoja anaacha urithi wa tabia ipi na desturi zipi za kuja kuigwa na wajukuu zetu watakaokuja na kusoma *Hansard* ya Bunge letu. Tukiendekeza kusherehesha ushabaki wa chuki za masilahi binafsi, hatutakuwa tunajenga masilahi ya nchi hii bali tunaenendekeza mambo ambayo ni pancha kwa masilahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, wakale wamesema mpanda ngazi hushuka, vilevile napenda kusema ya kwamba, mtu haachi asilia yake, mtu haachi hulka na silka yake hadi atakapovishwa hirizi itakayokuwa imekaangwa katika maji ya mafua ya mbuni ambaye ana matege najicho la chongo na jicho la kengeza ambalo ndiyo dawa ya kuondoa ukakamavu wa watu wenyewe migomo ya fikra.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muswada huu, wazee husema hamna chema kisicho na kasoro. Muswada huu una dhamira njema. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu asimamie; ni vyema nguvu za hoja ambazo zinatoka katika upande wa kila Mbunge, ambazo zina ustawi na maendeleo ya Jamii la Taifa letu, zipokelewe dhidi ya ushabiki wa kusema ya kwamba fulani anataka kuonekana anang'ara. Tuache kusutana kwa sababu ya ubora wa hoja na kwa sababu imetoka tu kwa mtu usiyempenda. Napenda kuwahakikishia Taifa hili kwamba, Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, katufundisha somo la subira na anapenda kusikiliza nguvu ya hoja siyo ushabiki wa kusherehesha maswali ya masilahi binafsi.

Mheshimiwa Spika, nikirejea kwenye hoja ya Muswada huu, Kifungu cha 4(1), naomba kushauri ya kwamba, kitamke bayana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuna maneno Rais bila maneno ya Rais wa

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. JOHN S. MAGALLE]

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vivyo hivyo napenda kushauri kwamba, Serikali iondoshe visingizio vya kuzaa fedhuli kwa matokeo ya kura. Hivyo basi, kituo cha kupigia kura kinachoitwa gari ni mfumo unaobia kusigana na kinatengua utulivu wa fikra.

Napenda kushauri ya kwamba, tusing'ang'anie mambo ambayo yanajaa fedhuli na kuzaa kusigana na matibuko ya utulivu wa fikra. Kwa nini tuwe na mambo ya kushindanisha matakwa binafsi na tunasherehesha matakwa binafsi? Kwa nini tuseeme hili ambalo linaibua kusigana na mteguko wa utulivu wa fikra tuliondoshe tu tusonge mbele. Si kila kitu tumpelekee Rais wetu atupe somo la maana ya maono ya kutanguliza hekima palipo na upungufu. Nimeona haya niyaseme kwa msisitizo mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kusisitiza ya kwamba, mtiririko wa maswali ya kifungu cha kupigiwa kura, kuridhia ama kutoridhia, Kifungu cha 4(4) cha mamlaka ya kuitisha kura ya maoni ya maswali yatakayokuwa na madhumuni ya sehemu mbalimbali. Naomba Sheria hii ifafanunue itasomeka upigaji kura utakuwa kwa kila kifungu cha sehemu ya Katiba au mnaandaa dodoso za aina gani za hoja? Ni vyema suala hili likafafanuliwa vizuri na wajibu hoja. Sheria hii inahimiza masilahi kuhusu kura ya maoni, siyo jambo la kugombewa na kitu chochote. Kura ya Maoni haina mshikamano na masuala ya kugombea Viti vya Kisiasa, Viti Maalum, Ubunge, Udiwani na Urais.

Kwa hiyo, yale ambayo ni kasoro za kuondosha umoja na mshikamano, ambayo yanahitaji kutolewa msukumo maalum, ni vyema basi akusanye yaje yaingie kwenye Katiba ijayo. Sheria hii nadhani tutakuwa tunaionea, bali kasoro zinazozaa mizozo kwenye kila upande zitatuliwe na kanuni zitakazotungwa kwa masilahi ya kwamba kila mmoja apige kura. Masuala ya kura za Uchaguzi wa Viti Maalum yaachiwe fursa yake kipindi kitakapofika. Fursa ya kupiga kura ilindwe mpaka kipindi kitakapofika. Fursa ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN S. MAGALLE]

kupiga kura ilindwe kwa masilahi ya umoja na mshikamano na kuondoa kusigana.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwamba wale walio nje ya Tanzania wapewe fursa ya kupiga kura; naomba nishauri kuwa ni wazo jema lakini halina maandilizi. Tutambue kuwa heri uchelewe ufile salama kuliko kuharakisha jambo ukaja kujikwaa ukajikuta umevunjika. Napenda kusema hayo kwa sababu moja kubwa; Taifa letu linahitaji kuwa na lindo la usalama na ulinzi mkubwa. Tutambue Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilipatikana kwa Mapinduzi Matukufu na hivyo hivyo palitokea kusigana na vivyo hivyo bado watu wana mitazamo ya masilahi binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiharakishe tu kwa sababu upande mmoja wa Tanganyika, tunaweza kwenda sambasamba na matakwa hayo. Vilevile sensa hajafanyika, kwa hiyo, naomba tuhakikishe kama tulivyo na hofu ya gari kuwa kituo cha kupigia kura, basi na vituo vya nje ya nchi tuvhofu kwa usalama wa raia wetu.

Rai ya tamko la Kifungu cha 5(3) ambalo linahusu kutolewa elimu ya uraia ya kuhamasisha na kutambulisha ufahamu na uelevu kwa Wananchi. Hicho ni kifungu cha 5(3), bila kuthiri kifungu hicho naomba kupendekeza kwamba, pawe na kifungu (a) cha kutolewa elimu kwa Wananchi na pawe na kifungu 5(3)(b) cha kuhimiza kutolewa elimu ya uraia kwa Wabunge Wateule wa Bunge Teule.

Nasema hayo kwa sababu hivi sasa tupo Wabunge wa mkusanyiko wa marika mbalimbali yenye umbo la ufahamu na uelevu, tulitoka wapi na tumefikaje hapa. Wapo watu ambao hawana uelevu makini na uzanifu kuhusu Mapinduzi Matukufu ya Tanzania na kuhusu madai ya Uhuru wa Tanganyika. Pana watu walisagika, pana watu walipoteza maisha yao, lakini tunataka kuendesha nchi hii kwa mitazamo ya kwamba, kila mmoja ana ukomavu wa ufahamu; la hasha, napenda kupinga kabisa kauli hiyo na mitazamo hiyo.

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. JOHN S. MAGALLE]

Mheshimiwa Spika, huwezi ukawa Sheikh bila kupertia madrasa na huwezi ukawa Askofu bila kupertia madrasa ya kuelimishwa kuhusu Biblia. Wengi wetu ambao sasa tunahitaji kuwa Wabunge wa kuhimiza fikra na mawazo ya kujenga Katiba mpya, wengine hatujui historia ya nchi hii, welevu wetu tunatofautiana. Naomba tukubaliane kwamba, Sheria itamke bayana elimu ya uraia itolewe kwa Wabunge wa Bbunge Teule. Sisi Wabunge Wawakilishi na wale Wateule. Muhimu sana tukatambua kwamba, uzalendo, uaminifu na utiifu kwa masilahi ya nchi, unaundwa, siyo ndoto wala siyo jambo ambalo linatokana na fikra za kufikirika.

Kuhusu Tume kutoa utaratibu wa Mfumo wa ruhusa za vyombo vya kuhamasisha, naomba kushauri ya kwamba, wakati wa kutolewa maoni tulihimiza wadau mbalimbali wa Vyama vya Siasa, Viongozi wa Madhebu mbalimbali na Wadau mbalimbali kwenda kutoa maoni. Leo tunataka kuwabagua! Ninaomba ubaguzi huu tusiuruhusu. Ombwe la watu kutofanya kazi za kisiasa ndani ya umma, nje ya Chama, usijengewe sharti la kisheria.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali isiogope. Natambua ya kwamba, hamasa zitakazotolewa hazitakuwa nje ya wigo wa Kanuni ama Sheria ambazo zinapendekezwa kuwa mawazo ya kupendekezwa kuwa katika Katiba inayotarajwa. Kwa hiyo, kwa nini tuwe na hofu? Naomba kusisitiza ya kwamba, tuondoshe mtazamo wa hisia za hofu kujenga Sheria gandamizi.

Naomba uhuru wa kutolewa maoni ambao upo katika Katiba, Ibara ya 18 na uhuru wa kushirikishwa Vyama vya Kisiasa upewe kipaumbele na hili ni kwa masilahi ya kujenga utulivu wa fikra za waongozwa na Viongozi wa Kisiasa.

Mheshimiwa Spika, nashauri Kanuni zitakazotolewa zijenge uamifu kwa Sheria hii na ziwe ni Dira ya kuhimiza umoja na mshikamano kwa masilahi ya nchi yetu. Napenda kuwaasa wadhamini na washirikishaji wa jamii, waepuke

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN S. MAGALLE]

Kuikaririsha jamii na matakwa binafsi na tuepushe kusherehesha mitazamo ya matakwa binafsi kuwa ndiyo dira ya kujenga Tanzania njema. Naomba hilo kulihimiza.

Mheshimiwa Spika, naomba kushauri madai ya haki, siyo madai ya kuibua kusigana na kupambana. Napenda madai ya haki yawe fursa ya kuelimishwa palipo na umo na upungufu wa ufahamu. Busara na hekima na karama zote za Mwenyezi Mungu, zituongoze tunaposhirikiana katika mambo ya masilahi. Wabunge tuna deni katika Bunge Maalum kuwa nuru ya mtazamo wa kutegemewa na Wabunge watakaokuwa Wateule wa Mheshimiwa Rais. Napenda kusema ya kwamba, tutunze ukweli kwani ni bei rahisi kuliko kutunza uwongo. Gharama za kutunza uwongo na kukaririsha uwongo ni kubwa zaidi kuliko gharama za kutunza ukweli. Chemsha bongo zinazotoka katika upande wa Upinzani, naomba kusisitiza kwamba, ziwe lindo la ubora kwa masilahi ya nchi yetu. (*Makofii*)

Iwapo kanuni zitakuwa na udhuru wa kutumikia, naomba hasa kuhusu kanuni, kama zitatungwa ziwe na udhuru wa kutumikia Sheria hii na kutumikia masilahi ya nchi, tutambue ya kwamba, patakuwa ni mazalia ya mizozo. Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali saidia kuondosha ulemavu wa upofu wa fikra za masilahi binafsi katika kanuni. Kinachonasua chema chenye kasoro siyo mashindano kutafsiri hoja zinazotolewa na mtoa hoja na mjibu hoja. Hekima ndiyo huwa inanusuru palipo na kasoro inayohitaji kutatua kusigana baina ya makundi mawili.

Naomba kusema ya kwamba, tuachane na dhana ya kila mwamba kila mwamba ngoma huvutia kwake. Tukubaliane kila mmoja kutoa na kupokea. Naomba kusisitiza kitakachochomoa Bunge Maalum kutoka ombwe la elimu ya uraia ni kuhakikisha elimu ya uraia inatolewa. Vilevile naomba kusisitiza kwamba, mada za semina hizi zitambulishie tumetoka wapi na tumefika wapi hapa. Mada kwa nini tulikataa ukoloni mamboleo itolewe na mada kuhusu Mapinduzi ya Zanzibar itolewe na mada za kuaminisha Waasisi wa nchi zetu walisagika kwa sababu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN S. MAGALLE]

gani zitolewe. Watu wasifikirie nchi hii ipo tu na inapatikana kutoka kwa Mwenyezi Mungu bila watu kuhangai.

Semina ya Elimu ya Uraia, itakuwa ufunguo wa fikra endelevu kwa Wabunge na itakuwa ujazo palipo na ombwe la sintofahamu. Naomba kusisitiza kwamba, Tanzania njema itajengwa na fikra njema zenye ujazo wa kuelewa uzalendo, uaminifu na utiifu na kuelewa historia ya Tanzania hii. La sivyo, tutajikuta Bunge lile litajaa kusigana kwa sababu ya ombwe la sintofahamu la kukosa elimu ya uraia ambayo tunaikimbiza kwa Wananchi, lakini sisi tuna sintofahamu kubwa sana. Napenda kuasa masikio ya Viongozi yapende kusikiliza ukweli kuliko kukimbilia tamu tamu za uongo mtamu.

Mheshimiwa Spika, dhambi ya kubaguana ni mbaya sana. Humu ndani tumeanza kubaguana kwa makundi kwamba huyu hafai kuzungumza upande fulani, huyu hafai; ya nini hayo? Tutazame hoja ina mustakabali wa kujenga masilahi yetu. Tutafikia hiyo mbegu itaota mtandao wa kufigana na kuanza kuendelea kwa tuisaidiane. Wewe Mpemba, mimi Msukuma na hapo hapo utasema Msukuma wa Pemba, Msukuma wa Unguja, yatatoka wapi hayo au Msukuma wa Bara. Hivi leo mimi Shibuda utanizuia niszungumzie masilahi ya Zanzibar wakati nimelelewa huko kwa sababu tu nipo CHADEMA!

Fikira zetu ziwe na mitazamo ya hekima, tutanguliwe na hekima, tutanguliwe na busara dhidi ya kusherehesha ushabiki wa masilahi binafsi na kusherehesha mapenzi binafsi pale panapohitajika hekima na busara ya kusherehesha masilahi ya Taifa. Mungu Ibaraki Tanzania. Ahsanteni.
(Makofi)

SPIKA: Kwa mara ya kwanza nimesikia Kiswahili cha Kisukuma vizuri. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, atafuatiwa na Mheshimiwa Mahadhi Maalim.
(Kicheko)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kupata fursa ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi kidogo naanza kupata mashaka kwamba, Katiba ambayo tunategemea kuiandika basi itakuwa na matatizo kama tutaendelea na mwendo huu ambao tunaendelea nao hapa.

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kwamba, tunaandika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni Katiba ya Watanzania wote. Sasa hili suala la kuanza kubaguana, suala la kuanza kusemana kwa sababu ya vyama na tunaandika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo mwisho wa siku itakuwa ndiyo kimbilio la watu wote, sidhani kama tutaandika Katiba ambayo itakidhi haja na vigezo vya karne zinazokuja ambazo watakaotumia ni vizazi vyetu. Katiba iliyopo imeandikwa na waliopita ambayo tunaitumia sisi. Wengi wa Wabunge waliomo humu Katiba hii imeandikwa wakati hatujazaliwa. (Makof)

Pamoja na viraka vilivyomo, imetupeleka hapa tulipo na leo tunaisifia Tanzania kwamba ni kisiwa cha amani. Sasa tusipokuwa makini katika suala hili la Katiba na tukawa wawazi katika kueleza na kuvumiliana, fikra ya mtu ambayo anaitoa ni fikra yake, ni mawazo yake. Mheshimiwa Shibuda hapa wakati anazungumza sijui kama mnamfahamu vizuri maneno yake, lakini tamathali zake za semi anazozitoa kila moja inalenga katika kujenga umoja na taswira hasa ya kujenga Utaifa ambao tunautaka. (Makof)

Mheshimiwa Spika, Katiba tunayoiandika ni ya nchi si ya Chama, si Katiba ya Zanzibar, si Katiba ya kikabila, ni Katiba ya nchi ambayo vizazi vyetu vitakuja kurithi, tutawaandikia Katiba ambayo ni ya upande mmoja. Athari zake ni nini? Tuangalie mfano mdogo tu hapa, athari ndogo tu, kwa mujibu wa Katiba hii, Rais wa Zanzibar alikuja kuwa Makamu wa Rais hapa. Kwa mujibu wa Katiba hii,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN]

anaondoka Zanzibar kuja kuwa Makamu wa Rais, yeze ni Waziri kule. Anakuwa Makamu wa Rais hapa anamaliza kipindi anarudi Zanzibar anaambiwa hana haki ya kupiga kura ni mgeni. Hivi tunamkomoa nani? Hivi tunaandika hizi Sheria au tunatunga Sheria kumtungia nani? Tunategemea nani aje atuandikie Katiba nzuri na atutungie Sheria nzuri? Watanzania tuliopo leo tunatakiwa kufanya mambo yetu kwa faida yetu na kwa faida ya vizazi vijavyo, hatukomoani.

Kama waliandika Sheria ile Zanzibar kumkomoa Mpinzani, matokeo yake sasa wamekuja kumkomoa CCM mwenzao. Sitaki kuzungumzia u-CCM na u-CUF na u-nini, lakini hebu tuandikeni vipi ambavyo vitakuwa *productive* kwa watu wetu. Mimi hili naomba niliseme na naomba niwaambie ndugu zangu Watanganyika, mimi nitaita hivyo. Hii Tanzania, tunaiita Tanzania leo inatokana na Tanganyika na Zanzibar. TAN ni Tanganyika, ZAN ni Zanzibar, I na A ikaongezewa ikapatikana neno Tanzania. Sasa leo Mtanganyika ashindwe kujinasibu kwamba mimi ni Mtanganyika, tunapoteza historia na mdharau kwao ni mtumwa. Kwa hiyo, lazima tunapoandika tuandike na tuseme Tanganyika na Zanzibar, ndiyo historia ilivyo tunakataa nini? Panafichwa nini? (*Makofii*)

Nadhani tuwe wazi na sisi sasa ndiyo wa kufanya haya. Hilo la kwanza naomba lizingatiwe vizuri na kila mmoja ajielewe hapa. Mimi nitawashangaa sana Wabunge wa CCM leo na napata mashaka kwa sababu mimi nilikilia huko nikiwa kijana wa *Youth League*; namna gani leo mnapata Wabunge wanakuja hapa hawajui hata wanazungumza nini! (*Makofii*)

Anazungumza Zanzibar, haijui hiyo Zanzibar. Kwamba, ukizungumza Zanzibar unazungumza Pemba na Unguja; hajui. Sasa sijui mnawapate hawa watu? Aah, kufa kwa kile Chuo cha Kivukoni ndiyo kinaleta matatizo haya. (*Kicheko*)

La pili, ambalo nataka kuzungumza, katika kura ambayo inakuja kupigwa ya maoni kuamua hiyo Katiba

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN]

ambayo tunaitaka kwa faida yetu. Nani atapiga hiyo kura; ni Watanzania. Sasa mimi hapa kidogo naomba wenzangu tuangalie kwa umakini wake.

Tanzania leo ni kimbilio la wageni. Nchi zote zilizotuzunguka zikiwa na machafuko, zikiwa na matatizo yoyote, wanakimbilia hapa. Kuna watu wako hapa leo huwezi kusema huyu ni mgeni. Huwezi kujua, hofu yangu, watu wengi watakuja kupiga kura hali ya kuwa siyo Watanzania halisi. Kuna watu wengi wana *Passport* za Tanzania hali ya kuwa siyo Watanzania. Tunayajua haya, kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali katika hili iwe makini sana. (*Makofi*)

Ningependa kabla ya kuingia katika hii kura ya maoni basi tufanye kazi tujue hasa huyu ni Mtanzania na huyu ni Mtanzania kwa kuishi, yaani haya mambo yabaguliwe, vinginevyo watakuja piga kura ambao si Watanzania. Tumeona hivi karibuni tu, katika kutoa ushahidi wa hili mtu anaishi Tanzania anaingia katika Jeshi mpaka anakuwa Kanali, anakimbilia katika nchi ndiyo tunakuja kugundua kwamba siyo raia. (*Makofi*)

Sasa ni mambo ambayo tunatakiwa tuwe waangalifu sana katika hili, kwa sababu tunakokwenda tunataka kujenga. Katiba imetumika kwa zaidi ya miaka 52 hii na tutakayoiandika itatumika kwa zaidi ya miaka hiyo. Kwa hiyo, lazima tuwe waangalifu tujue tunaandika nini kwa faida ya nani. Tukileta uchama hapa, tukileta upande wa labda wa kimikoa au nini, hatutaandika kitu ambacho kitakuwa *productive* na sisi tutakuwa *mas'uli* juu ya hili.

Mheshimiwa Spika, nataka nilisemee suala la Zanzibar, suala la Masheha. Wenzetu hawa walipoinuka hapa kila mmoja anasema Masheha sawa, Masheha sawa, mimi nasema Masheha sawa, lakini si sawasawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Masheha ndiyo chimbuko la matatizo pale. Wao ni watumwa na hawa Viongozi wetu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN]

hawa wanaosimama hapa wakalizungumza hili, wanazungumza tu, lakini *yakuuluna Malaya-filauma*. Wanayoyasema siyo wanayoyafanya. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hili la Masheha mimi nasema kama wenzetu wanabisha, namwomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali yuko pale, Waziri wa Sheria yuko pale, Waziri wa Mambo ya Ndani kama yupo, *IGP*, twende Zanzibar. Kuna Sheria hii ya Uzanzibari Mkaazi, vitambulisho vile tuwakusanyie sisi Wazanzibari ambao hawana zile *ZAN ID* halafu mchukue Sheria, ipo Sheria. Unatakiwa ufungwe kama huna. Sasa twende ili mkaone na mimi nasema hili kwa dini yangu ya Kiislamu; *Wallahi Wabillahi Watallahi*. Endapo hamkuona tatizo mlethe hiyo ripoti hapa mimi nitajiuzulu kuwa Mbunge kama wao wanakataa hili. (*Makofi*)

Mimi nina ushahidi ndani ya Jimbo langu watu hawapewi fomu za kwenda kuchukua hizo vitambulisho na Masheha kwa maagizo ya Wakuu wa Wilaya. Nina huo ushahidi twendeni, nikiwa mwongo mimi nitawajibika hapa. (*Makofi*)

Masheha hawa wanaandikisha watoto walio chini ya umri wa miaka 18. Mimi natoa ushahidi leo hapa, kama ni mwongo niwijibike kwa hili. Kuna vijana katika Kituo cha Mizingani juzi tu wakati wanaboresha Daftari, Zuhura Saleh Makame, Samira Amour Kombo, Adam Mussa Kombo, Said Ali Othman, Mwalimu Said Kombo, Wahida Kassim Makame, Zulfa Bakar Othman, Mwanaache Bakar Othman, ni chini ya umri wa miaka 18, wamepewa *ZAN ID* na wameandikishwa kwenye Daftari. Twendeni, msipoliona hili basi mimi nitawajibika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Kifungu cha 5 au Ibara ya 5 inazungumzia haki ya kila Mtanzania kupiga kura akifikia umri wa miaka 18. Ukiangalia katika televisheni kila siku katika Usia wa Baba Mwalimu, kama si leo ni kesho, anazungumzia haki hii. Viongozi wa leo tunalikalia hili halafu mtu mzima anasimama hapa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN]

anajifanya ye ye muumini, *hamsa swalawati* anasema uongo hapa. Haya hayatupeleka na mimi nasema katika hili *Alaisallahu*. Maana yake, hili basi Mwenyezi Mungu atabainisha. Limebainika kwa Rais wa Zanzibar kuja kuwa Makamu wa Rais anarudi kule anaambiwa mgeni, lakini litabainika katika yajayo. Tuweni wa kweli, hivi tunapofanya haya tunamfanya nani? Tunamkomoa nani? Tuna fikra gani au kwa sababu labda unaona hutarudi kama Mbunge hapa? Aah, hivi nani ataishi milele hapa? Wangapi wamepita hapa, halafu tunakuwa wanafiki mtu anakula kiapo pale anashika Msahafu au Biblia kuheshimu Katiba hii halafu Katiba hii hii anaivunja! (*Makofi*)

Mtanzania akifikisha miaka 18 anatakiwa apige kura. Tena imetajwa hapa, leo unaambiwa kama hujatupa cheti cha kuzaliwa, mzee ana miaka 60, 70 atapata wapi cheti cha kuzaliwa wa enzi hizo? Leo eti hiyo ni sababu ya kwamba wewe hujathibitisha. Sasa twendeni, Waheshimiwa mpo, kwanza, katika kila jambo tukifikia pahali tunakuja katika Mahakama ya Rufaa ambayo ni ya Jamhuri ya Muungano, basi twendeni na hili lifike katika Mahakama ya Rufaa tuone.

Waheshimiwa Wabunge, mimi nasema tunaandika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lazima tuweke uzalendo mbele, lazima tuweke masilahi ya nchi hii mbele na lazima tuangalie tunakokwenda na sisi ndiyo tunawajibika kufanya leo.

Nataka nimwombe sana Makamu wa Pili wa Rais, tunaambiwa hatumsemi Makamu wa Kwanza, tunamsemwa. Mimi nikuombe sana Makamu wa Pili wa Rais na nikuombe kwa sababu ni wajibu wangu kufanya hivyo; wewe ni Mwislamu, mimi ni Mwislamu, tunaambiwa katika Uislamu kama unaweza kuondoa kitu kibaya kwa mkono wako kiondoe. Katika hili mimi siwezi, lakini wewe unaweza. Kama huwezi kuondoa basi sema. (*Makofi*)

Mimi kusema naweza na nasema; Mheshimiwa suala hili la Wazanzibari kutopewa *ZAN ID* si kwamba unamnyima

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN]

haki ya kupiga kura tu, Sheria ile mmetunga ninyi mkiwa pale Wawakilishi, mmeieleza, mtu hawezi hata kusafiri kama huna ZAN ID, tiketi huuziwi. Huwezi kufungua hata akaunti kama huna hicho kitambulisho. Tunamnyima haki ngapi huyo mtu? Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais utakwenda kuwa *mas'ulli* juu ya hili kwa sababu unaweza kuliondoa hili hivi sasa. Ziondoe hizi tofauti zetu. Haya mambo baada ya kufa ukishawekewa ubao tu kuna malaika wawili watakuja kukuuliza Mheshimiwa juu ya haya Mwenyezi Mungu aliyokupa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa unao uwezo wa kuondoa hili, nakuomba sana liondoe, hawa watu waandikishwe hata kwenye hii kura ya maoni tu ambayo inatupeleka kwenye Katiba. Halafu hizo *game* zetu nyingine huko basi acha tuzicheze hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofii*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. ISRAEL Y. NATSE: Mheshimiwa Spika, nami naomba kutoa mchango wangu katika Muswada huu kama ifuatavyo:-

Kwanza, Jina na kuanza kutumika, Ibara ya (1); nafikiri ni vyema Jina la Sheria hii kuitwa Sheria ya Kura ya Maamuzi kuliko kuiita Kura ya Maoni, kwani hapa Watanzania wanafanya maamuzi juu ya Katiba wanayoitaka na si maoni. Pili, haki ya kupiga kura katika kura ya maoni, Ibara 9 (i). Daftari la Wapiga Kura kwa pande zote lirekebishwe maana tangu Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010 hadi leo, kuna vijana wengi sana waliofikisha umri wa kupiga kura na wengine kupoteza kadi zao. Hivyo, ni muhimu sana kwa Madaftari hayo kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kufanyiwa kazi kubwa kuhuishwa.

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. ISRAEL Y. NATSE]

Mheshimiwa Spika, Ibara 9(4), nashauri itazamwe kwa undani zaidi kwani kwa watu wa vijijini siyo rahisi kuwa na vitambulisho vingine zaidi ya kile cha mpiga kura, hivyo kuwanyima haki yao ya kupiga kura. Hili ni muhimu sana kwa upande wa vijijini. Mijini ni afadhali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 35, Kifungu cha (5), nashauri kifungu hiki kiondolewe hakina umuhimu kwani *it is obvious* kama Katiba itakataliwa lakini kuwepo kwake pale inashawishi watu kutokuwa huru.

Mheshimiwa Spika, Ibara 37(2); hili ni wazo zuri kwa Watanzania wote kushiriki katika zoezi hili. Hoja ya msingi hapa ni je, Serikali imejiandaaje kuwahakiki hao Watanzania Waishio duniani kote hasa tukizingatia muda tulionao (*Timeframe*)?

Kupinga matokeo ya kura ya maoni, Ibara ya 43, Kifungu cha (2) na (3), kwa maoni yangu hili si halisia (*not realistic*), kwani ukiangalia muda na madai au masharti yanayotakiwa, inaonesha kuwa hakuna dhamira ya kweli kwamba, unaweza kupinga matokeo ya kura ya maoni. Angalia *costs implications, timeframe, geographical position et cetera*, ni kitu ambacho hakiwezekani.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iangalie muda au kupunguza masharti ya kupinga matokeo ya kura ya maoni.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba, muda haukuwa wa kutosha kuwasilisha Majedwali ya Marekebisho, ni muhimu Serikali katika majumuisho, ikatoa majibu ya kutosha kutohana na michango ya Wabunge ya kuzungumza na ya maandishi. Pia Serikali izingatie kuwa, wengine hatujapewa nakala ya Jedwali la Serikali, hivyo, michango niliyooita na mchango huu, hauhusu Jedwali la Serikali. Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi na Mwanasheria Mkuu, watoe maelezo ya sababu za Serikali kutokuwasilisha Jedwali lake mpaka hivi sasa. Haki

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN J. MNYIKA]

ya kupiga kura ni haki ya msingi ya asili na ya kikatiba ya binadamu na raia.

Katika majumuisho, Serikali itumie fursa hiyo kutoa maelezo ya sababu za Tanzania kutoridhia Mkataba wa Demokrasia, Uchaguzi na Utawala Afrika (*African Charter on Democracy, Elections and Good Governance*). Matokeo yake, Tanzania imekuwa ikinyimwa haki za raia kupiga kura kwa nyakati mbalimbali. Hivyo, Waziri Mkuu aeleze maandalizi yaliyofanyika mpaka sasa ya kifedha na vifaa na pia Katiba iliyopangwa na Tume ya Uchaguzi mpaka hivi sasa na lini hasa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura (DKWK) utaanza?

Mheshimiwa Spika, aidha, suala la Zanzibar litolewe majibu ya kina ikiwemo kueleza namna ambavyo kasoro zilijitokeza kwenye uboreshaji wa daftari uliofanyika katika siku za karibuni. Hivyo, marekebisho yafanyike kwenye vifungu vya 9 (ikiwemo vipengele vya 3 na 4), 34 (hasa kipengele cha 2 na kuongeza kipengele cha 4 ili kuondoa kasoro zote zinazotokana na masharti yenye kukwamisha Wazanzibari kuandikishwa kutokana na masharti ya Sheria ya Ukaazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali izingatie kwamba, kwa mujibu wa masharti mapya yaliyotokana na Mabadiliko ya Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 2010 hasa Ibara ya 132(2) na 133(2); masharti hayo yaktumika kwa kurejea mapendekezo ya Muswada wa Kura ya Maoni au Maamuzi kifungu cha 2 na 4(2), sheria inaweza kukwama itakaposilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi.

Mheshimiwa Spika, Jina na Jina Refu la Muswada kwa Lugha ya Kiswahili lirekebishwe badala ya kuwa Muswada wa Kura ya Maoni uwe Muswada wa Kura ya Maamuzi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 4(2) kifanyiwe marekebisho ili kupunguza mamlaka makubwa aliyopewa Rais juu ya kupanga na kutangaza kipindi cha kampeni ya

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. JOHN J. MNYIKAJ]

kura ya maamuzi na kipindi cha kura ya maamuzi kwa ujumla. Ni muhimu urefu wa kipindi kwa maana ya idadi ya siku za kampeni na kipindi kizima zitajwe kwa mujibu wa sheria. Kazi ya Rais iwe ni ile ya Kifungu cha 4(1) pekee ya kuitaka Tume kuitisha kura ya maoni. Tume iwe na mamlaka ya kupanga tarehe. Aidha, Jedwali la Kwanza, Fomu Na. 1, vipengele vyake vinakinzana na masuala yaliyotajwa kwenye 4(2); hivyo, marekebisho yanahitaji kufanyika.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kifungu cha (4) kifanyiwe marekebisho mengine makubwa ili kuwezesha kuundwa Tume Huru ya Kusimamia Kura ya Maamuzi. Badala ya kuipa jukumu hilo Tume ya Taifa ya Uchaguzi (*NEC*) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (*ZEC*), Serikali na Kamati ya Katiba na Sheria kwa pamoja wangezingatia maoni ya wadau yaliyotolewa mbele ya Kamati. Aidha, kama Serikali haikubaliani na maoni hayo, ingetumia uzoefu uliotajwa kwenye Rasimu ya Katiba mpya katika kuunda Tume Huru ya Kura ya Maamuzi. Iwapo Serikali inataka kushikilia msimamo wa kutumia Tume zilizopo, ingefanya kwanza marekebisho ya Ibara ya 74 ya Katiba ya sasa kwa kuongeza uhuru wa Tume na Ibara ya 98 kwa kuweka mfumo na utaratibu wa kura ya maamuzi Kikatiba.

Muswada huu ukipitishwa kama ulivyo, Bunge litakuwa limetunga Sheria inayokinzana na Ibara ya 98 ya Katiba na pia yenye kutumia Tume isiyohakikisha haki kinyume na makubaliano na Rais ya kujenga kuaminiana na mwafaka wa Kitaifa kwenye mchakato wa mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha (5) kifanyiwe marekebisho kupanua uhuru na wigo wa asasi za kiraia na mashirika yasiyo ya kiserikali kutoa elimu ya uraia na kutekeleza programu za uhamasishaji wa umma. Tume ibaki na mamlaka ya kuizua taasisi au asasi ikikiuka izuiwe na ichukuliwe hatua.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha (7) kifanyiwe marekebisho, ielewewe kwamba, uhuru wa Tume ni pamoja

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN J. MNYIKA]

na kutokutumia Watendaji wa Serikali kama Wakurugenzi wa Halmashauri, ambao wanawajibika kwa mamlaka nyingine na pia wana kazi na majukumu mengine. Walau Tume iwe huru kwa kuajiri wasimamizi wa uchaguzi wa Majimbo na wasaidizi wao nje ya Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango wa awali, ningependa kusisitiza kwamba, kujenga kuaminiana na mwafaka wa kitaifa kwenye Katiba mpya kupitia kuboresha Muswada wa Kura ya Maamuzi (*The Referendum Act*), 2013 ni sehemu ya kulinda masilahi ya Wananchi na usalama wa nchi. Badala ya kufanya propaganda potofu kwamba wanaopinga Muswada ulivyo na kutaka marekebisho wanalenga kuleta wingu na kuharibu amani, ni muhimu maoni yakaheshimiwa na kufanyiwa kazi. Kinyume chake ni kujenga mazingira ya vurugu kwenye uchaguzi wa kura ya maamuzi (*referendum*) kama ilivyokuwa kwenye baadhi ya Majimbo katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010 na kama ilivyotokea Kenya mwaka 2006 na 2007.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha (8) kifanyiwe marekebisho waratibu wateuliwe kwa majina yao na siyo kuleana kwa ofisi zao. Hii ni kwa sababu Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na hasa Mkuu wa Mkoa mwenyewe ni Wateule wa Kisiasa (*Political Appointees*), ambao kuratibu uchaguzi kunafanya mazingira ya uratibu huo kuingiliwa kisiasa au kutokuaminika mlongoni mwa wadau wa uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha (9) kifanyiwe marekebisho kuepusha masharti ya ukaazi kukosesha baadhi ya Wazanzibari fursa ya kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha (10) kifanyiwe marekebisho kuwezesha wadau kuhakiki vituo vyta kupigia kura vilivyotangazwa ikiwemo mipaka yake na maeneo yake. Lengo liwe ni kujenga imani juu ya mchakato kutokana na uwepo wa vituo hewa vyta kupigia kura katika chaguzi mbalimbali zilizopita chini ya Tume ya Uchaguzi ambayo imeelezwa wazi kutokuwa huru na haki.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN J. MNYIKAJ]

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha (11) kirekebishwe kwenye *side notes* iendane na matakwa ya 11(2).

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha (13) kifanyiwe marekebisheso ili kuwezesha kuwa na mfumo na haki ya kukata rufaa kwa Tume iwapo msimamizi wa uchaguzi ngazi ya Jimbo atakataa kusajili Kamati ya Kura ya Maamuzi (*Referendum Committee*) na Kamati husika isiporidhika na uamuzi huo kukata rufaa kwa Tume.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha (15), mamlaka ya kuteua Mawakala yasiwe chini ya Kiongozi mmoja bali Kamati husika ya Kura ya Maoni (*Referendum Committee*). Hivyo, hata mamlaka yaliyotajwa kwenye Kifungu cha 13(3) yanahitaji kufanyiwa marekebisheso na kupunguzwa. Mamlaka ya Kiongozi yawe ni kwenye kuratibu na kufanya mawasiliano ikiwemo ya kuwasilisha majina.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 17(4) kifanyiwe marekebisheso, gharama za kampeni viwango vipangwe na Tume ya Uchaguzi badala ya Waziri ambaye ni mteule wa kisiasa na mwenye masilahi katika uchaguzi. Hii itaiongezea Tume mamlaka ya usimamizi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 26 kifanyiwe marekebisheso kuwezesha Tume ya Uchaguzi kutoa sampuli (*sample*) ya swalii na karatasi ya kura, kwa mwelekeo wa swalii; ni suala muhimu katika haki na uhuru wa mchakato wa kura ya maamuzi (*Referendum Act*).

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono Muswada huu upite ili kuruhusu taratibu zingine zifuate. Naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu ambao ni muhimu sana na sisi ni lazima tutambue fursa hii tuliyopewa na Wananchi. Ni vizuri tukakubaliana kwenye masuala ya msingi na si yale ya ushabiki wa kichama, maeneo tunayotoka, kabila au dini.

Mheshimiwa Spika, naomba tupitishe Muswada huu haraka ili wahusika waende kutoa elimu kama Ibara ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. RICHARD M. NDASSA]

5(c) inavyosema. Vilevile Ibara hiyo ya 5 baada ya kuwa *gazette*, zile (a), (b), (c), ziwe kama ifuatavyo; (c) iwe ndio (a), (a) iwe (b) na (b) iwe (c) ili kupata mtiririko mzuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Muswada huu.

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa ya kuchangia Muswada tajwa hapo juu kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia Kifungu cha 43(2), kinachozungumzia kупinga matokeo ya kura ya maoni. Kifungu hiki kinaitaka Kamati ya Kura ya Maoni kuwasilisha ombi la kutaka kупinga matokeo ya kura ya maoni baada ya kupata si chini ya asilimia kumi ya saini za idadi yote ya wapiga kura waliosajiliwa kutoka katika Majimbo matano ya kila upande wa Muungano.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kifungu hicho, Kifungu cha 43(3) cha Muswada kinasema kuwa, pingamizi hilo la matokeo ya kura za maoni liwasilishwe katika Masjala ya Mahakama Kuu ndani ya siku 14 baada ya kutangazwa kwa matokeo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuangalia jiografia ya nchi yetu, ni vigumu sana kupata asilimia kumi ya wapiga kura kuweka saini katika pingamizi siku 14! Hapa ni lazima tuamini kuwa, kwa kuminya muda wa kuwasilisha pingamizi ni wazi kuwa waleta pingamizi wengi watashindwa kukamilisha utaratibu na hivyo matokeo mabovu yatapita bila kupingwa na kulilettea Taifa Katiba isiyofaa kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. ABDULLA JUMA SAADALLA: Mheshimiwa Spika, kwanza, nashukuru kwa kuletwaa Muswada huu. Muswada ambao katika uhalsia wake umeshirikisha pande zote za Muungano na hakuna hata Mbunge mmoja aliyelalamikia hilo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. ABDULLA JUMA SAADALLA]

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii, kumetokea maelezo fulani fulani juu ya mchakato huu Zanzibar. Kwanza, imezungumziwa juu ya Mwanachuoni aliyezungumzia machafuko ya utambuzi wa wapiga kura kule Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mtu anaweza kufanya utafiti lakini uhalisia wa utafiti mara zote uko wazi kutolewa makosa au kukubaliwa kama ilivyoelezewa humu Bungeni. Mhusika alitumia neno Zanzibar kwa maana ya Unguja na Pemba na kama ni hivyo uhalisia wake uko wapi hasa kwa kutilia maanani mgawanyiko wa viti kivyama baina ya Pemba na Unguja? Ndio tuseme Masheha walikuwa *fare*, walitenda haki Pemba na kudhulumu Zanzibar?

Mheshimiwa Spika, hatuwatendei haki hawa wazee wetu na kazi nzuri wanayoifanya, naamini wanatuona na wanapembua nani mchawi wao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa matatizo yanayolalamikiwa ni ya wote CCM na CUF kwa upande wa Zanzibar, ina maana Viongozi hawa wanafanya kazi vizuri sana. Wanakuwa wahanga wa lawama tu kwa kazi nzuri wanayofanya kisheria, kikatiba na kitaratibu zao za kazi kama zinavyowalazimu.

- (1) Muda wa ukaazi *3 years*.
- (2) Cheti cha kuzaliwa.
- (3) Umri wa miaka 18.

Mheshimiwa Spika, Zanzibar sasa tuna Serikali Shirikishi nayo imepatikana baada ya kura ya maoni. Katika upigaji wa kura za maoni; Masheha ndiyo hawa hawa, utaratibu ndiyo huu huu, Uwakala wa ZEC ndiyo uleule na watu ndiyo walewale wataongezeka au kupungua kidogo tu. Iweje matokeo yale yalikubalika kwa kishindo hivi sasa hawa wawe wabaya?

Sote tulikubali kuwa zaidi ya asilimia 60 walikubali Serikali Shirikishi. Juu ya yote haya, Zanzibar tuna Serikali

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. ABDULLA JUMA SAADALLA]

Shirikishi ndiyo iliyochagua Masheha na ndiyo inayoongoza Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa mawazo yangu, *ZEC* sheria na kanuni zake na *NEC* sheria na kanuni zake, zitumike katika mchakato wa maoni ya kupitisha katiba hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchaguzi mmoja kuwa na sheria mbili; suala hili halina uhalsia na ni muflisi kwani sisi humu ndani tuko kwa sheria hizo hizo mbili na tunafanya kazi nzuri sana. Sina shaka na kuwa na Tume moja lakini kwa kuwa masuala haya siyo ya Kimungano, kuna ubaya gani kuwa na utamaduni wa kuwa na Tume mbili ikiwa tunaona haki inatendeka? Sheria inatungwa kulingana na mahitaji ya jamii.

Mheshimiwa Spika, Watanzania walioko nje; nahisi kulihusisha jambo hili ni mapema sana, kama ilivyokuwa kituo cha gari kuwa kigumu kuanzisha, basi mahitaji muhimu ya kuweza kushirikisha ndugu zetu wa nje yanahitaji kutayarishwa; miundombinu ya mtandao, *mobilization*, utayari wa Balozi zetu na kadhalika. Nadhani matayarisho yafanywe au mchakato usitishwe.

Mheshimiwa Spika, asasi za kiraia zinamwakilisha nani? Maoni yangu; Vyama vya Siasa navyo viwemo katika mchakato wa kutoa elimu juu ya upigaji kura ya maoni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. WARIDE BAKARI JABU: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Zanzibar ya Daftari la Wapiga Kura inasema huwezi kupiga kura Zanzibar kama hujawa mkaazi katika eneo husika kwa muda wa miaka mitatu au miezi 36, ndiyo maana Rais wa Zanzibar hakupiga kura Zanzibar kwani pia wapo Wabunge wengi hawakupiga kura hiyo, hivyo daftari ni sahihi kabisa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. WARIDE BAKARI JABU]

Mheshimiwa Spika, Bunge halina mamlaka ya kuingilia mamlaka halali ya kujadili sheria iliyotungwa na Mhimili mwininge; hivyo, wanaopinga Daftari la Wapiga Kura Zanzibar siyo sahihi. Nashauri hoja hii ijadiliwe Zanzibar Baraza la Wawakilishi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Muswada huu ni halali, naunga mkono usimamizi wa kura za maoni kusimamiwa na ZEC na NEC, si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kutoa mchango wangu juu ya Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni wa Mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, ninatumia nafasi ya awali kabisa kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Tanzania, kwa uamuzi wake wa kuleta Muswada huu ili tuweze kuujadili kwa lengo la kuendelea kuwahabarisha Watanzania na kupunguza shughuli kubwa itakayofanywa na Bunge Maalum la Katiba. Mungu ambariki sana na aendelee kumpa hekima daima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu muda wa kukusanya maoni ya Katiba; napenda kukiri kuwa muda uliotumika kukusanya maoni unatosha kabisa kwani Tume iliweza kufika maeneo yote yaliyoandaliwa Tume hiyo kufika. Hata hivyo, Katiba ambayo tunayo sasa, tumekaa nayo kwa muda wa miaka 50. Hivyo ni wazi Watanzania wanajua ni sheria zippi ambazo hazikuwatendea haki na tayari wanafahamu wangependa sheria hizo ziandikwe vipi ili ziweze kuwa na tija kwa Watanzania. Ninaipongeza Serikali iendelee na utaratibu wake.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuandaa mfumo mzuri wa kuunda Kamati za Kupiga Kura za Maoni kwa kuzingatia makundi yote; mfano wanaume, wanawake, vijana, wanaoishi na ulemavu na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DIANA M. CHILOLO]

kadhalika. Hivyo, sioni hofu yoyote katika uwakilishi huu kwani kila kikundi kina uwakilishi ndani ya Kamati hizi. Ninaomba Watanzania wasipate hofu na zoezi la kura za maoni. Ninaipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuonesha mshangao wangu kwa Wapinzani kuendelea kupiga kampeni ya Serikali tatu ambazo zitafanya Marais kuwa watatu, Makamu wa Marais watatu, jambo ambalo litatupa gharama kubwa bila ulazima wowote, badala ya kuelimisha Watanzania kuangalia sheria zinazowagandamiza, haki ya elimu, haki ya matibabu na kadhalika. Ninaendelea kuamini kuwa, Upinzani kumbe ni kipinga kila kitu hata kama ni mambo mema na yana masilahi kwa jamii kubwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumalizia kwa kuunga mkono hoja hii na ninawapongeza sana Mheshimiwa Chikawe - Waziri wa Sheria na Katiba, Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki - Naibu Waziri wa Sheria na Katiba na Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema - Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ni ukweli usiopingika kuwa, mchango wao ni mkubwa sana katika zoezi la kutengeneza Katiba mpya.

Nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowapongeza Mheshimiwa Mizengo Peter Kayanza Pinda - Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri mwenye dhamana ya Muswada huu. Mungu awabariki sana kwa juhudhi na busara zao.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kupata muda wa kuchangia hoja ya kupata Katiba bora, ambayo itakuwa kwa ajili ya manufaa ya Watanzania wote bila ya kujali itikadi ya vyama vyaya siasa.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, hatua iliyofikiwa mpaka sasa ni baada ya busara kubwa kutumika na kwa kuzingatia hoja mbalimbali hasa zile za wachache au

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA]

Upinzani, ambazo kimsingi zilizingatia masilahi mapana ya uwakilishi wa maoni ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, suala la uboreshwaji wa Daftari hili la Wapiga Kura ni muhimu sana katika kila chaguzi. Kumekuwepo na matatizo mengi sana hususani wakati wa kupiga kura. Yanakuwepo matukio ya wapiga kura kufika kwenye kituo na kufikwa na machungu ya kukuta majina hayapo kwenye daftari au kwenye vituo husika kukuta yamebadilishwa. Hivyo, ni muhimu sana Daftari hilo kuboreshwa upya na kazi hii ipewe muda wa kutosha ili Wananchi wote wapate haki yao ya msingi ya kupiga kura kuitafuta Katiba waipendayo ndani ya nchi yao.

Masharti na vikwazo vipunguzwe na hili litapata ufanisi mara pale zoezi la kuandikisha Vitambulisho vya Kitifa vitakapokuwa vimetolewa kwa Wananchi wote. Suala hili ni muhimu sana kwa masilahi ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu vituo vya kupigia kura; ni muhimu vikafahamika mapema na taratibu nzuri zikafuatwa. Kumekuwepo na ukiukwaji mkubwa wa sheria hasa vituo vya kupigia kura kuwa mafichoni na muda mwagine kuwa na vituo hewa. Leo hii vituo ambavyo vimependekezwa ni pamoja na majengo au taasisi za Serikali, maeneo ya watu binafsi yaliyoridhiwa, lakini changamoto ikawa ni vituo vya magari, utata unaojitokeza ni kuwa je, gari hili litakuwa sehemu moja tu au litakuwa linazunguka kila kona? Hapo awali au katika chaguzi zilizowahi kufanyika udanganyifu wa vituo hewa umekuwepo? Sasa kama haya magari yatafanya kazi hiyo, hofu ni kubwa sana kuwa kutakuwepo udanganyifu mkubwa, lakini ikumbukwe kura hii ni kwa ajili ya kupata Katiba nzuri kwa ajili ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kuhusu Tume huru ya Uchaguzi. Katika chaguzi zilizokwishafanyika, kumekuwa na uingiliwaji mkubwa wa Tume hiyo na kuifanya kutokuwa huru. Katika suala hili, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inapaswa kuwa huru na kufanya kazi yake kwa uhuru zaidi. Aidha, katika

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA]

suala hili Serikali inapaswa kuweka mazingira huru ya Tume hii. Tume hii pamoja na kuratibu shughuli hizi Tanzania Bara na Visiwani, inaonekana kuwa Tume ya Uchaguzi ya Bara inapaswa kufanya kazi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na hii iwe kwa kutumia Sheria moja tu. Tume hizi zisipokuwa huru na bado kukawa na sheria zinazopingana, hakika hakutakuwa na matokeo mazuri. Ikumbukwe kuwa, ufanisi mzuri wa Tume hii ndiyo matarajio ya kupata Katiba bora kwa manufaa ya Watanzania wote.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Muswada huu unapendekeza kuwa Tume ya Uchaguzi Tanzania Bara na Tume ya Uchaguzi Zanzibar ndizo zitasimamia zoezi zima la upigaji wa kura hii muhimu ya maoni; napendekeza kuwa, Tume hizi ziwe huru kama ambavyo Ibara ya 74(7) ya Katiba inavyosema.

Vilevile kwa kuwa Ibara hii ya Katiba imekataza Tume hizi kufuata amri au maagizo ya mtu yejete au Idara yoyote ya Serikali au maoni ya Chama chochote cha siasa. Hivyo basi, kwa ushahidi na uzoefu ambaao tunao kuhusu Tume hizi za Uchaguzi kutokuwa huru na kwa namna moja au nyininge kuegemea upande mmoja wa Chama Tawala hasa pale matokeo ya uchaguzi yanapokuwa yameonesha Wapinzani wameshinda, ni vyema vyombo hivi vikawa huru na vijumuushe Wananchi wa Vyama vyote na Rais asiteue Mwenyekiti wa Tume ili kuipa Tume uhuru zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja iliyotolewa na Kamati ya Katiba na Sheria kwamba, Daftari la Kudumu la Kupigia Kura liboreshwe ili kutoa nafasi kwa wale ambaao wamefikisha umri wa kupiga kura wapate haki hiyo na pia wale ambaao wamepoteza vitambulisho vyao wapate haki ya kupiga kura. Kwa kuwa daftari hili litatumika kupiga kura hii ya maoni, ni vyema Serikali ikafanya haraka na kutoa muda mrefu zaidi wa Wananchi kujianzikisha katika Daftari hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. JUMA SURURU JUMA: Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, pili, naunga mkono Tume za Uchaguzi za NEC na ZEC ziendelee na utaratibu wa kusimamia Madaftari ya Wapiga Kura kama ilivyoelekezwa na sheria hii.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuarifu kwamba, malalamiko yaliyotolewa na Wajumbe kutoka CUF kwamba, Masheha wanapendelea upande mmoja wa chama, napenda kusema kwamba maelezo hayo si ya ukweli, kwani Masheha hao hao ndiyo waliofanikisha kutoka sehemu zote za sheria kuisimamisha Serikali Shirikishi ya G.N.U. Pia Masheha hao hao ndiyo waliofanikisha kusaidia uboreshaji wa Daftari la Wapiga kura. Si hivyo tu, Masheha hao hao ndiyo waliosaidia Chama cha CUF kuandikisha watu wengi wa Kisiwa cha Pemba kupata ushindi mwingu wa Majimbo yote Pemba na kuwanyima wafuasi wa CCM kwa Pemba kutojiandikisha katika Daftari la Wapiga Kura; hivyo, Masheha hawana lawama hizo kwani wanatekeleza sheria.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika Muswada uliopo mbele yetu. Naomba nianze kwa kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

Jana ultoa wito hapa kwa Wanasheria kutumia taaluma yao katika kusaidia mchakato na siyo kupotosha, nami nikiwa mwanafunzi wa Sheria, naomba nitoe mawili, matatu, katika kuchangia. Kuna suala ambalo limezungumzwa na watu kadhaa juu ya uhalali wa Sheria ambayo tunaitunga na ikaoneshwa kwamba, kwa kuwa hakuna kifungu cha Katiba kinachotambua au kutupa mamlaka ya kutunga Sheria hii, basi linalotakiwa kwanza ni kufanya mabadiliko ya Katiba yenyewe. Kikachambuliwa pia Kifungu cha 21 hasa katika maelezo ya Msemaji wa

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFAJ

Kambi ya Upinzani halafu wakaonesha kwamba Kifungu hicho bado hakitoi mamlaka hayo.

Jana yalitolewa maelezo na mwenzangu Mheshimiwa Simbachawene na kila nikisoma sioni kwa namna gani unaweza ukakiondoa Kifungu hicho katika hili ambalo tunalifanya. Naomba na mimi pia ninukuu, Kifungu cha 21(2) kinasema: "Kila raia anayo haki na uhuru wa kushiriki kwa ukamilifu katika kufikia uamuzi juu ya mambo yanayomhusu yeye, maisha yake au yanayolihusu Taifa."

Kifungu cha 21(1) kinatoa pia haki ya mtu kushiriki moja kwa moja au kupitia kwa wawakilishi juu ya masuala yanayomhusu au ya Taifa. Sasa kwangu mimi haihitaji kuwa mtaalam wa sheria kujua hicho kinafaa moja kwa moja katika suala ambalo tunalifanya. Katika kudhihirisha kwamba Kifungu cha 21 hakitoshi, ukatolewa mfano wa Katiba ya Zanzibar kwamba, laiti Katiba ya Zanzibar ingelikuwa inatosha, kwa sababu kifungu kama hicho cha 21 kipo, basi kusingekuwa na kifungu katika Katiba ya Zanzibar juu ya suala la kura ya maoni.

Napata shida kidogo kujua kama hii ni kutofahamu kifungu ambacho kinatumika Zanzibar au ni upotoshaji wa makusudi! Nasema hivi kwa sababu Zanzibar kifungu ambacho kimetumika hapa cha 80(a) kilikuja baada ya mchakato wenyewe wa kura ya maoni kuwa umeshafanyika. Kifungu hiki kimeingizwa katika Mabadiliko ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar. Mabadiliko haya ilikuwa ni kutekeleza maamuzi ambayo yamefikiwa na Wananchi katika kura ya maoni. Sasa huwezi ukakitumia kifungu kile kuonesha kwamba lazima kiwepo kwanza kwenye Katiba ndiyo uweze kuwa na Sheria ya Kura ya Maoni.

Sheria ya Kura ya Maoni ilikuwepo kwanza, Wananchi wakapiga kura ya maoni halafu katika mabadiliko ya Katiba ndiyo kikaingizwa Kifungu cha 80(a). Pia kwa mtu yejote ambaye anafahamu Sheria, Kifungu cha 80(a) hakitoi haki ya mamlaka ya kupiga kura ya maoni. Chenyewe kinaeleza katika mazingira gani kura ya maoni

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA]
inaweza kutumika katika kubadilisha Katiba tu. Kwa hiyo, ni dhahiri Kifungu cha 21 kinajitosheleza wala huhitaji kuwa na kifungu maalum katika Katiba kuweza kuwa na Sheria ya Kura ya Maoni.

Vilevile ilioneshwa kuwa kuna wasiwasi wa kuipa Tume ya Uchaguzi jukumu la kusimamia kura ya maoni. Kifungu kilichotumika ni cha 74 tena cha Katiba. Yupo Mbunge mmoja alisoma vifungu vyote akaacha Kifungu cha 74(6)(e) kwa sababu 74(6) ndiyo kinatoa majukumu ya Tume ya Uchaguzi. Yametajwa (a), (b), (c) na (d), lakini mwisho ikaelezwa (e) kutekeleza majukumu mengine yoyote kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge. Alipofika hapa akaacha.

Msemaji wa Kambi ya Upinzani yeye akakinukuu hiki, lakini akatumia msingi mmoja wa kutafsiri Sheria akasema kwamba, kutekeleza majukumu mengine yote kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge, lazima kioane na yale majukumu mengine ya msingi ambayo ni kusimamia na kuratibu uandikishwaji wapiga kura na kusimamia zoezi la uchaguzi. Akasema suala la kura ya maoni halioani. Ni msingi sahihi wa kutafsiri Sheria kwamba, kama chombo au Taasisi imepewa jukumu maalum na Sheria, ni lazima pale unapoambwiwa jukumu lingine lolote litakalotungwa na Sheria ya Bunge lazima lioane na majukumu hayo ya msingi.

Kwa hiyo, ingeshangaza na kweli ingekuwa ni uvunjaji wa Katiba kama tungenesema leo tunaipa Tume ya Uchaguzi hapa jukumu la kuratibu shughuli za Vyuo Vikuu. Unaposema unalipa jukumu la kusimamia kura ya maoni, jina lenyewe linajitosheleza ni kura na kura ni katika majukumu ambayo Tume ya Uchaguzi inapewa. Kura ya Maoni pia ni uchaguzi, mtu anchagua ndiyo au hapana. Kwa hiyo, hoja ni zile zile, watu wanasema tusingize siasa, lakini unashindwa kuelewa kama kweli hoja hizo ni za kisheria. (*Makofii*)

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA]

Mheshimiwa Spika, pili, kulikuwa na suala ambalo limechangiwa na watu wengi kidogo, suala la haki ya Watanzania walioko nje kupiga kura, wengine wakionyesha kwamba hii kidogo ni maendeleo mazuri, na kwamba sasa Watanzania hao nao watapata fursa hii ambayo wamekuwa wakiikosa muda mrefu, na wengine wakionyesha wasiwasi wao, kwamba labda suala hili kwa wakati huu ni vigumu kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, nilichotaka kutanabahisha ni kwamba kwa ilivyo hivi sasa haki hiyo siyo kwamba ni *automatic*. Ni kwamba Sheria tunayoitunga mpaka sasa inasema kwamba: "Tume inaweza kuweka masharti maalum kwa ajili ya upigaji Kura ya Maoni kwa Raia wa Tanzania ambaao wanaishi nje ya Jamhuri ya Muungano." Kwa maana hiyo, ili Watanzania waweze kutumia haki hiyo, kwanza Tume iweke masharti maalum. Kwa sababu Tume inaweza, maana yake pia Tume inaweza isiweke. Kama haikuweka ina maana Watanzania hao hawataweza kupiga kura.

Kinachochanganya kidogo labda ni kifungu cha 37(2), kinachosema kwamba: "Tume kwa Madhumuni ya Kura ya Maoni itaweka utaratibu wa kuandikisha raia wa Jamhuri ya Muungano ambaao wanaishi nje ya Jamhuri ya Muungano."

Sasa hiki kwa mtu ambaye sio mtaalam wa sheria kama mimi, anaweza akafikiri kwamba kinalazimisha Tume, kwamba ni lazima watu hawa waandikishwe. Lakini maana ya kifungu hiki ni kwamba iwapo Tume itaweka hayo masharti maalum kwa ajili ya Watanzania wanaishi nje ya nchi, ndio hapo sasa italazimika katika kifungu cha (2), kwamba lazima waweke utaratibu wa kuandikisha. Lakini kama Tume ikiamua kwamba haijaweka masharti yoyote, au haijatoa hiyo haki sasa kwa ajili ya upigaji kura kwa Watanzania wanaishi nje, basi hiki kifungu cha (2) hakitafanya kazi. Ina maana hakutakuwa na haja ya kuwaandikisha.

Mheshimiwia Spika, wasiwasi wangu ni kwamba inawezekana kifungu hiki kilikuwepo kwa kuzingatia ile hali

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA]
ya mwanzo ambapo tulikuwa tunatunga sheria kwa ajili ya kudumu. Kwa hiyo, inawezekana tulizingatia hivyo. Lakini kwa sasa inawezekana hali bado, lakini huko mbele hili likiwa tayari, tuwe tayari tunayo sheria hii.

Kwa hiyo, kwa vile sasa hivi sheria hii imekuwa ni maalum kwa ajili ya upigaji kura ya maoni. Basi tuzingatie kwamba katika hali halisi ya sasa, kama hatuko tayari basi, huna haja ya kuwa na kifungu hiki. Lakini kama tunahisi hali inaweza kuruhusu, basi inawezekana ukawa na kifungu hiki. Isije kuwa Kifungu hiki kinaendelea kwa sababu ni mabaki tu ya wakati ule wakati ule tunafikiria kwamba sheria hii itakuwa ni ya kudumu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo naomba nichangie kidogo ni suala ambalo limechangiwa na watu wengi sana. Hili ni suala la utumikaji wa Daftari la ZEC. Katika hali ambayo nayo nahisi ni upotoshwaji wa makusudi, inatumika kama ni hoja ambayo itawanyima Wazanzibari haki yao ya kupiga Kura ya Maoni.

Ninasema ni upotoshwaji wa makusudi kwa sababu yameelezwu mengi kuhusiana na suala la ukaazi na sheria hiyo ya Mzanzibari mkaazi ya Zanzibar, lakini ukitazama kifungu cha 34(2), hilo tayari imeishalitatu. Suala liliopo hapa ni kwamba au kifungu cha 34(2), kinasema kwamba: "kwa madhumuni ya kifungu cha 1(b), kura zitakazohesabiwa kwa Tanzania Zanzibar zitajumuisha kura za watu walioandikishwa katika Daftari la Wapiga Kura la Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, na kura za watu wanaoishi Zanzibar na waliondikishwa chini ya Daftari la Kura la Tume ya Taifa ya Uchaguzi."

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo sheria hii imeweka wazi kwamba kama hujatosheleza suala ukaazi, kwa mujibu wa Daftari la ZEC, utaingia katika kura la Daftari la NEC ambalo kila mtu anaandikishwa, haulizwi ukaazi, wala suala la ID. Kwa sababu katika utaratibu wa kawaida *constituency* yake ni Tanzania nzima. Kwa hiyo, wote ambao hawatakithi matakwa ya ukaazi, wataingia kwenye Daftari

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA]
hili la kudumu la NEC, na kwa hiyo, huwezi ukasema kwamba
watu hao watanyimwa fursa.

Mheshimiwa Spika, sasa nguvu nyingi zimetumika
kuelezea matatizo ya Masheha na Sheria ya Ukaazi. Nafikiri
tunalileta mahali sipo, na hili limeelezwa. Sheria hiyo ni ya
Baraza la Wawakilishi. Bunge hili haliwezi kuibadilisha. Sasa
kama tunazungumzia Sheria, nafikiri kama tunapiga siasa
kama vile wengine wanavyosema tusipige siasa, tuzungumzie
sheria; ni dhahiri kwamba hapa kinachotanyika ni siasa na
siyo kuzungumzia sheria iliyopo mbele yetu. (*Makof*)

Kwa kifupi sana, nizungumze kidogo kwamba
kulikuwa kumetumika hoja ambazo ni za andiko langu, na
Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Sikusimama hapa kuunga
mkono kwamba yale aliyojasema ni sahihi au siyo sahihi kwa
sababu ni andiko la zamani. Nakumbuka *title*, sikumbuki
yaliyomo. Kwa hiyo, siwezi nikasema ni sawa au siyo sawa.
Ila napata wasiwasi kidogo, kwa sababu ukitazama hata
alivyoandika, taratibu za kiuandishi zinataka utofautishe yale
maneno ya mtu unayemnukuu na maneno yako.

Mheshimiwa Spika, ukitizama katika hotuba hii, kuna
wakti yanachanganywa yangu na ya Msemaji wa Kambi
ya Upinzani. Kwa hiyo, bila kutofautisha kwamba haya ni ya
andiko ambalo linanukuliwa na haya ni ya Msemaji wa Kambi
ya Upinzani.

Pia kwa jinsi ya ufundi uliotumika kutumia kesi ya
Mchungaji Christopher Mtikila kama ni hoja mojawapo ya
kwamba kifungu cha 21 hakiwezi kutumika katika suala la
kutunga sheria ya kura ya maoni, kitu ambacho siyo sahihi.
Nina wasiwasi kwamba ufundi kama huu ungewezekana
kutumika katika kutumia andiko langu kuhalalisha yale
ambayo yanasesewa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, kumeelezwa hapa kwamba moja
ya tatizo la Sheria ya Ukaazi, kwamba inaathiri, na mfano
uliotolewa wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar ambaye yeye
mwenyewe hakujipigia kura. Ni kweli amefanya hilo kutokana

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA]
na Sheria hiyo ya Ukaazi. Lakini kama nilivyosema, hilo ni suala
la kulijadili katika Baraza la Wawakilishi kama sheria hiyo
inafaa au haifai, ibadilishwe nini.

Mheshimiwa Spika, binafsi nataka kumpongeza
Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, kwa kuthamini na kuheshimu
misingi hiyo ya sheria. Kama mgombea wa Urais, angeweza
kukunjakunja akatumia baadhi ya mbinu kwamba na yeze
apige kura. Lakini aliiheshimu na akafuata misingi hiyo ya
sheria. *(Makof)*

Mimi mwenyewe pia ni mmojawapo ambaye
sikujipigia kura kwa sababu Jimbo ambalo nimekwenda
kugombea, siyo Jimbo ambalo nimejiandikisha kupiga kura.
Lakini nimempigia mwenzangu Mbunge ambaye yumo humu
ndani, kwa sababu naishi katika sehemu hiyo. Lakini
nimefanya hivyo pia, tena kule Jimboni kwangu *CUF*hakuna,
ni wa kuhesabu tu.

Ningeweza kufanya mambo nikaweza nikapiga hata
Jimboni kwangu. Lakini nimefanya hivyo pia kwa kuheshimu
misingi ya sheria. Lakini na mwenzangu ambaye amekaa
Mheshimiwa Mbunge wa Chambani, naye nina habari za
uhakika kwamba hakujipigia kura kwa sababu pia ya
kuheshimu sheria hiyo hiyo.

Kwa hiyo, sheria ipo na ni halali, isipokuwa kama
tunayo matatizo nayo sheria hiyo, sehemu ya kuisemea ni
kwenye Baraza la Wawakilishi, ndiko kwenye mamlaka wa
kuweza kuibadilisha. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naomba
kuwasilisha. Ahsante. *(Makof)*

SPIKA: Ahsante kwa kutuelimisha. Sasa namwita
Mheshimiwa Shamis Vuai Nahodha.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kutoa maoni juu ya Muswada wa Kura ya Maoni.

Mheshimiwa Spika, tangu jana nimekuwa nikiwasikiliza kwa makini sana baadhi ya Wabunge wa CHADEMA na CUF. Katika michango yao wamependekeza kwamba Serikali itumie Sheria za Jamhuri ya Muungano katika Kura ya Maoni. Wametoa hoja mbili. Hoja ya kwanza; iwapo Sheria za Zanzibar zitatumika, wapo Wazanzibari kutokana na sharti la ukaazi watanyimwa fursa hiyo. Lakini hoja ya pili, ni sharti la kuwa na vyeti vya kuzaliwa.

Mheshimiwa Spika, hoja na ushauri huu inavutia sana ukiusikiliza. Lakini sina hakika na dhamira iliyomo ndani yake, sina hakika sana. Lakini kwa bahati mbaya mimi slo klongozi wa kiroho, kwa hiyo, siwezi kutafsiri dhamira zilizoko ndani ya roho za watu. Lakini nimesomea Ualimu, na kutokana na saikolojia ya Ualimu au Elimu, mtu akisema jambo naweza kujua dhamira yake ni nini. Kwa msingi huo basi, naiomba Serikali iwe makini sana katika kuzingatia ushauri huu unaotolewa. Nitatoa sababu tatu.

Mheshimiwa Spika, ya kwanza; Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka Bunge lilitopita, katika kikao kilichopita tulipokuwa tukijadili Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. Wabunge hawa hawa wanaojenga hoja hii, walisema Zanzibar ipewe haki yake, ipewe uwakilishi wa haki wa usawa, kwa sababu Zanzibar ni mdau wa Muungano, na mimi naikubali hoja hiyo ni ya msingi, ni kweli. Ndiyo maana wakati ule nilikaa kimya kwa sababu nilihisi wanazungumza jambo la maana. Lakini leo wanageuka.

Wanasema katika hili, tukifanya hivi sheria za Zanzibar zikitumika tutakuwa tunavunja Katiba ya Jamhuri ya Muungao. Sasa najiuliza, wamesahau walilolisema wakati ule? (*Makof!*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

/WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA/

Mheshimiwa Spika, Zanzibar, wamependekeza Sheria za Zanzibar za Uchaguzi zitumike katika kura ya Maoni. Wakaenda mbali, wakasema, kura zihesabiwe Zanzibar. Sasa Waheshimiwa Wabunge nauliza Wazanzibari na mwakilishi wao Serikali ya Umoja wa Kitaifa imesema hilo. Sasa sisi ni nani ambao tunapingana na ushauri wao? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo pili, kama hoja hii ya kutumia Sheria za Zanzibar katika Kura ya Maoni ni za msingi, na zinatetea maslahi mapana ya Zanzibar, basi busara inatutuma, nasema mahali pazuri pa kujenga msimamo ingelikuwa ni Baraza la Mapinduzi, kwa sababu Baraza la Mapinduzi, lina uwiano mzuri sana na wakaribu wa Mawaziri kutoka Chama cha Mapinduzi na Chama cha CUF. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili, hata Baraza la Wawakilishi lina uwiano huo huo ambao unakaribiana. Sasa napata taabu kidogo, nasema wenzetu Waheshimiwa Wabunge hawa wa Chama cha CUF, hivi wanatapa nafasi ya kukaa na Mawaziri na Viongozi wanaotokana na Chama chao, na kujuua maslahi mapana ya Zanzibar? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hata katika Majimbo yao pia wapo Wawakilishi katika Majimbo yao wanaotokana na chama chao. Sina hakika kama wanapata nafasi hiyo. Lakini nisiende huko, lakini cha msingi nasema ni vizuri tukayaheshimu maoni na mapendekezo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la tatu, kutokana na mitizamo hii inayobadilika badilika, mara Zanzibar isikilizwe, mara Zanzibar ishirikishwe. Mimi nadhani Serikali ya Muungano inapata taabu sana kuona ni wakati gani na kwa mambo gani Zanzibar isikilizwe na wakati gani Zanzibar isisikilizwe. Maana utaambiwa wakati mwingine ishirikishwe, wakati mwingine isishirikishwe.

Mheshimiwa Spika, najua sisi tunaofanya kazi katika Serikali ya Muungano, na hasa sisi wengine tunaotoka

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA]

Zanzibar, hasa mimi, napata taabu kweli! Napata taabu sana.

Mheshimiwa Spika, sasa ushauri wangu ni nini? Napenda kutoa ushauri ufuatao: Serikali ya Muungano naiomba sana isiingie kwenye mtego huu ulipo mbele yake. Tukiufuata ushauri huu wa kwamba Sheria za Muungano ndiyo zitumike katika Kura ya Maoni, tutaingia na malumbano na migogoro isiyokuwa na sababu na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mimi naomba tuuruke mtego huo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, najua wako Wazanzibari ambao watakosa fursa kutokana na masharti ya ukaazi.

Mheshimiwa Spika, Iakini kama alivyosema Mheshimiwa Mahadhi - Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, Sheria zetu za sasa za uchaguzi za Muungano zinaruhusu hivyo. Wazanzibari ambao hawana sifa ya kuandikishwa katika Daftari la Kudumu hasa tunapokuja katika masuala ambayo ni ya Muungano, utaratibu uko wazi wanaorodheshwa tu katika Daftari la Kudumu la Tume ya Uchaguzi ya Taifa, na utaratibu huu siyo mgeni, upo tu hata kwenye uchaguzi Mkuu wa Rais na Wabunge tunautumia utaratibu huu. Mimi nadhani hili litatusaidia sana katika kuwapatia haki Wazanzibari.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, limezungumzwa sana hapa kwa hisia kali, suala la sharti la ukaazi. Baadaye nitatoa pendekezo langu la ufumbuzi wake ni nini. Lakini kabla sijafika huko, niseme kwamba kwa nini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuja na pendekezo hili la sharti la ukaazi wa miaka mitatu katika Jimbo kama ni sharti kuu la kushiriki kwenye Uchaguzi wa Zanzibar?

Waheshimiwa Wabunge, mazingira ya Zanzibar tunayafahamu sana. Kwa bahati njema sana Wazanzibari ni wakereketwa sana wa shughuli za kisiasa. Sasa ilibainika wakati wa uchaguzi, na kwa sababu ya mazngira na masafa kuwa madogo sana kati ya Jimbo moja kwenda Jimbo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA]

lingine; pale Zanzibar, umbali kutoka Jimbo moja kwenda Jimbo lingine ni katika mita 500 mpaka kilomita moja.

Sasa katika hali hiyo Wapiga Kura ambao wanadhani Majimbo yao yako salama kwa kutetea ushindi wa vyama vyao fulani fulani, wanakuwa rahisi sana kutembea kwa miguu na kwenda kwenye Majimbo mengine. Ndiyo maana Serikali ikaja sasa na Sheria hiyo. Ni lazima kuwe na sharti. Sasa mimi sio Mwanasheria, inawezekana sana kwa nia safi kuwa jambo hili likawa linapingana na Katiba. Lakini nauliza: Je, dhamira yeke nayo ni mbaya? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kama ni suala la kuwabana watu wanaofanya ujanja na hila, mbona CCM nao inawezekana wanafanya hivyo hivyo; na Chama cha *CUF*, nao inawezekana wanafanya hivyo. Sasa hili dai la kwamba watu fulani wanaonewa, linatoka wapi?

Mheshimiwa Spika, hili nafikiri kwa sababu Mheshimiwa Mahadhi Maalim - Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, kasema mahali pazuri pa kushughulikia jambo hili ni kwenye Baraza la Wawakilishi. Lakini kwa sababu limesemwa hapa, nafikiri ni vizuri tu nami nilizungumze hapa.

Mheshimiwa Spika, nafikiri tumezisikia hoja na tumeusikia wasiwasi wa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, wanaposema kwamba baadhi ya wananchi wananyimwa haki zao kutokana na sheria hii ya Ukaazi. Basi mimi naiona ni busara, bahati nzuri mimi ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Napendekeza sisi Wabunge tunaotoka Zanzibar, tupate nafasi ya kukaa na wenzetu wa Baraza la Wawakilishi tulizungumze jambo hili. (*Makof*)

Kama iko mantiki ya kuona kwamba hii sheria ya miaka mitatu haifai tena, basi tuiangalie na tufanyie marekebisho. Lakini nasema hii siyo sheria ya pekee. Lakini kwa bahati mbaya wenzangu Wabunge wanaotokana na Chama cha *CUF*, wanazungumzia sheria hii tu. Iko sheria ambayo watu wa Zanzibar wenye asili ya Bara hawaipendi, lakini hawana cha kufanya, inayoitwa Sheria ya Mzanzibari,

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFAT]

ambayo inawataka Wazanzibari wenyewe asili ya Bara wanapoamua kukaa Zanzibar, sharti lake wakae miaka kumi. Mimi nasema, na hii si inavunja Katiba hivyo hivyo? Lakini baadhi ya watu wanaipenda hasa hawa wanaosema Sheria ya Ukaazi inawaudhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema haki ni haki tu. Kama ya miaka mitatu inawaudhi, ya miaka 10 je? Mbona miaka 10 ni mingi zaidi? Lakini kwa sababu ya miaka mitatu inatetea Chama fulani, ni nzuri. Lakini ya miaka 10 inawaonea watu wa Bara ambao wakati mwengine hatuwapendi, tunaona sawa tu. Mkuki kwa nguruwe! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa natoa ushauri ufuatao, na hasa na mimi ni mionganoni mwa wa wadau wanaopendekeza kamba ili kuepukana na tatizo hili la mashari ya ukaazi, ama kwa wale wa miaka 10 na miaka mitatu, mimi napendekeza Zanzibar sasa wakati umefika tuanzishe mjadala wa kuanzisha mfumo mpya wa uchaguzi ambao unaitwa *proportional representation*. (*Makofi*)

Mfumo wa Uchaguzi ambao hakutakuwa na shaka ya kuwaondoa watu kwenye Jimbo moja. Mnampigia Kura Rais wa Zanzibar, halafu Chama kinachoshinda mnapewa asilimia ya ushindi mlioupata na Chama cha Pili, kitapewa asilimia ya Wabunge au Wawakilishi kwa idadi mliyoipata kwenye kura. Tukifanya hivyo, misuguano ya kimajimbo, kuhamisha watu kutoka Jimbo moja kwenda katika Jimbo lingine itaondoka. Kwa maana hiyo Zanzibar yote itakuwa ni Jimbo moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nadhani huu ndiyo ufumbuzi wa kudumu. Sasa wale ambao kwa dhati ya moyo wao, kama kweli wanaipenda Zanzibar, nafikiri waniunge mkono, na nitafanya kila linalowezekana kuandaa hoja maalum katika Baraza la Wawakilishi juu ya jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maelezo hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mimi katika orodha yangu, wote waliomba kuchangia wamezungumza, isipokuwa mmoja ambaye hayumo humu ndani. Kwa hiyo, nimekamilisha. Ninawashukuru sana kwa sababu nilikuwa nataka hivyo, kwamba katika kipindi hiki cha asubuhi tuzungumze, halafu tukirudi saa 11.00 Jioni tuwape nafasi wenye hoja waanze kutoa majibu.

Kwa hiyo, hivyo hivyo wale ambao walikuwa na *Amendments* zao, naamini wamekutana na Kamati na wamejadili. Napenda hivyo kwa sababu ni kawaida katika Mabunge yote. Huwezi mtu kukurupuka tu na *Amendment* yako hapa ukategemea itakubalika. Kwa sababu inakuwa ni ya kwako mwenyewe. Kumbe utaratibu huu mwингine unashirikisha wengi zaidi na kujadili. Hata ikibidi hata ule upande wa pili nao wenye hoja yao wanaweza kupata nafasi pia ya kuona namna ya kufanya. Naomba hilli liwe hivyo, siyo kwamba tuwe na ufundi tu wa kurupuka na *Amendments*, hivyo sivyo tunavyofanya. Kwa sababu lengo letu ni kutunga Sheria ya Kudumu na si sheria zile ambazo tunasema kama hoja binafsi namna hii, hapana.

Kwa hiyo mimi nashukuru kwa wale waliokuwa na *Amendments* zao wameshirikiana huko, wamejadiliana. Kama nilivyosema, tukileta maneno yetu hapa siyo lazima wenzako wayakubali jamani. Mkishakubali hilo, tutakuwa tunatunga sheria. Hivyo siyo kwamba na wewe ukileta *amendments* lazima waikatae, hata kama ina mantiki, nayo siyo sahihi.

Kama ina mantiki tupime mantiki ya hoja zile, bila kujali ni nani aliyeleta. Utakuta jioni tukija hapa, ameleta Mheshimiwa Tundu Lissu, wa Tundu Lissu wote watafuatana. Ameleta sijui nani huyo na akina nani, wote watafutana. Jamani, sivyo! Tunatunga sheria ya nchi jamani! (*Makofi*)

Kama Mheshimiwa Tundu Lissu, kaleta kitu cha maana tumuunge mkono. Kama ameleta kitu chenye hoja ya kutupeleka mbele, tuunge mkono bila ya kujali. Kama ameleta kitu kisicho na maana na tuseme sababu lakini, siyo

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[SPIKA]

tupinge tu, tuseme na sababu. Kwa hiyo, nadhani tukienda hivyo, tutakuwa na *political maturity* kwa watunga sheria. Hatuna hiyo! Ndiyo kasoro yetu kubwa.

Hatuna *political maturity*. Kama Waheshimiwa hamtajifunza hivyo, hamtakuwa wanasiasa. Muda wenu utakuwa mfupi sana katika maisha ya siasa. Kwa sababu ni lazima tuwe na *political maturity* na kuelewa kwamba sisi tuwaangalia watu walioitulo hapa, vyama vyetu baadaye. Wote tuna klabu zetu huko huko, mtagombana huko huko, mtamaliza, lakini hapa tuwawakilishe wananchi.

Kwa hiyo, nawaombeni sana tutakaporudi jioni tutakwenda kwa utulivu sana, tutasikiliza *amendments* moja baada ya nyingine, tutafanya maamuzi. Kwa hiyo, niwashukuru kwa mchango tuliokuwanao hapa, na hizi *innuendo* zenu mlizofanya, hapa *please*, kila mtu akae nayo peke yake. Hizo *innuendo* mlizofanya hapa kila mtu abakie nayo yeye mwenyewe kama roho yake ilimpendeza. Lakini haikuwa na manufaa kwetu sisi kama nchi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo moja muhimu kabisa. Hivi sasa mimi nadaiwa kutoa Taarifa hapa Bungeni kwamba Wabunge ambao hawakutangaza mali zao mwaka 2012 na wanaitwa na Baraza la Madili. Hilo ni Baraza kabisa! Kuna mwenzetu amepata adhabu humu!

MBUNGE FULANI: Ni nani huyo?

SPIKA: Simtangazi!

Kwa hiyo, nawaomba sasa tarehe 30 Desemba, 2013, iko mlangoni. Kwa hiyo, nimeombwa niwatangazie Wabunge kwamba Afisa wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi yuko eneo la Mapokezi katika Jengo la Utawala kwa ajili ya kukusanya fomu za tamko za mali na madeni za Wabugne ambao hawajarejesha. Tafadhali tumieni nafasi hii kuondoa usumbufu wa kuzipeleka kwenye Ofisi ya Kanda. Unaweza pia Ofisi ya Kanda ukapeleka na isipelekwe Makao Makuu na ukashtakiwa hivyo hivyo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

Waheshimiwa Wabunge, nawaomba msilifanyie jambo hili mzaha, lina *implications* zake mbaya kwenu. Wale wahusika wako pale, pelekani fomu, wasiochukua wajaze, tarehe 30 Desemba, 2013 ni kesho tu. Kwa hiyo, hili jambo ni muhimu sana msilisahau wala msilizembee.

Sasa baada ya kusema hivyo, naomba nisitishe shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 6.53 Bunge lilitishwa Mpaka Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kipindi cha asubuhi nilisema wachangiaji wote kutoka kundi la Wabunge walimalizika, sasa tuanze na wenye Muswada na waanze kujibu na nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, nami nishukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia Muswada huu uliopo mbele yetu. Lakini kabla sijaendelea napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, (Sera, Uratibu na Bunge). Lakini pia napenda kuwashukuru na kuwapongeza sana Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na vilevile Wabunge wote ambao wamechangia hoja hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu uliopo mbele yetu ni kielelezo halisi cha nia ya Serikali katika kuhakikisha kwamba mchakato huu wa mabadiliko ya Katiba unaendelea, lakini pia unakuja kukamilika na hii ni mwendelezo tu wa hatua mbalimbali ambazo zinahitajika kabla ya kufikia kwenye kupitisha Katiba hiyo inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu wa Kura ya Maoni utakapopitishwa utaipelekea nchi yetu kuwa na historia ya kipekee, kwani hivi sasa tutakuwa na muundo wa kisheria na kitaasisi ambao utaainisha ni namna gani basi masuala ya

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIAJ

kura ya maoni yatakavyoendeshwa lakini pia ni namna gani Katiba hii inayopendekezwa itakavyoweza kupitishwa katika kura ya maoni.

Mheshimiwa Spika, wako ambao walikuwa na hofu mbalimbali, napenda kuwatoa Waheshimiwa Wabunge waliokuwa na hofu, tuwe na imani. Imani huzaa imani na unapokuwa katika majadiliano yoyote siyo rahisi wote kukubaliana. Tukubaliane kutokukubaliana, lakini pia tuwekeane staha na cha msingi ni kwa yale mambo ambayo yanatuunganisha na siyo kuzingatia mambo ambayo yanatugawa.

Mheshimiwa Spika, nikianza katika kuchangia Muswada huu kuhusiana kwanza na endapo ibara ya 21 inaweza kuhalalisha mchakato wa kura ya maoni.

Mheshimiwa Spika, katika ibara ya 21 sina haja ya kurudia kwani wengi wamebainisha kama Mheshimiwa Simbachawene, Mheshimiwa Mahadhi lakini pia Mheshimiwa Waziri aliyewasilisha Muswada huu.

Ukiangalia katika ibara ya 21 ndiyo inayotoa uhalali wa wananchi kutoa maamuzi mbalimbali kuhusu mambo yanayowahusu, yanayohusu maisha yao lakini pia yanayaohusu maslahi ya Taifa letu. Siyo mara ya kwanza nchi yetu imepitia michakato mbalimbali ya kuhitaji kura mbalimbali za wananchi wetu ili kupata maamuzi ya masuala mbalimbali.

Ukiangalia katika mwaka 1965 kupitia agizo la Mheshimiwa Rais tulipitisha Katiba kupitia mfumo huo, lakini pia mwaka 1977, 1984 na vilevile 1992 wakati tulipokuwa tunataka kuingia katika Mfumo wa Vyama Vingi nako pia tulitafuta maoni mbalimbali ya wananchi kupitia waraka wa *White Paper*.

Mheshimiwa Spika, napenda tu kutoa angalizo kwamba wako watu wengine wanaisema kwamba ibara hii hairuhusu mchakato wa Kura ya Maoni, lakini vilevile hakuna

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA]

sehemu yoyote ambayo Katiba imeharamisha kuwa na Kura ya Maoni. Kwa hiyo, nasema ni halali kuwa na mchakato huu na ndiyo mchakato ambao kwa kweli utatufikisha katika kuwa na uamuzi katika suala hili zito la Katiba, ni suala zito, linaweza likababuwa muundo wa Muungano, linaweza likapelekeea kubadilisha muundo wa Serikali, kwa hiyo, ni vyema wananchi wenyewe nchi yao waweze kutoa maamuzi katika suala hili zito.

Mheshimiwa Spika, nikija katika ibara ya (4) ya Muswada huu, wako ambao walikuwa wanahoji ni kwa nini sasa Mheshimiwa Rais peke ndio awe na mamlaka ya kuelekeza Kura ya Maoni kufanyika?

Mheshimiwa Spika, wako ambao walikuwa anapendekeza hata Azimio la Bunge liweze kutolewa kuendesha Kura ya Maoni, wapo ambao walikuwa wanapendelea wananchi wenyewe waweze kuitisha Kura ya Maoni, lakini mimi nasema, ibara hii ni sahihi kabisa, Mheshimiwa Rais aendelee kuwa na mamlaka ya kuelekeza Tume kuitisha Kura ya Maoni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sio hilo tu, labda hoja hii ingeweza kuwa na mantiki au na msingi huko mwanzoni kabla Muswada huu haujarekebishwa. Wote mtakumbuka kwamba Muswada ambao ulichapishwa awali ulikuwa umeruhusu Kura ya Maoni katika jambo lolote litakalojitokeza litakalohitaji Kura ya Maoni. Lakini hivi sasa Muswada huu unahu Katiba mpya peke yake. Wananchi wameshirikishwa katika hatua mbalimbali, wametoa maoni katika rasimu ya kwanza, wananchi wameweza kutoa maoni katika Mabaraza ya Katiba.

Vilevile ukiangalia katika *aspect* ya Wabunge au Azimio la Bunge na lenyewe pia Wabunge watashirikishwa kuititia Bunge la Katiba na watajadili na kuipitisha Katiba hii inayopendekezwa. Lakini mwisho wa siku ndiyo maana tunakuja na sheria hii ya Kura ya Maoni ambapo wananchi wote kwa ujumla wao, aidha ni Wabunge, aidha ni mwananchi mmoja mmoja lakini wote wataweza kushiriki

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA]

kuipigia kura Katiba hii inayopendekezwa. Kwa hiyo, naona bado ni sahihi na ninaunga mkono ibara hiyo ya (4).

Mheshimiwa Spika, nikija katika mapendekezo mbalimbali ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na kuanzishwa kwa Tume huru ya masuala ya Kura ya Maoni.

Mimi naunga mkono mapendekezo kama yalivyo hivi sasa katika Muswada huu, kwa sababu katika Muswada huu ni Tume ya Uchaguzi ya Taifa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ndizo ambazo zimepewa mamlaka. Lakini wako ambaao wana hofu kwamba ni lazima tuunde Tume huru itakayosimamia masuala ya kura ya maoni, lakini Tume huru ya uchaguzi unaangalia masuala gani mpaka unasema ni huru au siyo huru? Zipo Nyanja mbalimbali ambazo zinaweza kuangaliwa kupima kama Tume ipo huru au la.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika eneo la kwanza ni uteuzi wenyewe wa Wajumbe. Wote tumekuwa tukiona mara kadhaa Waheshimiwa Wajumbe wana sifa zao na wamefuata vigezo mbalimbali ambavyo Mheshimiwa Rais alivizingatia katika kuwateua.

Katika eneo la pili, ni upatikanaji wa fedha. Mara zote Serikali imekuwa ikihakikisha kwamba Tume inapatiwa fedha za kutosha za kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu, ni namna gani basi Tume hiyo inalindwa na Katiba? Wote mtakubaliana nami katika ibara ya 74(6) ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano, imelinda Tume, imeitambua na hakuna shaka yoyote.

Mheshimiwa Spika, mwisho katika eneo la nne ni kuhusiana na muda wa Utumishi wa Tume (*Security of tenure*). Waheshimiwa Wajumbe hawa wanapokuwa wameteuliwa ni mpaka watakapo kwa wamemaliza kipindi chao cha uteuzi ndipo watakapoondoka katika Tume hiyo. Hakuna hata mara moja aliywateua anaweza kuingilia kuwaondoa katika ujumbe wao.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA]

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, pamoja na kwamba Mheshimiwa Rais ndiye anayewateua, Mheshimiwa Rais anawateua kama Mkuu wa Nchi. Mara zote hatujawahi kusikia hata mara moja ni lini Mheshimiwaa Rais ameweza kuingilia utendaji wao. Lakini vilevile Mheshimiwa Rais anapowateua anazingatia sifa na vigezo mbalimbali vilivyoainishwa katika masharti ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, niombe tu kwamba jamani, Tume hii mnayoilalamikia ndiyo ambayo imetuingiza Waheshimiwa Wabunge hapa. Wakati matokeo yanatangazwa, hakuna hata mmoja aliyesema mimi sitaki kwa sababu sina imani nayo. Kwa hiyo, naomba sana tuisiwavunje moyo, kwani imani huzaa imani, tuwape ushirikiano ili tuweze kupata Katiba nzuri tunayoitarajia itakayotutoa hapa kwenda miaka 50 ijayo na zaidi. (*Makofii*)

Vile vile katika hoja ya tatu, wako amba walikuwa wanasema kwamba tutafute Tume nyingine, bado haina mantiki. Nchi mbalimbali za *SADC*, wote wamekuwa wakitumia Tume ya Taifa ya uchaguzi katika kuendesha mchakato mbalimbali wa Kura ya Maoni. Ukiangalia katika *ECOWAS*, nchi za Afrika Magharibi, Liberia na nyinginez, wote wamekuwa wakitumia. Wapo amba walitoa mfano wa nchi ya Kenya, lakini vilevile na sisi Tanzania lazima tujisikie na tujivunie, ni nani na sisi atatoa mfano wa Tanzania? Tunatengeneza na sisi sheria na mfumo kwa ajili ya mazingira ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda tu kusema katika eneo lingine kuhusiana na namna ya kupinga matokeo ya Kura ya Maoni. Mheshimiwa Christine M. Lissu aliliongelea hili. Katika kifungu cha 43(2) kipo bayana kabisa. Wapo amba wamesema kwamba 10% kupata idadi ya waliopiga kura katika Majimbo mbalimbali itakuwa ni taabu.

Napenda tu kuwaelimisha Waheshimiwa Wabunge kwamba dhamira ya kifungu hiki cha 43(2), Kamati hii inayokusudiwa hapa ni Kamati ya Kura ya Maoni ya Kitaifa. Kila Kamati ya Kura ya Maoni ya Kitaifa itakuwa ina Wajumbe

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA]

wake kutoka Majimbo mbalimbali. Kwa hiyo, sidhani kabisa kwamba itakuwa ni kazi kupata 10% ya idadi ya kura kutoka katika Majimbo matano Zanzibar na kutoka katika Majimbo matano Tanzania Bara.

Eneo lingine ambalo Mheshimiwa Christine Mughwa alikuwa na hofu ni katika kifungu cha 43(3) kuhusu muda wa kupinga matokeo ya Kura ya Maoni. Ukiangalia katika kifungu cha 43(3) iko wazi kabisa kwamba ni siku 14. Sidhani kama kuna mashaka yoyote. Kamati hii ya kitaifa ni moja. Ni vitu gani hivyo unavyoviandaa ambavyo siku 14 zisitoshe? Tumejionea hapa Waheshimiwa mbalimbali ambaao wamekuwa wakigombea Urais ndani ya siku chache tu wamekuwa wakipata sahihi zile zinazohitajika kukidhi matakwa ya kugombea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba hili lipo sahihi kabisa na idadi hii inatosha kabisa ili kuhakikisha kwamba kweli amepata dhamira ya wale aliokuwa anawawakilisha katika Kamati hii ya Kitaifa.

Kwa hiyo, tunaomba sana mtukubalie kifungu hiki kiendelee kama kilivyo kwani kinatosha. Lakini siyo hivyo tu, tutakapoongeza muda zaidi tutajikuta mchakato huu basi hatutakaa tuupate kabisa Katiba hii mpya inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Padogo hapa!

SPIKA: Hama hapo, sogea mbele. Hapo huwa mnajikunja watu warefu hamfai kabisa kukaa hapo.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, nami naomba kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kulisaidia Bunge katika mambo ambayo yapo mbele yetu.

Naomba pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wa pande zote hapa Bungeni kwa michango yao mizuri na utulivu wao katika kuchangia hoja.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kwamba tunaanza kubadilika na sasa tunaanza kutunga sheria. Nichukue nafasi hii pia kuwashukuru watu ambao wametusaidia nje ya pazia; watumishi, maafisa wa Ofisi yangu pamoja na Tume ya Uchaguzi *NEC* pamoja na *ZEC* na wenzangu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa ajili ya kuzungumzia mambo mawili tu ili kusudi nitoe nafasi ya kuzungumzia mambo haya kwa kina kwenye vifungu kwa kifungu.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja mbili na nitazungumza kwa kifupi. Kuna hoja kwamba mchakato huu unakiuka Katiba. Naomba hapa kumshukuru sana Mheshimiwa George Simbachawene na Mheshimiwa Mahadhi Maalim kwa michango yao kwenye jambo hili. Mimi naongezea tu katika sehemu moja.

Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba mchakato huu unavunja Katiba kama ambavyo lilisemwa jana na kama ilivyoonyeshwa kwenye baadhi magazeti leo. Napenda kuchukua nafasi hii, kuwashauri wenzetu wa magazeti kwamba na wenyewe inapaswa kusoma vitu kabla ya kuvitoa kwa umma kwa sababu vingine vinapotosha. Nadhani kinachohitajika hapa ni elimu.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la mchakato huu unahusu sheria itakayoismamia Kura ya Maoni ambayo ni Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ambayo tayari tuliipitisha hapa na sasa ni sura ya 83 ya sheria zetu. Jambo kubwa

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]

linalokusudiwa katika mchakato huu ni mabadiliko ya Katiba ya nchi. Watanzania wenzetu, sote tunataka Katiba Mpya. Kila mtu na kila Mbunge anafahamu sasa kwamba tuko kwenye mchakato wa kubadilisha Katiba yetu ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni ambao uko mbele yako, unajitambulisha kama Muswada wa Sheria itakayoweka Muundo wa kisheria na kitaasisi katika uendeshaji wa Kura ya Maoni juu ya Katiba inayopendekezwa. Kama tunakubaliana na mawanda hayo, ni wazi kwamba katiba ya Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa jedwali la kwanza la Katiba linalowekwa kwa masharti ya ibara ya (4) ya Katiba ndilo jambo la Muungano. Mabadiliko ya Katiba yanayotarajiwa kuamriwa kwa Kura ya Maoni ni mambo ya Kikatiba ya kuweka Muundo wa Muungano, madaraka ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na pia yaweza kubadilisha mambo haya ya Muungano. Inawezekana kuathiri pia uwepo wa Jamhuri ya Muungano.

Hayo ndiyo mambo tunayozungumza na ndio tunayoyatarajia kuwekwa kwenye Kura ya Maoni. Sasa Watanzania kama raia wa Tanzania wanayo haki kwa mujibu wa Ibara ya 21 imeshazungumzwa sana, haki ya kimsingi (*fundamental right*) ambayo huwezi kumnyang'anya mtu kufikia uamuzi juu ya mambo haya yanayotuhusu sote. Kura ya Maoni ni utaratibu tu unaomwezesha kufikia kwenye lengo hili na hakuna msingi kwenye jambo hili la Muungano kusema kwamba utaratibu huu siyo wa Muungano. Kwa nini?

Kwanza Katiba yenyewe kama alivyosema Naibu Waziri haiweki utaratibu wa kufanya hivyo. Pili, haizuij utaratibu huu. Kile ambacho hakizuiwi, kinaruhusiwa. Tumewahi kufanya hivyo kwenye *whitepaper* kwenye mfumo wa Vyama vingi na hatukuwa na matatizo. (*Makofii*)

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilifanya mchakato huu baada ya kutunga sheria bila kubadilisha Katiba. Tatu, sababu ya mapendekezo yaliyotolewa na kutenganishwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]

na Kura ya Maoni na Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ilikuwa ni kuweka sheria inayosimamia jambo moja tu la Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hoja inayojengwa kwamba Kura ya Maoni siyo jambo la Muungano, haina sifa zozote za kitafiti na mimi sitaki kuendelea zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna hoja ya mwisho pia kwamba sheria hii itakwenda kwenye Baraza la Wawakilishi ili kupata ridhaa. Kwa bahati mbaya ushauri huo siyo sahihi. Kinachotakiwa hapa ni kwamba sheria yoyote ambayo inafuata masharti ya Ibara ya 64 ya Katiba ya Nchi, Ibara ya 98 ya Katiba ya Nchi na ibara ya 100 inayowapa ninyi Waheshimiwa Wabunge uhuru wa kusema, inapelekwa kwenye Baraza la Wawakilishi siyo kupata ridhaa. Siyo kwenye *ratification*, inakwenda kama tunavyofanya kwenye vitu vingine hapa, inakuwa *laid'* inapelekwa kwa taarifa, siyo kwa ajili ya ridhaa. Hili ni suala la Kikataba, ni vizuri Waheshimiwa Wabunge mfahamu mipaka ya jambo linalofanywa hapa kwa utaratibu ambaao haukiuki Katiba. Likimalizika, linapelekwa kwenye Baraza la Wawakilishi, haliendi kwa ajili ya ridhaa.

Napenda kusisitiza hiyo kwa sababu nimeona kwenye wasilisho la Mhesimiwa Tundu Lissu, alikuwa anasema kwamba, tujihadhari, itakwenda kwenye Baraza la Wawakilishi ili kupata ridhaa. Hakuna ridhaa! Ibara ya 132 ya Katiba ya Zanzibar ipo wazi, inasema tu kwamba itapelekwa kwenye Baraza la Wawakilishi, siyo kwa ajili ya majadiliano ila kwa ajili ya taarifa.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri sasa utaratibu ambaao umezoleka na masharti ambayo yanatolewa na Katiba ya Zanzibar ni kwamba Sheria itakayopitisha Bunge lako Tukufu iwe ni Sheria inayohusu mambo ya Muungano. Sheria ya Kura ya Maoni tumeona kwenye Ibara za mwanzo, Ibara ya (2) ni kwamba inahusu mambo ya Muungano. Pia ipitishwe kulingana na maelekezo yaliyo chini ya vifungu vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Utaratibu huo wa Ibara ya 97 pamoja na Ibara ya 98 umefuatwa.

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu na la mwisho, linahusu kwamba tulihitaji kubadilisha Ibara ya 98 ili kuruhusu mchakato huu upite. Imesemwa kwamba tunasukuma; nafikiri kuna maneno yametumika, kauli ya kufunika kombe *dash dash* apite. Nafikiri hii *dash dash* ni "mwanaharamu". Sasa hii siyo lugha ya Kibunge. Kwenye matumizi haya ya haki za watoto hatutumii neno hili "mwanaharamu". Kwa kweli ni kukiuka haki za watoto, nafikiri Wabunge wenzangu tuepuke maneno hayo.

Mwisho, kuna maoni kwamba hii Kura ya Maoni kwa kweli siyo Kura ya Maoni, ni Kura ya Maamuzi. Ni kweli. Ni kura ya Maamuzi kwa sababu maoni yao yanasema unaikubali Katiba au huikubali? Ukitsema huikubali ni uamuzi. Lakini jambo ambalo limezoleka sasa ni *referendum*, yaani ni Kura ya Maoni. Yaani katika isimu ya maneno haya, ukisema Kura ya Uamuzi, haleleweki vizuri. Lakini *essentially* hii ni Kura ya Uamuzi.

Mheshimiwa Spika, nafikiri *semantics* siwezi kuingia ndani zaidi kwa sababu ya muda, wale ambao watapenda labda baada ya Muswada huu tunayo mada wanaweza wakachukua wakasoma.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera, Uratibu na Bunge).

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, naomba kwanza niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Muswada na huu na kutokana na umuhimu wake, Wabunge waliochangia kwa kusema ni 32, lakini pia wapo Waheshimiwa Wabunge walioandika ambao wanapata 10.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana wote waliochangia, nafikiri muda huu wa siku mbili tumeutumia vizuri. Yapo mambo mengi sana yamezungumzwa, lakini kwa sababu tunatunga Sheria, yalikuwa ya aina mbili.

Moja, wengi walikuwa wanataka tufanye marekebisho katika vifungu mbalimbali, na mtaangalia kwenye Marekebisho ambayo nakala zake tumewapeni, yaliyo mengi ya msingi tumefanya. Mengi! Kwa hiyo, naomba mpitie vifungu hivyo vilivyofanyiwa marekebisho, mtagundua kwamba wengi mliosema yale ya msingi, hata haki ya Wazanzibar kupiga kura, yote nayo imezingatiwa kwenye hiyo *Schedule of Amendment*.

Mheshimiwa Spika, kati ya waliosema, naomba niweke rekodi sawa maelezo kwanza ya Mheshimiwa Habib Mnyaa, ye ye ali sema hoja moja, kwamba Mheshimiwa Rais wa Zanzibar hakuweza kupiga kura kutokana na kukosa kitambulisho cha Mzanzibar Mkaazi kilichotolewa kwa mujibu wa Sheria Na. 7 ya mwaka 2005. Sasa hii nataka kuweka sawa, siyo kweli. Mheshimiwa Rais wa Zanzibar anacho hiki kikadi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar hakupiga kura Zanzibar kutokana na kuwa alikuwa amejiandikisha Bara, siyo kwa sababu ya kukosa ile kadi. Alijiandikisha Bara. Kimsingi Mheshimiwa Rais alikuwa na sifa zote za kuandikishwa Zanzibar, ikiwemo kuwa na kitambulisho cha Mzanzibar Mkaazi ambacho alikitumia kugombea nafasi ya Urais Zanzibar. Mheshimiwa Rais alitumia haki yake ya kujijandikisha katika daftari la NEC kwa kuwa, wakati huo alikuwa anafanya kazi na kuishi Tanzania Bara.

Kwa hiyo, hii nilitaka kuweka rekodi maana walitaka *ku-justify* kwamba sifa iliyomfanya asipige kura ni kitambulisho cha Ukaazi. Hapana, anacho na alikuwa nacho na alikitumia wakati anagombea urais. Kwa hiyo, nilitaka kuweka hiyo rekodi ya kwanza sawasawa.

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, nilifikiri niwataoe hofu Waheshimiwa Wabunge. Muswada huu umejadiliwa, lakini wengi wakijadili niliwaona kama wana hofu kubwa sana kwamba katika *process* hii, hili ndiyo litakuwa tukio la mwisho kuhalalisha Katiba. Kwa sababu Katiba yetu hii imepita katika *process* hizo zote tatu. Maoni yamekwisha, tunasubiri Bunge, na baadaye tutakuja kwenye Kura ya Maoni.

Mheshimiwa Spika, nataka niwaondoe hofu na ninawaombe tu Waheshimiwa Wabunge na wale watakaokuwa Wajumbe wa Bunge la Katiba. Mimi naamini kwamba kazi nzuri ikifanywa ndani ya Bunge la Katiba itakuwa imerahisisha sana utekelezaji wa Sheria hii. Kama Wajumbe wote wa Bunge la Katiba tukiwemo sisi Waheshimiwa Wabunge, maana sisi Wabunge wote ni Wajumbe Bunge hili litakalokuja la Katiba. Wabunge, Taasisi mbalimbali za Jamii, *NGOs*, Vyama vyta Siasa na wote wengine watakaoshiriki, tukiwa wamoja, na tukitoka hapa wamoja, matumizi ya Sheria hii yatakuwa mapesi sana.

Mheshimiwa Spika, lakini kama tukiendeleza hofu kwenye Bunge la Katiba, tukijenga tabaka la Vyama, tabaka la Itikadi, tusipoafikiana Sheria hii tunayoitunga leo na yenye we itakuwa ngumu sana kutekelezeka. Kwa sababu inaweza ikasababisha mapambano. Kwa hiyo, rai yangu, naomba sana viongozi wote wa makundi mbalimbali yatakayoleta Wabunge wa Bunge la Katiba, tuzungumze ndani ya Bunge, nje ya Bunge hata kuanzia sasa kwa sababu wote tunajua ni mambo katika Rasimu ile yatakayotuvutanisha sana.

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri kuanzia leo tuanze kuzungumza ili tupunguze hizo tofauti ili tukifika hapa basi tuwe tunasahihisha au kurekebisha, lakini mambo ya msingi tumeelewana, nami ningefurahi sana tuelewane kwa sababu hakuna jambo ambalo nchi hii limetushinda kuelewana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hiyo ndiyo rai yangu kwamba kama tukitumia muda vizuri kwenye Bunge la Katiba tukaelewana, Sheria hii itakuwa nyepesi sana. Hofu inayokuja

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE))
ni hiyo kana kwamba sisi tutakaokaa kwenye Bunge la Katiba
hatutaelewana, kwa hiyo, tutapeleka kwa wananchi
Muswada au Katiba ambayo sisi wenyewe hatukuelewana.
Tukifanya hivyo, basi hizo kampeni na elimu havitaelewaka.

Maana kwa Sheria hii kutakuwa na maeneo ambayo
tutafanya kampeni na bado tutatoa elimu, lakini kama
hatutaelewa katika kutunga hiyo rasimu yenye, basi hata
kama hiyo elimu tungeitoa namna gani hatutaelewana.

Kwa hiyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge
kwa sababu najua wenzetu wanaokuja sisi ndio wenyehi wao,
ndio tuliotunga Sheria kuanzia mwanzo mpaka mwisho,
tuelewane ili tuweka muafaka wa Kitaifa, tuelewane tujenge
kitu kimoja. Hata tukimeguka, kundi moja likishinda kwa kura
asilimia mbili, tatu, hiyo Katiba itakuwa na matatizo maisha
yote. Kwa hiyo, mimi nafikiri tumeelewana. Siku hizi za karibuni
tumekuwa tunaelewana katika *process* hii; tumeshindana
hana, tunatoka nje, tunazungumza, lakini tunakuwa wamoja
tunarudi.

Tutumie uzoefu huo, Mheshimiwa Rais ametufundisha
kwamba tunapokuwa pamoja, tukikaa pamoja tukizungumza
kama *stakeholders* huwa tunatoka na jibu linakuwa moja na
tunakuwa wamoja kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, uzoefu ambao
Mheshimiwa Rais ametufundisha, nafikiri ni lazima, kwa
sababu ye ye sio Mjumbe; sasa tuchukue ule uzoefu tuubebe
sisi, tukae pamoja, makundi tofauti tuulizane. Maana hata
sasa hatujui hofu inatoka wapi? Mimi sijui hata wadau
wenzangu waliomo humu CHADEMA wana hofu gani na
CCM au CCM wana hofu gani na *CUF*? Sijajua! Kwa sababu
hatuambizani ukweli, yaani hatuulizani; hofu yako nini?
Pengine unachohofia wewe na mimi nahofia hicho hicho.
Sasa tuelewane tu ili tutulize hizo hofu. Tunaweza kufa kwa
kihoro hapa kumbe hofu yetu wote ni jambo moja tu.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nashauri tuzungumze ili
angalau Muswada huu ambao naamini tutaupitisha leo,

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]
utekelezeke kiraishi sana. Vinginevyo natabiri kwamba inaweza kuwa hata Sheria nzuri namna gani, lakini nia yetu isikamilike.

Mheshimiwa Spika, nimeona liseme hilo kwa sababu hasa nimeona ndiyo msingi wa hofu. Nani atapiga kura? Itakuwaje? Sijui vipindi gani? Masahihisho mengi yatakuja hapa, akina Mheshimiwa Mnyika wataleta mkeka wa marekebisho haya, lakini yote yale yanaziba matundu ya hofu. Hofu tu! Lakini sasa dawa ya hofu ipo na tumejenga uzoefu. Bunge hili tunaweza tukasimamia, tukatekeleza mambo yote vizuri.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye utangulizi na kama wengi walivyosema, hofu nyiningine inatokana na Tume hizi za Uchaguzi. Lakini nataka nisemee Daftari la Wapiga Kura. Wenzetu Zanzibar wameshafanya, wamefikia hatua kubwa. Wameshamaliza kusajili, sasa imebaki hatua ya kubandika tu. Sisi huku nataka niwahakikishie kama nilivysoma kwenye hotuba yangu, kazi hiyo tunaifanya. Serikali imeshatoa fedha zote za awali za maandalizi kwa ajili ya maandalizi ya kuainisha vituo vyote vitakavyotumika kupigia kura ya maoni na maandalizi ya msingi. Fedha hizo tumeshawapa Tume na wameanza kuzitumia. Sasa hivi wameanza *process* ya ununuzi wa mitambo ya kisasa itakayotumika katika kufanyia usajili wa wapiga kura.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kazi hiyo nataka niwatoe hofu, na nilisema juzi kwenye hotuba kwamba zoezi hili la Kura hii ya Maoni, halitafanyika mpaka zoezi hili la urekebishaji wa Daftari la Wapiga Kura limefanyika. Kwa hiyo, hofu nyiningine hii naomba msiwe nayo kwa sababu hata kwenye bajeti tuliweka fedha za kutosha za kuendesha zoezi hili, na tunazo na tutazitumia katika kuhakikisha kwamba Daftari letu la limeboreshwa kama wenzetu Zanzibar walivyofanya.

Kwa hiyo, Daftari la Wapiga Kura litarekebishwa, kila mtu mwenye haki ya kupiga kura atapiga, awe Mtanzania Bara, Mtanzania Visiwani na kura zitahesabika kwa mujibu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE))
wa Sheria na kila watu watahesabu kura upande wao, tutajua Watanzania Bara wanaounga mkono Katiba hii kwa asilimia ngapi na Wazanzibar wanaounga mkono Katiba hii kwa asilimia ngapi? Kwa kutumia Wawakilishi wao watakaopiga kura waliosajiliwa kwenye Madaftari ya Kupigia Kura ya ZEC na NEC.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba mbalimbali ambazo majedwali haya tumegawa ya marekebisho tumezingatia sana maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, lakini pia tumezingatia maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani na tumezingatia na maoni ya wasemaji wengine waliochangia hoja mbalimbali kwa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mwanzo, kwa kuwa, huu Muswada wa kutunga Sheria, nilifikiri niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge tushirikiane katika kuyasoma hayo majedwali vizuri ili tuweze kuona tulichokizingatia tukilinganishe na Sheria yetu na kwa umaja wetu niwaombe sana tushirikiane, tupitishe Sheria hii ili iweze kutuhitimishia vizuri mchakato wetu wa utungaji wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, niliwasilisha kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba niunge mkono hoja hii ili nimpishe mwenye Muswada aweze kuhitimisha hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa mtoa hoja.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kusema mambo machache sana kuhusiana na Muswada uliopo mbele yetu. Lakini kubwa nataka niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla wenu kwa michango mliyoitoa, mmeitoa kwa hisia tofauti, sikushangaa sana. Lakini kwangu mimi pamoja na wenzangu huku tulikuwa zaidi tunajali kipi kimesemwa ambacho tunafikiri ni vizuri kikapewa uzito unaotakiwa kwa maana ya kukubali kufanya marekebisho hapa na pale kwa lengo la kwenda mbele.

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Mheshimiwa Spika, lakini pengine kwa namna ya pekee niwashukuru sana wenzangu wa upande wa Upinzani, maana nilikuja sikuwa na uhakika kama watacaa mpaka mwisho, maana nilihisi pengine watatoka nje kama ambavyo wamekuwa wanafanya mara nyininge. Lakini safari hii kwa kweli ukomavu wa hali ya juu sana umeonyeshwa.

Kwa hiyo, nami nataka niwashukuru sana katika jambo hili zuri na kwa kweli niwasihi, hata huko tunakokwenda, hii ndiyo njia sahihi. Tunakutana, tunabishana, hata tukirushiana maneno, lakini bado tunaendelea kuwa ni Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mwisho wa yote hatutakosa kupata maeneo ambayo tunaafikiana kwa maslahi ya nchi yetu. Kwa hiyo, kwa kweli kwa hili nasema tunashukuru sana, ndiyo maana Muswada umeona umejadiliwa vizuri sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tangu tumeanza zoezi hili linalotupeleka katika kuwa na Katiba mpya, wote mnajua tumetoka wapi na sasa tupo wapi. Lakini nataka niseme tu kwamba tumepitia katika hatua mbalimbali, na katika kila hatua tulipotakiwa kuja Bungeni hapa ama kuleta Sheria au Sheria ya Mabadiliko, kuna mambo ambayo nimeona ni vizuri niyaseme hata katika hatua hii sasa ambayo tunajadili Muswada wa Kura ya Maoni.

Mheshimiwa Spika, jambo moja ambalo tumelizingatia sana, kwanza, ni kuhakikisha sisi wenyewe Serikalini tunajandaa vizuri ili tuwe na mapendekezo ambayo tunaamini hata yakiletwa Bungeni yataungwa mkono na Wabunge wengi.

La pili, muda wote tumejitahidi sana kuhakikisha wenzetu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wanashirikishwa katika kila hatua katika ngazi ya Serikali ili kutuhakikishia kwamba haya tunayoyaleta huku ni yale ambayo vilevile upande wa pili wanayajua, na kwa kiasi kikubwa wameona yana mantiki na kwa hiyo, kuyaunga mkono na sehemu nyininge wametupa ushauri na tumeuzingatia vilevile kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

kuboresha baadhi ya maeneo tuliyokuwa tumeyapendekeza.

Kwa hiyo, kwa kweli hili ni jambo la msingi na sisi tunasema tutaendelea nalo kwa sababu limeimarisha sana ushirikiano katika hatua zetu zote za utunzi wa Sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tatu, chini ya uongozi wa Rais wetu alisema, ni vizuri kabla hamjaenda popote lazima mhakikishe Vyama vile Vikuu ambavyo vina Uwakilishi Bungeni mnakutana nao, mnazungumza hilo jambo kabla hamjkwenda kule ili mwone Vyama hivi kwa sababu ndio wadau wakubwa wana mawazo gani, wana mitazamo gani, wana mapendekezo gani; jambo ambalo tumelizingatia muda wote.

Kwa hiyo, hata katika Muswada huu mnaojadili, tulifanya hivyo hivyo na tunataka tuwashukuru sana viongozi wa Vyama vya Siasa vyote ambavyo tuna Uwakilishi hapa Bungeni kwa michango mingi na mizuri ambayo ilitolewa katika hatua hiyo ya awali ili kuhakikisha kwamba tunapokuja hapa hatuji tu na wazo la Chama kimoja eti kwa sababu tu ndio Chama kinachotawala, hapana. Sisi wote tuna kazi moja ya kuwasaidia Watanzania ili tuweze kupita katika hatua mbalimbali kwa pamoja. Baada ya pale sasa ndio tulikuwa tunakuja kwenye hatua ambayo tunakuja kwa Spika, tunawasilisha mawazo, Kamati zinakutana zinajadili, lakini hatimaye tunaingia kwenye hatua hii ambayo leo tupo.

Kwa hiyo, kwa kweli nimefarijika kwamba katika hatua zote hizi, yapo mambo mengi tumeyapata. Kama walivyosema wenzangu, nataka tuwahakikishie tu kwamba jitihada kubwa sana imefanyika kuweza kuyachukua yale ambayo tunaona yanaweza kuimarisha Muswada kwa lengo la kusaidia Taifa letu liweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, ushauri huu umekuja kwa sura nydingi na bado najua wakati Kamati tutapata ushauri zaidi na mapendekezo zaidi. Kwakuwa itakuwa ni wakati wa

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

majadiliano, basi kwa ujumla wetu nawaomba tu wote tutazame jambo hili kama ni letu sisi wote, siyo la Chama ambacho kipo madarakani na Serikali yake, hata kidogo! Huu ni Muswada kwa ajili yetu sisi wote na kwa hiyo, tuone namna nzuri ambayo tutaweza kuupitisha na kuufikisha katika hatua yake ya mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nipo hapa kwa sehemu kubwa kusisitiza tu baadhi ya maeneo machache sana, lakini kubwa ilikuwa ni kuwashukuruni kwa kazi nzuri mliyoifanya, na niwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wangu pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali amba muda wote wamejaribu kufanya kazi hii kwa umakini mkubwa sana; Kamati ya Mheshimiwa Mama Pindi Chana, wamefanya kazi kubwa muda wote pamoja na Wajumbe wake. Sina budi kusema ahsanteni sana kwa michango na ushauri mbalimbali amba mmeutoa.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri na hata Mwanasheria Mkuu wamegusia baadhi ya maeneo mengi na wametoa ufanuzi wa kitaalamu, mimi sitaingia kwenye masuala ya utaalamu, nataka tu nijaribu kuonesha maeneo ambayo nafikiri tuyaseme ili Watanzania wote waweze kuona nini hasa tunajaribu kufanya.

Kulikuwa na ushauri nadhani ultoka kwenye Kambi ya Upinzani, kwamba kwa uzito wa jambo hili na kwa hofu kwamba inawezekana muda uliobaki pengine siyo mkubwa, tunaweza tusifike mahali tunapotaka, tukaombwa kwamba, kwanini Muswada huu usisitishwe kwa sasa tupate muda zaidi, tuweze kuutafakari zaidi, na pengine kuujenga kwa namna ambayo ni nzuri zaidi?

Mheshimiwa Spika, ni jambo jema na hata kwenye masikio linalia vizuri tu. Lakini mimi nataka niwasih sana, kazi ambayo mmekwishaifanya mpaka sasa ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Tume ilipozunguka nchi nzima kukusanya maoni yale na hatimaye kuja na rasimu ile ya kwanza, tukaondoka tukaenda kwenye Mabaraza ya Kata

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

kazi imefanya kubwa, tunasubiri rasimu ile ya pili ambayo ndiyo tutakuja kuifanya kazi sasa kwenye Bunge letu. Ni hatua shirikishi, ni hatua pana imewapa Watanzania upeo mkubwa sana wa ushiriki kwa kadri inavyowezekana. Katika hatua hii kazi tulionayo sisi ni kujitahidi kuhakikisha Watanzania wengi waweze kupata ile fursa ya kushiriki katika kuamua juu ya Katiba ambayo sasa tunafikiria kuiandaa.

Mheshimiwa Spika, mimi nitakuwa mtu wa mwisho kusema ndiyo tuahirishe, kwa sababu kazi iliyofanyika ni kubwa na nzuri.

Waheshimiwa Wabunge, michango yenu hapa kwa sehemu kubwa ndiyo inawakilisha mawazo ya watu kwa kiasi kikubwa sana, ndiyo maana nasema kwa sehemu kubwa yale mliyosema mazito yote, Serikali hii imeyasikiliza na kwa sehemu kubwa imeyazingatia sana. Kwa hiyo, nadhani tusonge mbele.

Waheshimiwa Wabunge, msisahau wakati wa kampeni jambo hili lilijitokeza na mkatupa matumaini ya kwamba mkiingia madarakani ndani ya siku 100 tu tutapata Katiba mpya. Sasa wote mmeona ugumu wake. Ndio! Mmeona ugumu wake, ndiyo maana lazima kwa kweli hatua kwa hatua tujaribu kushirikiana kuona kitu gani tutakifanya kwa maslahi yetu sisi wote ili tuweze kufika hatua ambayo inatakiwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa niwaombe twende mbele, tutaenda tunazungumza na bado kazi ni kubwa Bunge la Katiba litakutana, mtakuwa na nafasi kubwa sana kabla hata hatujafikia kwenye hatua hiyo nytingine. Kwa hiyo, tuna kila sababu kwa kweli ya kusema hapa tulipo sio pabaya twende ili tuweze kufika hadi mwisho.

Mheshimiwa Spika, Sasa kitu kimoja ambacho nimeona nikiseme hapa, ni hili ambalo Mwanasheria Mkuu wa Serikali amelieleza kwamba kutokuwepo kwa kipengele ndani ya Katiba kinachoruhusu uwepo wa Kura ya Maoni ni kasoro kubwa na haiwezi hata kidogo ikarekebishika. Katika

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

hatua mbalimbali hata kwenye *cabinet* tulizungumza sana jambo hili katika kujitahidi kujiridhisha kuona kama jambo hili tukienda nalo hivi tutakuwa tunakiuka taratibu au tunavunja Sheria, tukapata hata ushauri kutoka nje yetu sisi wenyewe lakini kwa kweli kauli moja tulikubalina kwamba hapana. Jambo hili kwa Katiba ilivyo, bado tuna mamlaka kama Bunge kuweza kutunga Sheria kwa ajili yoyote ile au kwa madhumuni yoyote yale na ndiyo maana tukaridhika kwamba sisi nafikiri tupo salama tukienda na jambo hili.

Kwa hiyo, nataka niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge lakini kubwa zaidi Watanzania, kwamba jambo hili lilihofanywa na Bunge letu Tukufu ni jambo sahihi tu, na limezingatia taratibu za nchi kwa kiasi ambacho tuliweza kushauriwa hadi hapa tulipofika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Zanzibar, leo asubuhi nimefarijika maana nimeona maeleza yamejitokeza hapa Mheshimiwa Vuai ameeleza lakini walikuwepo vile vile ambaao wamelieleza vizuri. Linalosemwa ni jambo zuri tu na lina uzito wake. Tatizo nililopata mimi ni kama Bunge hili tuna mamlaka ya kuweza kusema liwe hivi au lisiwe hivi, kwa jambo ambalo linasimamiwa na Baraza la Wakilishi, ilikuwa ndiyo tatizo langu kubwa sana. Lakini nashukuru tu kwamba wengi nadhani baada ya mjadala ule mzuri na mawazo mbalimbali yaliyotoka inaelekea wengi tunakubaliana kwamba hata kama hoja ipo haliwezi kuwa ni jambo la Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, isipokuwa tuombe kwa uzito wake na kwa kadri watavyoona inafaa, basi Baraza la Wawakilishi wanaweza wakalichukuwa jambo hilo wakalifanya kazi na hatimaye wakaona nini kinafaa kwa mazingira yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini hili wakati linazungumzwa nilikuwa nalitazama hasa kwa maana ya uchaguzi au chaguzi ambazo zimekuwa zikifanyika kila baada ya miaka mitano ama wakati wa kupiga kura, chaguzi ndogo na kadhalika. Lakini kwa maana ya Kura ya Maoni, nimelifikiria sana na mimi nashukuru sana wenzangu waliotangulia wamelieleza vizuri.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Mheshimiwa Spika, Daftari la kudumu la Tume kwa sasa lina orodha ya Watanzania wa Bara wanaoishi Zanzibar, lakini hawawez i kupiga kura kwenye uchaguzi ule wa ndani. Lakini kwenye Daftari hili wapo. Lakini wapo vile vile Wanzazibari ambao hawajaweza kukidhi masharti ya ukaazi kwa mujibu wa Sheria za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Hawa nao wapo kwenye hili daftari. Katika chaguzi zilizopita hawa wamekuwa wakipiga kura, lakini kwa kumchagua Rais wa Jamhuri na Wabunge wale wanaohusiana na Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, rai iliyokuwa inatolewa ukiitizama kwa sura hii, mimi kwangu inanipunguzia hofu sana, kwa sababu hawa wanaweza bado kwa kutumia daftari hili hili wakapewa fursa na wakaweza kupiga Kura ya Maoni bila tatizo kwa sababu ni kitu ambacho kinatokana na Sheria hii ya sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niliwaomba sana wenzangu hapa kwamba pengine hili ni la kutazama tu, tuje na muundo gani, pendekezo la namna gani litakaloweza kuwabeba hawa na wala mimi sipati taabu, wakahesabiwe Zanzibar, sawa sawa tu. Kwa sababu halina tatizo kwangu hata kidogo! Kwa sababu ni Kura ya Maoni ndiyo tunajaribu kujengea hoja na tungependa watu wengi washiriki katika jambo hili kwa kadri itakavyowezekana.

Kwa hiyo, naamini wenzangu watakapokuwa wanawasilisha jambo hili watakuwa bila shaka wameliweka kwa sura ambayo itasaidia sana kuweza kuleta sura nzuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lilikuwepo jambo lingine ambalo ni uboreshaji wa daftari la kudumu. Sasa hili linatokana na hofu, hofu ambayo hata asubuhi nilijaribu kusema wakati nimeulizwa swalii, ni ya kweli, ni *genuine!* Kwa sababu wote tungependa jambo hili lifanyike vizuri kwa maslahi ya Taifa letu. Lakini kama nilivyo sema, nataka niwahakikishie Watanzania kwamba Serikali kwa jambo hili tumedhamiria tena kwa dhati kabisa kufanya kila litakaloweze kana ili

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

kuhakikisha kwamba uboreshaji wa Daftari unafanyika ili wale wote wenye stahili au wenye haki ya kuandikishwa waweze kuandikishwa na waweze kuja kushiriki katika kupiga Kura ya Maoni bila tatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hoja hapa ilikuwa ya kibajeti tu, lakini tunavyozungumza hapa tayari tumeshatoa kiasi cha fedha, ambazo kwa kweli kwa mahitaji ya awali zinatosheleza kuanza zoezi hilo, liweze kufanyika bila tatizo. Kwa hiyo, nataka niwahikishie tu kwamba tutafanya kila linalowezekana ili tuhakikishe kwamba jambo hili linakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, kulikuwepo na hoja vile vile ya utoaji wa elimu kwa umma. Jambo hili nalo ni kubwa. Nataka nikubaliane nanyi wote mlionchangia eneo hili kwa msisitizo mkubwa sana kwamba ni vizuri jambo hili likapewa nafasi kubwa, elimu ya kutosha itolewe na watu wote waweze kufikiwa na hiyo elimu kabla ya siku ile tutakapokuwa tunapiga hiyo Kura ya Maoni.

Nataka niseme tu kwamba kwa mujibu wa mapendekezo yaliyomo kwenye Muswada huu mtakuwa namna tulivyojitalidi kujaribu kupanga mawazo, namna elimu itakavyotolewa na tutatumia namna nyingine mbalimbali ili mradi tuhakikishe kwamba watu wanapata elimu ya kutosha ili tuweze kuwa na uhakika kwamba jambo hili linafanyika vizuri, na kila mlengwa anafikiwa kwa wakati ili aweze kutumia hiyo haki yake vizuri kwa kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili nalo nimeona tu niligusie kutokana na uzito wake ili wote hapa tuweze kuja kwamba sisi wenzenu na sisi tunalipa nafasi kubwa ili tuhakikishe kwamba linafanyika vizuri. Lakini ilikuwepo vile vile hoja nyingine nayo ni nzito vile vile juu ya Tume huru, kwa mawazo kwamba tunamashaka na Tume hii. Ni hofu ya kawaida mimi sidhani kama katika mazingira mnayokuwa nayo na hasa mnapokuwa kwenye chaguzi hizi, hasa zile chaguzi ambazo zinatafuta kushika dola, jambo hili huwezi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

kulipuuza hata kidogo, lazima usikilize kwa makini uone tatizo lipo wapi halafu hatimaye uweze kuona unafanyaje ili tuweze kuwa na angalau mfumo ambao unawapa watu kidogo hali ya kutulia na kuamini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kweli kwa maoni yangu lakini hata wenzangu Serikalini tumejaribu kulitazama sana jambo hili, pamoja na hofu iliopo, lakini mtaona kwenye Sheria hii au Muswada huu, tumejaribu vile vile kuweka mambo ambayo tunafikiri yanaweza yakasaidia kutupa amani kutupa uhakika kwamba jambo hili litawezekana na litasimamiwa vizuri. Utaona karibu kila hatua tumejaribu kuhakikisha kwamba vyama vitakuwa na Mawakala wake muda wote ili kuhakikisha kwamba yote yatakayokuwa yanatendeka yanakuwa wazi na kila Chama kinaridhika kwamba kina mtu au watu ambao wapo pale kama Wawakilishi kwa ajili ya jambo hili kubwa.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile Tume hizi, sijui lakini Tume hizi mkiziangalia mara zote Rais amejitahidi sana kuweka watu ambao wanaheshima zao, watu adilifu wenye uzoefu na upeo mkubwa na mara nyangi amekuwa akilenga sana kundi la Majaji. Kwanini Majaji? Majaji kwasababu kwa nafasi zao, kwa kazi zao, ni kazi ambayo ni ya kutenda haki. Kwa hiyo, wamejengewa mazingira haya makusudi kabisa ili kuhakikisha kwamba jambo hili linakuwa angalau linatoa amani kwa kadri itakavyowekana.

Kwa hiyo Mimi nataka niwaombe tu wenzetu na niwaombe Watanzania vile vile kwamba katika hatua hii na kwa namna ambayo mfumo huu wa Muswada ulivyo jambo hili naamini kabisa tunaweza tukaenda nalo vizuri litasimamiwa vizuri na tuna hakika kabisa kwamba matokeo yake yatawaridhisha nadhani Watanzania wengi ikiwa ni pamoja na Wabunge waliopo hapa kutoka Vyama mbalimbali.

Kwa hiyo, niwasihhi sana tulikubali, twende nalo, letu wote, kama kutakuwa na kasoro za hapa na pale, tutaambizana na wale Wahusika wote wataambia kwa

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

sababu *systems* zote hakuna ambayo ipo 100% perfect hakuna. Kwa hiyo, hapa na pale zinaweza kutokea hitilafu, kazi yetu ni kuona namna ya kuzirekebisha mara moja.

Mheshimia Spika, kubwa zaidi sasa ambalo nataka kulisema kwa ujumla wake, hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mimi nakushukuru sana kwasadabu umelieleza mara nyingi sana kwamba tunapokuwa na Miswada mizito hii, tuone kama kuna namna ya kuweza kuwa na maridhiano kwenye mambo ya msingi. Tusiingize sana uchama chama hivi kwa mambo ambayo yanahitaji kuamuliwa kimsingi. Kwa sababu tukifanya hili, hili ndilo litakalowapa Watanzania wanaotuona, wanaotusikiliza imani kwamba kweli tunafikiri Bunge sasa lipo pale kwa ajili yetu na siyo kwa ajili ya kundi fulani au Chama fulani kwa kadiri itakavyowezekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nisisitize tu kwamba katika mjadala huu ambao unaelekea mwishoni, kwa ujumla wake naweza nikasema pamoja na mengine yote ambayo yanaweza yalikuwa yalijitokeza hisia nyingine za kurushiana na nini, lakini kwa ujumla, mimi nilivyowatazama, nilivyowasikiliza, michango mingi imejaribu kusaidia tuweze kwenda mbele kama Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa vijembe wakati mwingine vinakuwepo, wakati mwingine navyo tuvikubali ndiyo sehemu zenyewe za majukumu ya Mabunge haya lakini tusivientertain sana, tusivifanye ndiyo vya msingi kuliko misingi yenewe ambayo inatuweka Bungeni kwa ajili ya majadiliano mazito tunapokuwa na mambo makubwa kama haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, nataka kuwasihhi, huko tunapokwenda, tuombe sana Mawaziri huko upande wa Serikali na upande wa Bunge vile vile tuone kwamba tunaweza tukafika mahali pengine tunapokuwa na jambo kubwa kama hili, licha ya viongozi wetu wa vyama kukutana na kuzungumza na kubadilishana mawazo badala ya kila

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

chama kujifungia. Tumelifikiria sana hili. Tuone kama tunaweza kufika mahali tukawa na kikundi cha Wabunge, lakini kutoka vyama vyote, tunakaa pamoja, tuna jaribu kuzungumza maudhui ya Muswada, lakini kwa lengo la kutaka twende mbele. Tukizungumza kwa mtazamo mmoja wa kutaka kutengeneza kitu kizuri, mimi naamini tunaweza kabisa. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa nini? Ni kwa sababu, ni kweli tuna utaratibu wa Kamati na ni kweli vile vile tunapata fursa kwenye *party caucus* tunazungumza, lakini bado nafikiri hatujafika mahali nikaona kwamba tumefikia hatua nzuri ya kuwa na mfumo wa maridhiano hata kama ni ya jumla kwenye mambo yale ya msingi kabla hatujaja hapa Bungeni. Pengine ni jambo tulitazame kwa pamoja, tuone katika hatua gani tunaweza na katika mazingira gani ili tusiache tu kwamba hilli ni jambo la viongozi tu, hapana na kwamba tungoje mpaka tuanze kurushiana maneno ndani ya Bunge, hapana. Tupate *forum*, tupate kikao kinachotuweka sisi wote. Sisi sote ni Watanzania wale wale na kesho na kesho kutwa Chama fulani kinaweza kuwa madarakani, kwa hiyo, hili litatusaidia sana ili tuweze kufanya kazi zetu, zionekana za maana na ziwe nyepesi zaidi. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema tangu mwanzo, nia yangu kwa kweli ilikuwa kuwashukuruni, kazi imekuwa ni nzuri kwa ujumla wake.

Mimi binafsi nimeridhika sana hasa kwa sababu tumeendelea kufanya kazi mpaka dakika hii. Lakini kubwa zaidi ilikuwa kwa kweli ni kutaka kutoa msisitizo kwa baadhi ya maeneo ambayo yatatupa fursa kwa sababu tutaingia kwenye hatua inayofuata ili tuone tutakavyokamilisha huu Muswada vizuri, baada ya pale basi tuone tunafanyaje kwa ajili ya kazi iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, katika kumalizia nataka tu niseme kwamba Tume hii ilimpoteza kiongozi mmoja wao mahiri sana, nafikiri wote mnafamu Dkt. Mvungi na tuko baadhi yenu wachache tulipata nafasi ya kwenda kushiriki katika mazishi

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

yake. Kwa hiyo, nilifikiri ni wakati mzuri wa kuwapa pole kwenye Tume, lakini vile vile familia, lakini Watanzania kwa ujumla kwa sababu alikuwa na mchango mkubwa sana katika Tume ile katika kipindi chake chote.

Kwa hiyo, tumempoteza, lakini ameacha kazi nzuri imeshafanya na hatua nzuri sana imeshafikiwa. Imani yangu ni kwamba Mwenyezi Mungu atampokea mahali pema Peponi na huko baadaye wengine tutakwenda kumuunga mkono, kwa sababu ni safari tu kila mmoja lazima aende huko, lakini imani yangu ni kwamba alichotuachia kitakuwa kimetusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, basi naomba kumalizia kurejea kukushukuru sana wewe, kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri na niwaombe tumalizie kazi iliyobaki vizuri kwa sababu ndiyo kazi iliyotuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa
kwa Mara ya Pili)*

SPIKA: Hoja hii imeungwa mkono. Katibu, tuendeleo na hatua nyininge.

KAMATI YA BUNGE ZIMA

**Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni wa
Mwaka 2013 (*The Referendum Bill, 2013*)**

Kifungu cha 1

Kifungu cha 2

Kifungu cha 3

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON.
MIZENGO K. PINDA, THE PRIME MINISTER AT THE
SECOND READING OF A BILL ENTITLED**
“THE REFERENDUM ACT, 2013”

(Made under S.O. 86(10)(b))

The Bill entitled “The Referendum Act, 2013” is amended:

A: In Clause 3 by-

(a) deleting the definition of the terms “polling station” and “proposed Constitution” and substituting for them the following:

“polling station” means a room or place designated and equipped for the casting of vote by a voter at a referendum;”

“proposed Constitution” means an enactment of the Constituent Assembly which is the subject of the referendum”

(b) deleting the word “Commission” appearing in the definition of the term “referendum campaign period” and substituting for it the phrase “President pursuant to section 4;

(c) adding in its alphabetical order the following definition:

“referendum period” means a referendum period specified by the President pursuant to section 4;”

Dodoma,

....., 2013

M.K.P.P

WM

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON JOHN
JOHN MNYIKA MEMBER OF PARLIAMENT FOR UBUNGO
CONSTITUENCY AT THE SECOND READING FOR THE BILL
ENTITLED THE REFERENDUM ACT, 2013

Made under standing order 86(11) and 88(2)

A bill entitled “**THE REFERENDUM ACT, 2013**” is amended as follows:

A: In Clause 3; after interpretation of ‘referendum campaign period’ add new interpretation of “referendum period” means the period beginning on the day on which the text of the referendum question is published and ending on the polling day of the referendum.

.....

JOHN JOHN MNYIKA (MP)

UBUNGO CONSTITUENCY

04.12.2013

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Katika kifungu hiki nilipata wasaa wa kukutana na Kamati ya Bunge pamoja na Serikali na mapendekezo yangu yallikuwa ni kuweka tafsiri ya neno “*referendum period*” kwa maana ya “kipindi cha Kura ya Maoni” na kwenye mazungumzo kwenye Kamati, Serikali ikakubali kwamba katika jedwali la marekebisho italeta kifungu ambacho kitaainisha tafsiri ya neno “*referendum period*.” Nimepitia jedwali la Serikali na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN J. MNYIKA]

kwa kuwa Serikali imependekeza marekebisho kwenye kifungu hiki, cha kubeba hiyo tafsiri, nakubaliana na mapendekezo yaliyowasilishwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

SPIKA: ahsante. Mheshimiwa Wenje.

SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON EZEKIA DIBOGO WENJE MEMBER OF PARLIAMENT FOR NYAMAGANA CONSTITUENCY AT THE SECOND READING FOR THE BILL ENTITLED THE REFERENDUM ACT, 2013

Made under standing order 86(11) and 88(2)

A bill entitled "The Referendum Act, 2013" is amended as follows:

- A. In clause 3 by deleting the definition of the word "commission" and replacing it by the following new definition, the independent referendum commission, whose members shall be appointed by the president of Tanzania from the list nominated by Academic bodies, law society of Tanganyika, Zanzibar law society, Representative from the judiciary, Tanzania human rights commission, member representing business councils, non-governmental organizations.

.....
Hon Ezekia Dibogo Wenje(MP)

NYAMAGANA CONSTITUENCY

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilipeleka mapendekezo ya kutoa *definition* mpya, maana mpya ya neno "Commission."

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya niliyoyatoa na ninashukuru kwamba hata Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyowasilisha hapa, aliona ni kweli kwamba kuna haja katika mchakato wa kutengeneza Katiba tuwe na maridhiano, lakini pia kuwe na haja ya kuaminiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana ni ukweli usiopingika kwamba mimi Wenje binafsi pamoja na Watanzania wengine wapo; *may be humu hawamo amba* hawaamini hii Tume ya Uchaguzi. Ndiyo maana nilileta mapendekezo ya kutaka badala ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Zanzibar ya Uchaguzi kusimamia hili suala la *referendum*, tuwe na kitu kinaitwa "*Independent Referendum Commission*."

Kwenye jedwali langu nimetoa mpaka mapendekezo ni namna gani hawa Wajumbe wanaweza wakapatikana kwa sababu kwenye Kamati tulibishana sana na hoja ilikuwa kwamba kwa sasa hatuna muda wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya, hayachukui muda mrefu kwa sababu nimetoa na *proposal* namna gani hawa Wajumbe wanaweza wakapatikana, ili iundwe Tume ambayo itakuwa huru kwa ajili ya *referendum* tu. Isisimamiwe na hii Tume ya Uchaguzi ambayo Kimsingi sisi tulio wengi hatuiamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba haya mapendekezo niliyoleta, ni kweli tulijadiliana kwenye Kamati, lakini sikuridhika na maamuzi yaliyotoka kwenye Kamati, ndiyo maana bado nimeyaleta hapa kwenu. Ni kwa nia njema tu kwamba twende kwenye *process* hii tukiwa tunaaminiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba haya marekebisho niliyoleta yakubaliwe.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Mbona hatujasikia umesemaje? Maana yake ulikuwa una-*justify*...

MHE. EZEKIA D. WENJE: *Okay.*

Mheshimiwa mwenyekiti, *new definition* ninayopendekeza ni kwamba, maana ya "Commission" jinsi ilivyopendekezwa kwenye Muswada iondolewe, halafu iwe replaced, sasa isomeke hivi: "*the Independent Commission*". Sasa itakuwa na maana ifuatayo: "*the Independent Referendum Commission whose members shall be appointed by the President of Tanzania from the list nominated by Academic Bodies, Law Society of Tanganyika, Zanzibar Law Society, Representative from the judiciary, Tanzania Human Rights Commission, member representing Business Councils, Non-governmental organizations.*"

Kwa hiyo, hayo ndiyo marekebisho ninayotoa kwenye *definition* kwamba isomeke hivyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwepo kwenye Kamati wakati Mheshimiwa Wenje anawasilisha mapendekezo yake. Ni kweli kwamba kuna kutokuaminiana kwenye mchakato wa Katiba. Kuaminiana huku pamoja na ufanuzi uliotolewa kwamba imani hujenga imani, hakuwezi kuzibwa bila kuwa na mazingira ya kikatiba na kisheria ya kuweka msingi ya kuaminiana huko.

Sasa kwenye ufanuzi wa Serikali, wametumia ibara ya 78 ya Katiba ya kwamba Tume inaweza kupewa kazi nyingine kuhalalisha jambo hili. Kwenye ufanuzi wa Serikali wametumia kisingizio cha kwamba kwa kuwa pendekezo la Mheshimiwa Wenje liko kwenye upande wa tafsiri na haliko kwenye vifungu vinavyohusika, basi pendekezo hili likataliwe. Lakini tuliwaeleza Serikali, naomba kuwaeleza tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha msingi ni nini hapa? Cha msingi ni kujenga kuwa na Tume huru kwa ajili ya

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. JOHN J. MNYIKA]

kusimamia Kura hii ya Maoni. Jambo hilo linawezekana kabisa kama tukiamua tu kwa dhamira ya dhati kujenga kuaminiana.

Sasa nisipoteze muda kwa sababu hoja ambazo zilipelekwa kwenye Kamati Serikali inazifahamu, kama Serikali haikubaliani na mapendekezo ya Mheshimiwa Wenje, Serikali iletu mapendekezo ambayo yatafanya wadau tuwe na imani na chombo ambacho kitakwenda kuisimamia Kura ya Maoni. Hili ndilo jambo la msingi ambalo tunaomba Serikali iridhie na kufanya marekebisho yanayostahili. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Serukamba. Nyie wengine ni dakika tatu tatu.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa iko hoja inajengwa ya kuleta kuaminiana. Ukiona mtu anaongea habari ya kuaminiana, maana yake yeye ndio haamini.

MBUNGE FULANI: Yeye sio mwaminifu!

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Ni kwamba yeye sio mwaminifu, analo tatizo ambalo ni vizuri lingesemwa, kuliko jambo ambalo halisemwi.

Tunachosema, Tume hii ya Uchaguzi ndiyo Tume ambayo wote humu ndani imetuleta hapa ndani, na ndiyo ilitangaza ushindi wetu, ndiyo imekuwa inafanya kazi. Leo Tume hii tunaipa kazi ya kwenda kuandikisha watu wapya, mbona hatui-*doubt* kwenye hili? Mbona hatusemi Tume hii isiende kufanya *registration?* Lakini kwenye *registration*, sawa; kwenye kura, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Serikali, tuendelee na mawazo ya Serikali ili twende tukafanye hii kazi ya kutengeneza Katiba.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kafulila.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati ana-*wind up* pamoja na wewe mwenyewe umekuwa ukisitisiza suala zima la kuaminiana, na kwamba tuaminiane kwa sababu jambo hili tunalolifanya, siyo kwa ajili ya Chama fulani ambacho leo kipo madarakani, kwa sababu kuna siku nyingine kitakuwa kiko kingine. Kwa hiyo, tutengeneze misingi zaidi kuliko siasa ambazo zitakuwa zinajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika wa tafiti mbalimbali, *academicians*, wataalam mbalimbali wa masuala ya haki za binadamu wamesema kwamba Tume ya Uchaguzi ya Tanzania siyo huru. Moja ya sababu ya madai ya Katiba mpya ni ili kupata Tume huru ya Uchaguzi. Yaani hii Katiba mpya tunayoidai, moja ya sababu yake ni ili kupata Tume huru ya Uchaguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo mifano ya dhahiri, hata nchi kama ya Zimbabwe, nchi ambayo kidemokrasia tunaweza kuihesabu kwamba ilikuwa nyuma sana, lakini walipokwenda kwenye mchakato wa Katiba mpya walitengeneza kwanza Tume huru ya Uchaguzi ili isimamie mchakato wa Katiba mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado nasisitiza kwamba ni suala la dhamira tu kwamba Serikali itapoteza nini ikiruhusu Tume huru? Mchakato wa Katiba siyo kwa ajili ya uchaguzi. Suala la kwamba tunachelewa, hatufanyi Katiba hii kwa ajili ya uchaguzi, ni kwa ajili ya nchi. Tusiharakishe!

MWENYEKITI: Wanaochangia ni dakika tatu. Mwenye hoja atachangia dakika tano. Kwa sababu mngekuwa mnaingia kwenye *point*, nini siyo huru au kitu gani siyo huru, mngekuwa mnatumia muda vizuri. Sijaona msemaji mwingine.

Mheshimiwa Assumpta, dakika tatu. Mkiongea maneno yasiyokuwa yenyewe, basi mnapoteza muda.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilikuwa napata wasiwasi sana kwa namna ambavyo ilikuwa inaelezwa Tume huru. Hivi ni nani ambaye atachaguliwa na nani ambaye hawezi kutii mamlaka iliyopo katika nchi hii? Anatoka wapi? Huyo mtu huru anayetoka nje; Uganda, Kenya au wapi? Si atatoka katikati ya Watanzania hawa hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua mtu ye yeyote atakayechaguliwa anayeipenda nchi hii, hivi kura ya "Ndio" na "Hapana," mtu anaficha "Ndio" anaweka "Hapana"! Mimi sioni kwa nini tunahangaika kurudia neno huru, huru, huru; hakuna mtu aliye kifungoni. Watu wote wako huru na ninaamini kabisa, hii Tume inaweza kufanya watu wakapatikana vizuri. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khatib.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami namuunga mkono moja kwa moja Mheshimiwa Wenje katika hili.

Mheshimiwa Mwehyekiti, matatizo mengi ya chaguzi zetu katika nchi yetu yamesababishwa na Tume hizi. Mheshimiwa Waziri Mkuu ametamka hapa kwamba ni vizuri kujenga mazingira ya kusikilizana ili jambo hili lifikie tamati njema. Katika kusikilizana, mojawapo ni hata ninyi wengi kusikiliza mawazo ya sisi wachache. Siyo kwamba sisi tuko tayari kukaidi hata zuri ambalo linatoka upande huo, wakati sisi tunakubali hayo, hata nyie mkubaliane na haya ambayo tunapendekeza.

Mheshimiwa Mwehyekiti, Tume hizi hasa ZEC zimehusika katika machafuko ya mara kwa mara katika chaguzi za Zanzibar. Siyo siri, tumeshuhudia watu wamepoteza roho zao kwa sababu ya Tume ile ya Zanzibar. Leo tunaporudi kusimamia jambo hili, ni lazima watafuata matakwa ya waliowateua. Tunaposema tuunge mkono kupata Tume huru, tuachane na hizi za chaguzi za miaka mitano, ina maana kwamba tunataka kuwachagulia

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. KHATIB SAID HAJI]

Watananzania kitu kitakachodumu miaka 50. Kwa hiyo, nakubaliana na naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Wenje.

MWENYEKITI: Dakika ni tatu. Msome hoja ya Mheshimiwa Wenje, msiseme tu, msome hoja yake. Maana sasa tunaanza kurudisha Muswada huko! Msome hoja ya Mheshimiwa Wenje ndiyo tunayoizungumzia. Mheshimiwa Anna Abdallah.

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Mimi nadhani kama ni suala tunalosema kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema tujenge kuaminiana, kuaminiana siyo lazima kuwe kwa upande mmoja kuamini wengine, lazima tuaminiane sote kwa pamoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili mimi nasema ingekuwa tunakwenda kwenye uchaguzi wa Ubunge au Urais tungesema tunataka Tume hiyo mpya. Lakini hili la "Ndiyo" au "Hapana," kwa kweli tutakuwa hatufanyi haki. Sisi wote hapa hata kama kulikuwa na matatizo, wote tumeingizwa humu ndani na hii Tume. Sasa Tume ingekuwa na upendeleo kusingekuwa na watu wengi upande wa *opposition* hata kidogo! Kwa hiyo, nasema, na hii ya kwamba upande wa CCM kuna watu wengi, ndiyo matakwa ya wapiga kura. (*Makofii*)

Kwa hiyo, naomba sana, hili lisitupotezee muda. Tuiachie hii Tume imalize, imalizane nao wote. Nafikiri hata huko tunakokwenda kwenye Katiba mpya hawatakuwepo, tutafanya kitu kipyta. Hebu tumalize hili. Mimi nashauri tulibakize kama lilivyo. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anna Kilango.

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Mwenyekiti, *actually*, kama mama Mheshimiwa Anna Abdallah amezungumza nilichotaka kuzungumza, lakini niongezee

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. ANNE K. MALECELÀ]

kidogo. Sasa hivi tunavyozungumza, wananchi wanatuangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mgawanyiko uko. Kwa Chama ambacho kimepata ridhaa ya wananchi kukamata Serikali, wanassema Tume iko sawa. Hawa wenzetu ambaao hawakukamata Serikali ndiyo wanaokataa Tume. Lakini kama alivyosema mama, mbona mmeingia wengi sana kipindi hiki kuliko kipindi kilichopita? Kwa hiyo, Tume hii ilikuwa huru ndiyo maana Wabunge wengi sana mmeingia. (Makofî)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu sasa tuamue kwamba hili jambo tupite nalo, kwa sababu "Ndiyo" na "Hapana" ile, na Mawakala watakuwepo, na watatoka kwenye Vyama vyote, hakutakuwa na kitu ambacho ni cha ajabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tusiwafanye wananchi wakatuona kwamba kila wakati tunapingana kwenye mambo madogo. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ukiangalia mapendekezo haya yanayowasilishwa na Mheshimiwa Wenje, kuwekwa kwenye kifungu cha tafsiri wakati kwenye Bodi yenyewe ya Sheria bado hujaweka, utakuwa kwanza umesha-*disturb*. (Makofî)

Pili, bado nirudie, hofu yao ya uhuru, ukiangalia katika ibara 74(11) ya Katiba yetu, inaeleza bayana kabisa kwamba Tume itakuwa huru. Haitapokea maelekezo kutoka kwa mtu yejote, Taasisi yoyote wala Chama chochote cha kisiasa. Lakini pia ukiangalia katika ibara ya 8 (4) ya Sheria ya Kura ya Maoni, inaeleza kabisa kwamba Afisa wa Kura ya Maoni hatafanya kazi kwa kutoa upendeleo wa aina yoyote.

Tatu, niseme tu kwamba nchi mbalimbali zimekuwa zikija kujifunza kutoka kwenye Tume hizi. Sasa lazima mjiulize,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA]

kuna nini? Sina haja ya kurudia mengine mengi ambayo mmesema kuhusu uwingi wenu mlivyoingia humu ndani.

Nne, niseme tu kwamba Zanzibar wenzetu walishapitia mchakato wa Kura ya Maoni. Tume hii hii ya Uchaguzi wa Zanzibar ilishiriki katika mchakato huo. Wote tumeona mema mazuri waliyoyapata, wameweza kufikia umoja wa Serikali ya Kitaifa kupitia Tume hii ya Uchaguzi ya Zanzibar. Ukiangalia katika tafsiri hii ya Tume ya Uchaguzi, na ya Zanzibar imo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tuwape nafasi, washirikiane na Tume ya Uchaguzi ya Taifa, wasogeze jahazi hili mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Wenje.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza ieleweke kwamba: kwanza, idadi ya Wabunge humu ndani ambao hatutokani na Chama Tawala kwamba tumekuwa wengi, siyo kiwango halisi cha kupima uhuru wa Tume ya Uchaguzi. *That is very crazy argument!* (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, hii Tume ya Uchaguzi, NEC walipokwenda kutoa maoni, kwenye Tume ya Katiba, wao wenyewe katika mapendekezo waliyosema, walikiri kwamba hawako huru. Walisema! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, hii Kura ya Maoni ya Katiba ni muhimu kuliko kura ya uchaguzi. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Kabisa!

MHE. EZEKIA D. WENJE: Tunatengeneza Katiba inayokwenda kupeleka Tanzania miaka 50 inayokuja. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. EZEKIA D. WENJE]

Kingine hii *technicality* inayosemekana kwamba nimeweka kwenye *definition; is true!* Once ukishabadiilisha *definition, then technically* popote pale ambapo hili neno linakwenda *ku-appear* humo ndani linabadilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepewa *model* hapa na Mheshimiwa Waziri. Huwezi ukatupa *model* ya Liberia. *Liberia can never be a model to Tanzania.* Kuna nchi nyngi, hata Mheshimiwa Kafulila katoa mfano wa Zimbabwe! *Liberia can never be our model.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa suala la Kura ya Maoni, kwa umuhimu wa Katiba kwa Tanzania, kwa umuhimu wa muda ambao Katiba itakaa, naomba hili lipite. Tatizo liko wapi?

MBUNGE FULANI: Hakuna haja!

MHE. EZEKIA D. WENJE: Tukiwa na *Independent Commission* na nimetengeneza, hawa wote watakuwa appointed na *President* baada ya kuwa *nominated* kutoka kwenye hizi Taasisi ambazo nimeelekeza kwenye hii *amendment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, naomba hii ipite. Hii ni kwa maslahi ya Taifa, siyo kwa ajili yangu Wenje, au kwa ajili ya Chama changu au kwa ajili ya Wapinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hii ipite.

MWENYEKITI: Kwanza mimi mwenyekiti, sijaelewa. Kilichokuwa siyo huru ni nini? Kama ni *appointment* na huwa hapa mnasema *President; what is not huru?* Ni nini? Mngetusaidia hapo tu labda tutaelewa. Nini kisichokuwa huru?

MBUNGE FULANI: Tume ya Uchaguzi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachozungumzia katika hoja yangu ni kwamba Tume ya Uchaguzi yenyewe, siyo huru, *regardless* mfumo wa *appointment* ni kwamba Tume yenyewe siyo huru. Hata hii Tume yenyewe imewahi kukiri mbele ya Tume ya Warioba iliyokuwa inakusanya maoni ya Watanzania kwamba yenyewe siyo huru. Vile vile kuna *research* zimefanyika hapa, Waheshimiwa Wabunge wengine wamesema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sababu hii Tume siyo huru...

MWENYEKITI: Ungesema kidogo ni nini hicho kinachofanya isiwe huru tukuelewe. Maana hapa ni *appointment*, kama unaishia *President*, na ile nyingine ni *President*. Sasa, ni nini hasa unachokizungumza? Kama tunataka kukuunga mkono, lakini *on which one?* Hebu zungumza Mheshimiwa Wenje.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, namba moja, Wajumbe peke yake wa hii Tume ya *NEC* walipo leo wanakuwa ni *self appointee* ya *President* moja kwa moja bila *check and balance*. Sasa mapendeleko tunayoleta hapa sasa hivi ni kwamba ipatikane Tume huru ambayo Wajumbe wake watakuwa *nominated* kutoka kwenye Taasisi mbalimbali halafu *from the nomination*, wanakuwa *appointed* na *President*. Hii angalau inaleta *checks and balance* na angalau inaleta *some confidence*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *this is the concept*. Kama Tume ya Katiba ilivyonanii. *This is the point!*

MWENYEKITI: Naomba tupige kura.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Mapendeleko ya Mheshimiwa Ezekeia D. Wenje
yaliamuliwa na kukataliwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 4

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON.
MIZENGO K. PINDA, THE PRIME MINISTER AT THE
SECOND READING OF A BILL ENTITLED
“THE REFERENDUM ACT, 2013”**

(Made under S.O. 86(10)(b)

The Bill entitled “The Referendum Act, 2013” is amended:

- B:** In Clause 4 by deleting the phrase “format set out in Form No.1 of” appearing in subclause (2) and substituting for it the phrase “Form set out in;”

Dodoma,
....., 2013

M.K.P.P
WM

SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON EZEKIA
DIBOGO WENJE MEMBER OF PARLIAMENT FOR NYAMAGANA
CONSTITUENCY AT THE SECOND READING FOR THE BILL
ENTITLED THE REFERENDUM ACT, 2013

Made under standing order 86(11) and 88(2)

A bill entitled "The Referendum Act, 2013" is amended as follows:

- B. In clause 4(1) by adding the following new words immediately before the word commission "the independent referendum"

.....
Hon Ezekia Dibogo Wenje(MP)

MHE. EZEKIEL D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho Kifungu cha 4, *definitely* kinatokana na Kifungu hicho kilichopita. Kwa hiyo, kwa kuwa mmekwisha ikataa, *then definitely* hii inakuwa haiwezi ika-stand tena.

(Kifungu Kilichotajwa hapo Juu Kiliptishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON.
MIZENGO K. PINDA, THE PRIME MINISTER AT THE
SECOND READING OF A BILL ENTITLED**
“THE REFERENDUM ACT, 2013”

(Made under S.O. 86(10)(b))

The Bill entitled “The Referendum Act, 2013” is amended:

C: In Clause 5 by-

- (a) deleting paragraphs (a), (b) and (c) of subsection (1) and substituting for them the following:
 - (a) the period for sensitization and public awareness on the referendum for the proposed Constitution;
 - (b) the day on which the referendum is to be held; and
 - (c) the polling time of the referendum.”
- (b) deleting subclause (4) and substituting for it the following:

“(4) Without prejudice to subsection (3), the Commission may allow civil societies and non-governmental organisations which are interested in carrying out civic education or awareness programme on the

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

proposed Constitution to carry out civic education or awareness programme for a period of not more than sixty days prior to the voting date.

(5) A civil society or non-governmental organisation which has been allowed to carry out civic education or awareness programme on the proposed Constitution shall notify the Commission of the date, place and time within which it shall carry out civic education or awareness programme.

(6) Where the Commission refuses a civil society or non-governmental organisation to carry out civic education or awareness programme, the Commission shall state the reasons thereof.”

Dodoma,
....., 2013

M.K.P.P
WM

**SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON JOHN
JOHN MINYIKA MEMBER OF PARLIAMENT FOR UBUNGO
CONSTITUENCY AT THE SECOND READING FOR THE BILL
ENTITLED THE REFERENDUM ACT, 2013**

Made under standing order 86(11) and 88(2)

A bill entitled “ **THE REFERENDUM ACT, 2013**” is amended as follows:

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. JOHN J. MNYIKA]

B: In Clause 5 (4) between ‘than’ and ‘days’ delete the word “thirty” and replace with the word “sixty”.

.....
**JOHN JOHN MNYIKA (MP)
UBUNGO CONSTITUENCY
04.12.2013**

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kifungu cha (5), nilipendekeza kwa sababu kwenye Muswada ulivyo hivi sasa unasema Asasi za Kiraia, Taafisi na hayo makundi mengine yatakayotoa Elimu ya Urai, au kufanya uhamashishi juu ya Katiba, yatafanya hivyo kwa siku 30 kabla ya siku ya kupiga kura. Lakini wakati makundi mengine yakambiwa siku 30 kabla ya kupiga kura. Tume kwa upande wake yenye we inatoa elimu siku 60. *Process ya kutoa Elimu ya Katiba kwa Tume ni siku 60.*

Sasa tulivyopeleka kwenye Kamati, tulizungumza na Serikali ikasema kwamba itakwenda kufanya marekebisho, nilikuwa napitia Jedwali la Serikali ambalo limeletwa hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kadiri nilivyo lisoma, Serikali imekubali ya kwamba sasa Asasi za Kiraia na Makundi mengine yatakayoruhusiwa na Tume kutoa Elimu ya Katiba yatafanya hivyo kwa siku 60 badala ya 30 ilivyokuwa mwanzoni. Sasa kwa kuwa Serikali imekubali siku 60 nakubaliana na mapendekezo ambayo Serikali imewasilisha. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Wenje.

SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON EZEKIA
DIBOGO WENJE MEMBER OF PARLIAMENT FOR NYAMAGANA
CONSTITUENCY AT THE SECOND READING FOR THE BILL
ENTITLED THE REFERENDUM ACT, 2013

Made under standing order 86(11) and 88(2)

A bill entitled "The Referendum Act, 2013" is amended as follows:

C. In clause 5(4) deleting the word **may** and substituting it the word "shall"

.....
Hon Ezekia Dibogo Wenje(MP)
NYAMAGANA CONSTITUENCY

MHE. EZEKA D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho yangu yako kwenye hiyo Ibara ya 5 (4), na ni mapendekezo madogo tu ambayo, ninapendekeza neno "may", itoke na iwekwe neno "shall". Kwa hiyo, isomeke kama ifuatavyo. Kwamba: "*Without prejudice the provision Subsection (3) the Commission Shall.*" Halafu hapo tunatoa neno "may". "*Shall allow Civil Societies and Non Governmental Organizations which are interested in disseminating civic education, or carrying awareness campaign on the proposed Constitution to disseminate the education and carry on the campaign for a period of not more than thirty days prior to the Voting date.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza tutoe neno "may," tuweke "shall". Kwa sababu ukiweka neno "may", itakuwa ni *discretion*, yaani itakuwa ni kwamba wakiamua sawa, wasipoamua pia sawa. Lakini kuna umuhimu sana wa Asasi nydingine hizi pia ku-participate katika kutoa Awareness program katika kipindi hiki cha *Referendum*. Kwa hiyo, mimi

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. EZEKIA D. WENJE]

napendekeza tuweke neno “shall”, ili iwe ni lazima kwa hizi Asasi nydingine ku-participate katika kutoa hii elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo mapendekezo yangu kwenye Ibara hii.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Leticia.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nashukuru. Nami naomba nichukue nafasi hii kumuunga mkono Mheshimiwa Wenje kwa hoja yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii ina maana kubwa saba, ina mashiko. Kwa sababu tukiacha “may” maana yake itakuwa *optional*. Wanaweza waamue kufanya hivyo au wasiamue kufanya hivyo. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu amekuwa akituambia kwamba “may” *it is a silent shall*. Sasa leo naiomba Serikali itupe *a loud Shall*, kama ilivyo na siyo vinginevyo. *Other wise* itakuwa ni matatizo kushughulikia suala zito kama hili na kuwapa watu *option* ya kuamua maamuzi makubwa kama haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ikubaliane na hoja ya Mheshimiwa Ezekia Wenje. Ahsante.

MWENYEKITI: Shida yangu, mnapojenga hoja hamtoi uzito. Hamtoi uzito kum-*convince* mtu mwingine akaamini. Maana yake hapa *Civic Organizations*, zipi hiso? Si zile zitakazokuwa *interested?* Sasa inakujaje na “shall”. Muwe mnajenga hoja jamani. (*Makofii*)

MHE DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa hoja iko wazi, kwamba ikitumika “may”, itakuwa *discretion* ya Tume kushirikisha hiso Jumuia za kiraia au la. Ikiwa “shall”, itakuwa maana yake ni lazima ishirikishe kwenye kutoa hiyo elimu kwa ajili ya mchakato mzima huu wa Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ikubali kuweka “shall” ili kusudi tuwe na uhakika kwamba hizi *NGOs* zitashirikishwa kweli. Kwa sababu ikibaki “may” inaweza

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DAVID Z. KAFULILA]

zisishirikishwe na isiwe kosa. Lakini ikiwekwa "shall" maana yake ni lazima washirikishwe, na wasiposhirikishwa litakuwa kosa kisheria.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnayika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri suala hili Serikali itakapotoa majibu itoe na ulinganisho na Jedwali ambalo Serikali imefanya marekebisho. Nakubaliana na Mheshimiwa Wenje, kuna haja ya kutumia neno "shall". Utetezi wa Serikali wa kutaka kutumia neno "may" ni kwamba ukitumia neno "shall", Taasisi yoyote ile hata kama haijakidhi masharti utalazimika kuiruhusu. Kwa hiyo, huo ndiyo utetezi wa Serikali kwa kutumia neno "may". Kwa hiyo, ili kuwe na *discretion* ya kukataa au kukubali, basi acha hili wingu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza sana suala la kutokuaminiana. Kwenye Jedwali la Marekebisho ya Serikali, kuna kifungu kinachosema: "*Where the Commission refuses a Civil Society or Non-Governmental organization to carry out Civic Education or Awareness program, the Commission shall state the reason there of.*" Sasa *Commission* ikikataa itaieleza hiyo Taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo langu nillonaloo ndiyo maana naunga mkono neno "shall" liwepo, hakuna utaratibu wa rufaa, juu ya maamuzi yaliyochukuliwa ya kukatalia.

Unaweza ukanieleza sababu za kunikatalia kutoa elimu ya uraia, na hapa hatuzungumzii *NGOs* peke yake, tunazungumzia Taasisi za Dini, tunazungumzia sekta binafsi, tunazungumzia Taasisi nyengine yoyote itakayotaka kutoa elimu ya Katiba. Sasa hapa wakikataliwa, wanaelezwa sababu, hawana mahali popote pa kukata rufaa.

MWENYEKITI: Ni dakika tatu.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Kwa hiyo, kama Serikali itaweka utaratibu wa kukata rufaa, basi neno "may" linaweza likakubalika.

MWENYEKITI: Dakika tatu.

MHE. CHALES J. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nasimama kusudi niwatoe wasiwasi wenzangu kuhusu neno "may" na "shall". Ni kwamba iko hoja suala hili ni muhimu. Siyo kila mtu atakayekuja anataka kutoa elimu mumpe nafasi ya kutoa elimu. Sitaki kutoa taarifa ya Kamati yako, lakini tumeyaona. Mtu anakuja, anazungumza jambo ambalo halijui. Kwa hiyo, hii *Commission* muipatie nafasi imtathimini huyu mtu, asilolijua asiliseme, anayojua basi aruhusiwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi ni kwamba *NGOs* na watu wengine wataruhusiwa kusema. Lakini nani anasema? Unakwenda kusema nini? Kwa hiyo, nafasi ya "may", ibakie pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ndiyo hayo Mheshimiwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtutura.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niliiyotaka kusema ni hayo ambayo Mheshimiwa Mwijage sasa hivi ameyazungumza. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Serukamba.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naunga mkono pendekezo la Serikali la kuacha neno "may" kutokana na sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli huu mchakato wa Katiba ndiyo uhai wa nchi. Tukitaka leo hii Bunge lako Tukufu tuitipishe Sheria hii, turuhusu kila mtu aje wakati huo aseme anachotaka kwa sababu Sheria inaruhusu, tutapata taabu sana. Inaweza ikaja *NGO* ambayo kazi yake inakuja kufanya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PETER J. SERUKAMBAJ]

kazi moja tu, ya kuwaambia Watanzania kataeni hii Katiba, kwa sababu ambazo *it is known to him* na Chama chake. *Unless* watuambie wenzetu kuna NGOs wameziandaa kwa kazi hii, sasa wana wasiwasi zinaweza zisifanye kazi hii. Lakini kama ni hizi NGOs tunazozijua, bado naamini Tume hii itapata nafasi kuwaruhusu wafanye hiyo kazi. (*Makofii*)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Jambo la kwanza ambalo tungepashwa kujuliza, ni kwamba, nini malengo ya hizi NGOs? NGOs mbalimbali zimeanzishwa kwa sababu gani? Ukipita katika NGOs mbalimbali utakuta kwamba kwenye *objectives* zake wame-state kwamba wanaenda ku-deal specifically na mambo gani. Lakini pia ukija katika matumizi ya lugha, ni wazi kwamba matumizi ya hizi *auxiliary verbs* au *helping verbs* zina maana kubwa sana katika lugha ya sheria. Matumizi ya neno "may", inaweza isiwe ni lazima katika lugha. Lakini unapokuja kutumia neno "shall" ina maana ni *obligator*, ni *obligation*. Huwezi ukakataa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo tunajua kwamba kwa Msajili wa hizi Asasi za Kiraia, kwa maana ya NGOs, wengine wamejikita katika masuala mbalimbali ambayo yanajihuisha na masuala ya kijamii. Wameomba kwamba wao wanaona itakuwa ni vizuri waka-participate kwenye kuweza kufanya *sensitization* kwa wananchi. Kuna sababu gani pengine Serikali itueleze; kuna sababu gani? Kuna wasiwasi gani wa kusema kwamba ni kwa nini Tume isiwaruhusu NGOs, mbalimbali ambazo zimekuwa *interested* kwenda kufanya *sensitization* kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama watasema kataeni Katiba, ndiyo uhuru wenywewe. Ndiyo uhuru wenywewe wa Taasisi hizo na ndiyo pia tutakuwa pia tutakuwa sasa pengine tunaangalia hata uhuru wa mtu mmoja mmoja. Hakuna tatizo kwamba iwapo mtu atasema kataeni rasimu hiyo au kubalini rasimu. Inawezekana tukapata rasimu ambayo ni nzuri, wakasema jamani atakayekataa rasimu hii atakuwa ana matatizo yake binafsi.

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. MOSES J. MACHALI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale ambao wataona kuna matatizo wakisema kataeni siyo kosa vile vile. Kwa hiyo, tutumie neno "*shall*" ili kuhakisha kwamba kila kitu kinakwenda kama kiliviyotakiwa.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ukiangalia katika Ibara ya 5 (3) ya Muswada huu, majukumu au mamlaka kuhusiana na uelimishaji kwa elimu kwa Umma yamekasimiwa kwa Tume. Sasa unapokuja kwenye kile Kifungu cha (4) ambacho tumekifanyia marekebisho 5(4) kama ambapo Jedwali la Mheshimiwa Waziri linavyoonekana, ndipo sasa Tume inaweza kuziruhusu Asasi zisizokuwa za Kiserikali. Lakini inaziruhusu baada ya kuwa imetoa taarifa kwa Tume. Hili siyo mara ya kwanza. Hata katika mchakato wa kupokea maoni mbalimbali Tume ya Katiba pia kwenye Kifungu Cha 17(9) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ilikuwa na sharti hili. Lakini siyo hiyo tu, katika Jedwali hili ukiangalia Kifungu cha 5(6), Tume endapo itakatalia Taasisi mbalimbali kutoa elimu kwa Umma, itatoa sababu.

Kwa hiyo, tunaomba sana Waheshimiwa Wabunge, kwenye hili mlafiki. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Wenje, msemaji wa mwisho.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika hii Na.1 hakuna *process* ya rufaa. Kwa maana ya kwamba Tume labda ikikataa, ikakutalia, kwa sababu wanasema "*interested parties*". Unaweza ukawa *interested* na uka-*apply* na wakakukatalia, lakini hakuna *room* ya kukata rufaa. Hiyo ni namba moja.

Pili, kwa ile ile *spirit* ya nia njema, naishauri Serikali kwamba tunaweza tukatumia neno "*shall*", lakini hapo mbele in the same same subsection tukaongeza maneno: "*Upon fulfilling the required standard that will be set out by the Commission.*" Kwa hiyo, ikasomeka jumla sasa kwamba: "*Without prejudice the provision Subsection (3), The Commission shall allow Civil Societies and Non-Governmental*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. EZEKIA D. WENJE]

Organizations,” halafu mwisho huku tukamalizia: “Upon fulfilling the required standard.” Hiyo sasa natoa ombi kwa Serikali, kama wanaona kwamba hili ni tatizo kuweka neno “shall” peke yake *then* wao wanaweza kuongeza hayo maneno ili bado ikakidhi kwenye zile *stanrards*, kwamba mtu aki-*fulfil* zile *standards* ambazo Tume itaweka, *then* iwe *obligatory*kwamba aruhusiwe kuendelea ku-*disseminate* hiyo *information*.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, naomba mniunge mkono kwenye hili. Ni muhimu kwa hizi Asasi kutoa hii *awareness campaign*.

MWENYEKITI: Hayo maneno aliyoongeza mnasemaje? Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno aliyoongeza Mheshimiwa Ezekiel Wenje, hayaathiri maneno yale ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri amesema. Unajua hapa ni msingi kama wa *accreditation*. *Accreditation* haiwezi kuwa *compulsory*sasa unapo *fulfill*/zile *conditions* ... (*Hapa mitambo ya sauti illkorofisha*)

(Saa 12.50 jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Siku ya Ijumaa Tarehe 6 Desemba, 2013 Saa Tatu Asubuhi)